ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tano - Tarehe 9 Juni, 2016

(Kikao kilianza Saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 90

Mgomo Kisiwani Pemba

Mhe. Shehe Hamad Mattar: – Aliuliza:
Kwa kuwa kifungu cha 5 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 kinatambua Zanzibar kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Na kwa kuwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilitangaza kufutwa kwa Uchaguzi wa tarehe 30/10/2015 na kutangaza Uchaguzi wa marejeo tarehe 20/03/2016.

Na kwa kuwa kila mwananchi aliyetimiza masharti alikuwa na haki ya kupiga kura kuchagua kiongozi anayemtaka.

Na kwa kuwa baada ya Tume ya Uchaguzi kutangaza matokeo ya Uchaguzi wa marudio kisiwani Pemba, baadhi ya wafuasi wa Chama cha *CUF* wameanzisha migomo katika maeneo tofauti ya kisiwa cha Pemba kwa kutoshirikiana na wenzao katika masulala ya kijamii kama vile mazishi, harusi na kusalimiana, jambo ambalo linazalisha chuki miongoni mwa jamii.

a) Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi wanaoendeleza chuki hizi katika jamii.

b) Je, Serikali imechukua jitihada gani ili kuhakikisha wananchi wanashirikiana kwa pamoja katika kuleta maendeleo ya nchi bila ya kujali itikadi za vyama vyao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 90 lenye vipengele (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli mara baada ya kufanyika kwa Uchaguzi wa marejeo hapo tarehe 20 Machi, 2016, kumejitokeza baadhi ya wananchi kuanzisha migomo katika maeneo mbali mbali, kuwepo kwa vitisho kwa wananchi waliokwenda kupiga kura. Kuwepo kwa matukio ya migomo ya madukani na gari za abiria, kufanya uharibifu kwa kuchoma moto kwa mashamba ya mikarafuu, mihogo na minazi, nyumba za wananchi na maskani za CCM, pamoja na kuwekewa alama za **X** na kupigwa mawe baadhi ya nyumba za wana CCM wakati wa usiku hasa kisiwani Pemba.

Pia kumejitokeza mtindo wa kupiga bakora wana CCM ndani ya misikiti kitendo ambacho ni kinyume kabisa na msingi wa dini ya kiislamu.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar, swali lake Nam. 90 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali inakemea vikali matukio hayo yaliyoashiria uvunjifu wa amani na utulivu uliopo hapa nchini. Aidha, Serikali imejipanga kuhakikisha matokeo hayo yanadhibitiwa.

Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama vitachukua hatua kali za kisheria kwa wahusika wote, pahali popote pamoja na kuzifungia leseni la biashara kwa wale wanaofanya ubaguzi katika kutoa huduma za kibiashara.

(b) Mhe. Spika, Serikali inaendelea kuchukua jitihada na hatua mbali mbali ili kuhakikisha wananchi wanashirikiana katika kuleta maendeleo ya nchi. Jitihada hizo ni pamoja na:-

- Serikali kupitia vyombo vya ulinzi na usalama imeimarisha ulinzi na usalama katika maeneo yote nchini na kuimarisha doria za Polisi za usiku na mchana kwa Shehia zote.

- Viongozi wa Wilaya na Mikoa kufanya mikutano na wananchi husika ili kukataza aina yoyote ya mgomo na vitendo vya uvunjifu wa amani.

- Serikali imeagiza wananchi kuendelea na shughuli zao za maisha kama kawaida na yeyote atakayesababisha vurugu nchini atachukuliwa hatua kali za Kisheria.

- Uongozi wa Ofisi ya Makamu ya Pili wa Rais umefanya mikutano na viongozi wa ngazi ya Mikoa, Wilaya na Shehia zote za Pemba kujadili suala la hatua za kuchukuliwa katika kuhakikisha wananchi wanashirikiana na wanaishi kwa amani. Mikutano hiyo ilifanyika tarehe 30/04 hadi 2/5/2016.

  Aidha Mhe.Makamo wa Pili wa Rais amefanya ziara maalumu kisiwani Pemba kwa ajili ya kulitafutia ufumbuzi suala hili na bado linaendelea kutafakariwa ndani ya Serikali.

- Vikao mbali mbali vya Serikali vimekutana kulipatia ufumbuzi suala hili kwa ajili ya kuimarisha amani na utulivu nchini. Nataka niwahakikishie wananchi kuwa Serikali iko imara na hatua zinazofaa zitaendelea kuchukuliwa kuhakikisha amani na utulivu na umoja wa nchi yetu unadumu.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Waziri, kwa majibu yako mazuri na maelezo mazuri na matumaini kwa wananchi, nina swali la nyongeza.

Pamoja na hatua zilizochukuliwa, mikutano mbali mbali na wenye magari kuzuiliwa leseni, je, ni hatua gani iliyochukuliwa kwa wale ambao kuwa wamewadhulumu watu kwa kuwapiga, kuwavunjia mali zao na watu hawa wameripotiwa katika vituo vya Polisi, ni hatua gani iliyochukuliwa mpaka sasa ili sisi tuwe na amani tutakaporudi majimboni, tuone tunaweza kufanya kazi zetu kwa vizuri katika kuwatumia wananchi wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, naomba kumjibu Mhe. Mattar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Ni kweli kwa mtenda kosa yeyote yule hatua za kisheria zinabidi zichukuliwe kwa muhibu wa kosa lenyewe. Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya uchunguzi wa kina kwa wale wote ambao watakaothibitika kwa mujibu wa sheria, na baada ya kesi zao kupelekwa Mahakamani maamuzi ya kisheria yatachukua mkondo wake.

Hata hivyo sasa hivi vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinajipanga zaidi kuhakikisha kwamba matukio ya aina hii hayatokei. Na napenda nitoe wito kwa wananchi wote na hususan wazee kuwakataza watoto wao kufanya vitendo ambavyo vinaashiria uvunjifu wa amani, maana mpango kabambe umeandaliwa na Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama, kuhakikisha kuwa vitendo hivi havijirudii na wale wahusika wanatiwa mbaroni, na adhabu kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Mhe. Ali Suleiman Ali: (**Shihata**): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe.Naibu Spika, Katiba yetu ya Zanzibar au ya Muungano inasema tu kwamba kila mwananchi ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa kwa anayempenda. Kwa kuzingatia hayo pia na anayechaguliwa ana haki ya kuwatumikia wananchi bila ya ubaguzi. Swali langu liko hapa:

Kwa kuwa tatizo hili limejitokeza katika nchi yetu na Chama kinachohusika ni Chama cha *CUF*, vyama vya upinzani vyote viko kimya vinaunga mkono Serikali kwa kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Je, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania, imechukua hatua gani ya kupeleka hatua rasmi ya Serikali juu ya adha hii inayowakuta wananchi wetu hususan Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Shihata, swali lake zuri kama ifuatavyo:

Mheshimiwa kwa sababu sasa hivi Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama vinakusanya ushahidi wote wa kila siku wa kila tukio na kila inapotokea. Dhamira kubwa ni kwamba vile vyama ambavyo vinakwenda kinyume na amani na utulivu wa nchi, hatua za kisheria kwa kushirikiana na Msajili zitachukuliwa ili kuona vyama hivyo havina nafasi vya kuendeleza ama kuvunja amani ya nchi.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa bado vitendo hivi vinaendelea kisiwani Pemba, hata jana Masheha wangu wamekatiwa migomba yao na mikarafuu, bado

vitendo vinaendelea. Je, Mhe. Waziri, atachukua hatua gani ya dharura ili kukomesha vitendo hivi visiendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Makamo wa Pili wa Rais, naomba kumjibu rafiki yangu Mhe. Mussa, Mwakilishi wa Kiwani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa naamini ni kweli vitendo hivi vinavyoendelea vya kudhalilisha, kuhujumu, kuharibu vipando vya wananchi sio tu kinyume na sheria za nchi bali ni kinyume na matakwa ya dini, wanaofanya hivyo inaonekana wazi, hasa katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhan inaonekana kwamba hata hiyo dini wameiweka nyuma yao. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, dini inakataza kabisa kabisa kukata miti, kuharibu vipando ambavyo ni rizki ya mja alivyovilima kwa ajili ya maisha yake. Vitendo hivi si tu vinachafua jina zuri la Zanzibar lakini vinachafua amani ya nchi yetu. Ni vitendo ambavyo havina muda tena wa kuvumiliwa katika nchi yetu.

Kwa hiyo nataka nimuhakikishie Mhe. Mussa, kwamba vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika Jamhuri ya Muungano na Zanzibar vitachukua hatua zinazofaa kwa wale wote wanaoshiriki na vitendo hivi. Na mimi kama nilivyosema awali wazee na watoto wanaojishirikisha kwenye mambo haya ni vyema wakaacha mara moja kabla ya mkono huu utakaoendelea Unguja na Pemba kuhakikisha amani yetu inapatikana.

Mheshimiwa jambo hili linasitikisha sana sana, haiwezekani kukata vipando vya wananchi ambayo ni mategemeo yao ya maisha ya kila siku, sio tu unamkosa Mungu, unaikosa Serikali, unajitia katika matatizo, unachukua wakati wa bure kwenda kukata vipando, unapoteza muda wako na unapata tabu kwa sababu lazima utagundulikana, Serikali itakutambua, utahukumiwa na jela utakwenda.

La pili umeshamkosa Mungu adhabu kubwa juu yako mbele ya Mwenyezi Mungu, na tatu ile tabu unayoipata kwenda kukata vipando vya mtu mwengine havina faida yoyote kwako. Jambo la kusikitisha, ni ujinga wa hali ya juu!

Nam. 87

Tatizo la Kuwepo Wafanyakazi Hewa

Mhe. Suleiman Sarahan Said: – Aliuliza:

Mara kadhaa tumekuwa tukisikia kwamba kumekuwa na wafanyakazi hewa katika Mawizara mbali mbali na malipo yao kuelekea kusikojulikana.

a) Tatizo hilo kwa hapa Zanzibar limekuwa na ukubwa gani hivi sasa.
b) Ni sababu zipi zinazopelekea kuwa na wafanyakazi hewa hapa nchini.
c) Kwa nini Wizara ya Fedha isikae na kushirikiana na Wizara au Taasisi zinazohusika na kugundua tatizo hili kabla ya kupeleka malipo hewa kwa Taasisi hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 87 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Muwakilishi kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na utaratibu wa kufanya uhakiki na ukaguzi wa taarifa za wafanyakazi na orodha za malipo yao kila baada ya muda, kwa lengo la kuhakikisha kuwa wanaolipwa ndio wafanyakazi halali wa Serikali. Kwa mfano mnamo mwaka 1994 iliyokuwa Idara ya Utumishi Serikalini kwa kushirikiana na Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iliendesha zoezi la ukaguzi wa watumishi kwa Taasisi zote za Serikali Unguja na Pemba.

Mwaka 2007 kupitia Mradi wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma, Serikali ilifanya sensa ya Watumishi kwa ajili ya kujua idadi halisi ya wafanyakazi waliopo Serikalini na iwapo kuna wafanyakazi wasio halali.

Aidha, mwaka 2011 Serikali kupitia iliyokuwa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliendesha zoezi la Ukaguzi wa Watumishi na Orodha ya Malipo ya Mishahara (*Staff Inspection and Payroll Auditing)* ambapo

watumishi wote walitakiwa kujitokeza wao wenyewe katika vituo maalum vilivyoandaliwa kwa ajili ya kupokea mishahara yao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa muda mrefu umepita tokea mwaka 2011/2012 Serikali ilipoendesha zoezi la Ukaguzi wa Watumishi, si rahisi kueleza ukubwa wa tatizo hili la wafanyakazi hewa kwa sasa. Kinachoweza kuelezwa hapa ni kwamba, zoezi lililofanyika hapo kabla limesaidia sana kutoa uelewa juu ya suala hili. Aidha, zoezi hili litakuwa endelelvu, ili kuhakikisha kwamba Mawizara yetu yanakuwa na idadi sahihi na inayokubalika ya watumishi.

(b) Mhe. Spika, kwa ujumla sababu kadhaa zinazopeleka kuwa na wafanyakazi hewa. Miongozi mwa sababu hizo ni pamoja na:-

- Watumishi wanaoshughulikia malipo ya Mishahara ya Watumishi kutokuwa waaminifu;

- Kutoripoti kazi kwa watumishi wapya katika sehemu walizopangiwa, hasa katika Halmashauri za Wilaya na Madaraka Mikoani;

- Kutotolewa katika mfumo wa Malipo (*payroll system*) kwa watumishi wa umma wanaofariki dunia, wanaostaafu au kuacha kazi; na

- Wafanyakazi kuhamishwa kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyengine bila ya kufutwa ndani ya mfumo wa malipo katika taasisi aliyotoka.

(c) Mhe. Spika, kwanza nataka nimthibitishie Mhe. Mwakilishi kwamba Wizara ya Fedha inafanya kazi kwa mashirikiano makubwa.

Mhe. Spika, mbali na mashirikiano hayo ya jumla na Wizara na Taasisi za Serikali, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora nayo inafanya kazi kwa mashirikiano ya karibu sana na Wizara ya Fedha, hususan katika masuala ya mishahara ya watumishi wa umma. Ni vyema ikafahamika kwamba pamoja na kuwa na mfumo wa malipo ambao unadhibitiwa na Wizara ya Fedha, lakini maelekezo ya kuingiza malipo ya mishahara ya watumishi katika mfumo huo kutoka ofisi yetu ya utumishi.

Aidha, hivi sasa Ofisi yetu iko katika hatua za mwisho za kukamilisha zoezi la kuoainisha Mfumo huo wa malipo ya mishahara na kumbukumbu za Watumishi (*Human Resource Database*) zilizoandaliwa na Ofisi yetu ya Utumishi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyafafanua japo amesema kwamba kwa kipindi hichi bado hawawezi kutoa *data* kamili, lakini Mheshimiwa nina swali moja lenye (a) na (b).

(a) Wakati wa kufunga hesabu za mwaka za Serikali, inavyoonesha wanafunga hesabu za pesa tu hawafungi hesabu za matatizo mengine, kwa sababu kwa kila mwaka nina uhakika kwa kila wizara inawezekana kuna mtu ambaye anastaafu au anaondoka, lakini kwa mtindo wanaouonesha inaonekana kwamba hawafungi hesabu za kijumla, wanafunga hesabu za pesa. Kwa hivyo, nilikuwa namuuliza huu ndio mtindo ambao unatumika kufunga hesabu za pesa bila ya kuangalia maelekezo mengine.

(b) Wafanyakazi wanapokuwa wanahamishwa kwenda upande mwengine na likatokea kosa la kwamba mtu huyu mishahara inakwenda huku na huku, hatua gani anazichukua baada ya kutokea suala kama hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, katika masuala aliyoyazungumzia haya yanayohusu Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa hiyo, kwa heshima yako na kwa ruhusa yako ningeliomba hili akalijibu Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kama nimelisikia vizuri swali ni kwamba wafanyakazi wanapohamishwa kutoka idara moja kwenda idara nyengine huwa wanapata usumbufu wa mishahara yao. Nadhani hivyo ndivyo Mhe. Mwakilishi alivyoulizia.

Kwanza suala la uhamisho wa wafanyakazi ni utaratibu wa kawaida ndani ya serikali, kuhamisha mshahara ni suala ambalo halitakiwi kuchukua muda ni suala la kiutawala, na kama hiyo imetokea basi ni suala ambalo tutalichukulia hatua kuhakikisha kwamba mfanyakazi anapohamishwa kutoka idara moja kwenda nyengine basi na mshahara wake unahamishwa kwa haraka, ili kupunguza usumbufu kwa wafanyakazi hao.

UTARATIBU

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, swali ambalo nimemuuliza ni la kwanza. Nilimuuliza kwamba zinapofungwa hesabu za serikali kwa mwaka inaonekana zinafungwa hesabu za pesa tu sio hesabu za kuangalia majumuisho ya vitu vyote.

Mhe. Naibu Spika: Hebu uliza tena hilo swali lako, maana hatukulisikia.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, nilimuuliza kila mwaka tunafunga hesabu za serikali, inavyoonekana kwamba tunafunga hesabu za serikali za pesa sio za matukio yote kujua kwamba tutakuwa na wafanyakazi wangapi. Kwa hivyo, ndio ikawa sababu kubwa ya kusababisha kuwa na wafanyakazi hewa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimtoe wasiwasi Mhe. Mwakilishi kwamba kumefanyika ukaguzi wa wafanyakazi mara nyingi tu, na ukweli kwamba sisi tumeanza mwanzo kuliko hata Tanzania Bara katika kukagua wafanyakazi wetu kwa ajili ya kugundua wafanyakazi hewa. Ulifanyika mwaka 2009, ulifanyika mwaka nadhani 2011/2012, na kwa wakati huo wafanyakazi hewa waligundulika kwa upande wa Pemba na hatua zilichukuliwa. Lakini hivi karibuni pia Ofisi ya Mdhbiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali naye alifanya ukaguzi lakini hakukugundulika kasoro, kasoro iliyogundulika ni kwamba wafanyakazi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali walikuwa ni wafanyakazi wa kada ya ulinzi wa maskuli, mishahara yao haikutoka katika kifungu kinachostahiki. Kwa hivyo, bado tatizo la wafanyakazi hewa kwa Zanzibar sio tatizo kubwa kama linavyofikiriwa.

Pamoja na hayo, kila mara tunapobadilisha mishahara basi pia tunafanya kazi hiyo ya ukaguzi kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikalini, ili kuhakikisha kwamba hakutakuwa na wafanyakazi hewa katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana naomba niongezee majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha, muulizaji anataka kujua kwamba serikali inapofunga mahesabu yake ya mwaka, je, inafunga kwenye fedha tu au na mambo mengine.

Kwa utaratibu wa sheria ya fedha kila mwisho wa mwaka wa fedha hesabu zinazofungwa ni za fedha, hazifungwi hesabu za vitu vingine. Pesa zilizopitishwa na Bajeti ya Serikali ukifika mwisho wa mwaka useme ni kiasi

gani kimetumika, kiasi gani kimebakia ndio utaratibu wa serikali. Kwa hivyo, haya mambo mengine ya utumishi na mengine hayamo katika kufunga hesabu za serikali, hesabu za serikali zinafungwa kwenye fedha tu. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Naibu Spika ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nipongeze tu kwamba maji haya ya wizara hii yamepata Waheshimiwa Mawaziri wa kuongeza nguvu na kutoa taarifa sahihi, lakini pamoja na hayo naomba kuuliza swali.

Mhe. Nabu Spika, katika vipindi vinne Mhe. Waziri alitueleza kwamba palifanyika ukaguzi wa wafanyakazi hewa, lakini bahati nzuri alipokuja Mhe. Waziri wa Fedha akasema kwamba hawakuwagundua katika miaka hiyo, lakini sasa wakati unabadilika na miaka inakwenda. Hivyo, haoni kwamba sasa hivi ujanja umezidi wa kuwa na wafanyakazi hewa kuliko huko nyuma tunakotoka. Wizara ina mpango gani wa kuliangalia hilo kwa makini, ili kutatua tatizo hili hasa ukiangalia watu wanaokufa hawaingizwi katika ulipaji wa mishahara katika maeneo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, serikali inaelewa uzito wa tatizo hilo, na kwa taarifa tu ni kwamba kipindi hiki tunachoendelea nacho ambacho kinaelekea kubadilisha ile mishahara ya wafanyakazi wa SMZ. Kazi hii itafanyika ipasavyo kabla ya kuingiza au kulipwa huo mshahara mpya wa wafanyakazi wa SMZ. Kwa hivyo, suala hili linaendelea kufanyika, kuhakikisha kwamba mishahara mipya itakayokuja hakuna mfanyakazi yeyote wa serikali atayelipwa fedha ambayo hastahiki kulipwa.

Nam 20

***ZIPA* Inalindaje Wawekezaji**

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:

Kwa kuwa *ZIPA* ndiyo Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi Zanzibar.
Je, ni utaratibu gani unaotumika na *ZIPA* katika kulinda maslahi ya wawekezaji wa nje na wa ndani ili wawe Mabalozi wazuri wa nchi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:
Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 kama ifuatavyo:-

Msingi wa kulindwa mali na maslahi au haki katika mali ya mtu yeyote upo katika Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kifungu cha 17 cha Katiba hiyo kinakataza kuchukuliwa kwa nguvu mali au maslahi au haki ya mtu yeyote.

Kifungu pia kinaweka masharti iwapo ni lazima mambo hayo kuchukuliwa. Miongoni mwa masharti hayo ni kuwa uchukuaji huo uwe ni muhimu sana kwa ajili ya ama ulinzi, usalama wa wananchi, mazingira ya afya, kuimarisha maendeleo ya upangaji miji au kuendeleza mambo yoyote yatakayoleta faida kwa wananchi kwa ujumla wake. Hata hivyo, Katiba pia imeweka sharti kuwa umilikaji na uchukuaji huo ufanyike kisheria na kwa kutolewa fidia inayolingana.

Mhe. Naibu Spika ni dhahiri kuwa Mali, Maslahi na Haki za Wawekezaji, kama ilivyo kwa watu wengine, zinalindwa dhidi ya uchukuaji wake na sheria mama ya nchi kwa maana ya Katiba.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Wawekezaji wa nje na hata wale wa ndani, Maslahi, Haki na Mali za Wawekezaji yanalindwa pia chini ya Sheria ya Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi Nam. 11 ya mwaka 2004. Kifungu Nam. 22 ni makhususi kwa madhumuni hayo, na kinafanya marejeo kwa kifungu cha 17 cha Katiba kama nilivyoeleza hapo awali. Kifungu pia kinaweka masharti kuwa ikiwa ni lazima Mali, Maslahi, au Haki kuchukuliwa, waziri anayesimamia vitega uchumi atalazimika kutoa amri katika Gazeti la Serikali, Mali, Maslahi au Haki hiyo kutiwa thamani na fidia ya kutosha ilipwe.

Mhe. Naibu Spika, zaidi ya hayo, wawekezaji wanalindwa kupitia mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaiheshimu na kuitekeleza mikataba hiyo. Miongoni mwa mikataba muhimu ni ule wa Shirika la Kudhamini Uwekezaji *(Multilateral Investment Guarantee Agency – MIGA)* iliyo chini ya Benki ya Dunia.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Jaku kaa kwanza nitakupa swali la pili, muache mwenye swali la msingi aulize swali la nyongeza. Mhe. Simai Mohamed Said.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ningependa kumuuliza swali langu moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Kwanza *ZIPA* imekuwa ni taasisi ambayo serikali imejenga matumaini makubwa sana katika wawekezaji wetu wa ndani na nje, na kwenye Mpango Mkuu wa Serikali, MKUZA ametaja kwamba ni utalii, biashara na huduma ambayo ni *tourism, trade and services.*

(a) Je, Mhe. Waziri akiwa yeye ndiye kiongozi mkuu ambaye anailinda hii taasisi na kuiendeleza kwa kuwa sasa wawekezaji wengi wa nje wanakosa matumaini na *ZIPA*, kama vile kwenye mpango uliopangwa kuwa *ZIPA* iwe *One Stop Center* na inaelekea sasa imekuwa ni eneo ambalo wanalikacha, wanakwenda kwa ajili ya ku-*renew* leseni zao pamoja na kutafuta barua za *working permits*. Je. yeye mwenyewe kama Mhe. Waziri atafanya njia gani ya kurudisha matumaini ya wawekezaji wa nje ili waweze kupata ile huduma ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga kwa ajili yao.

(b) Kwa ajili ya wawekezaji wa ndani ambao ni wazalendo ni hatua gani au taratibu ambazo wamepanga kuwasaidia wawekezaji hawa ili waweze kufunga mikataba mikubwa zaidi na wawekezaji wa nje ambao tunawaita *joint venture*, lakini pia kutoa ile elimu ya biashara, ili na wao watoke pale walipo na waweze kufikia katika viwango vya kimataifa na hatimaye kuongeza kipato cha nchi yetu. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza hatujapokea malalamiko juu ya utendaji wa kazi wa *ZIPA.*

Sasa kama yapo malalamiko hayo ningemuomba Mhe. Mwakilishi tukawasiliana ili tukajua hasa kitu gani kinalalamikiwa. Lakini jukumu la *ZIPA* kama alivyokwisha kulisema ni kushajihisha uwekezaji wa ndani ama wa nje, lakini pia kuidhinisha miradi na baada ya kuidhinisha miradi hiyo *ZIPA* inatoa hati, lakini pia inaielekeza kwa maana anaelekezwa waziri anayehusika na masuala ya ardhi kwa ile miradi inayohitaji ardhi kuweza kupatiwa huduma ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji huo.

Pia sheria ya *ZIPA* Nam. 11 ya mwaka 2014 iko wazi kabisa, maslahi anayostahiki, zile haki anazostahiki mwekezaji ziko wazi, likiwemo hili suala

la kulindwa mali yake, lakini vile vile uwezo wa kusafirisha au kuhaulisha fedha kupeleka kwenye *account* zake za nje.

Vile vile fursa nyengine za kuhakikisha kwamba anaweza kuajiri wataalamu hizo haki zote zipo kwa mujibu wa sheria. Sasa kama kuna malalamiko nitamuomba Mheshimiwa anijuilishe malalamiko hayo, lakini naamini kwamba *ZIPA* inatekeleza shughuli zake kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

La pili, wawekezaji wa ndani zipo taratibu nyingi, na hata ukitizama MKUZA ambao ndio tunaoutekeleza sasa hivi kuna suala zima la kushajihisha wawekezaji wa ndani kuwekeza katika sekta mbali mbali za kutoa huduma na za kiuchumi. Sasa ni sekta binafsi yenyewe nayo kujitutumua kushiriki katika ile miradi ambayo ipo na fursa ambazo zipo, lakini kile kitu kiko wazi, na naamini kabisa Mhe. Mwakilishi anaelewa hivyo kwamba serikali katika moja ambayo tunayatilia mkazo ni kuweka mazingira bora ya kibiashara yatakayowasaidia wawekezaji wa ndani kuweza kuwekeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana nami nimshukuru sana Waziri wa Fedha na Mipango kwa umakini wake wa hali ya juu, na uwezo wake wa kujibu maswali ya msingi na nguvu ya hoja.

Mhe. Waziri nakubaliana naye alipokuwa akijibu swali la nyongeza kuwa *ZIPA* iko makini katika kutekeleza majukumu yake, ni kweli kabisa, mimi nimeiona na niwashukuru sana viongozi wa *ZIPA*. Lakini kuna baadhi ya taasisi hasa taasisi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kumekuwa na usumbufu wa kufanya mazoezi ya kupanda ngazi na kushuka bila ya mtu kutaka kufanya mazoezi kwa miaka ama miezi kupata haki yake.

Je, Mhe. Waziri anatoa kauli gani kulitaja suala la hati. Ushahidi kamili mimi ninao, mtu kawekeza lakini mpaka leo *lease* yake hajapewa, ikiwa mwekezaji wa ndani hali hiyo wa nje atakuja kweli?

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa jinsi ya kupata ardhi uko wazi kwa mujibu wa sheria, na kama nilivyosema mwanzo kwamba ikitoka *ZIPA* wakitoa hati kwa maana ya kwamba wameidhinisha ule mradi, basi *ZIPA* inamuandikia waziri anayehusika kuwa tayari hati amepewa waziri.

Sasa kwa mujibu wa kifungu nafikiri cha Sheria ya Ardhi 46(3), yeye baada ya kuridhika anatoa sasa hati ya ukodishwaji wa ardhi baada ya kupitia *ZIPA*. Sasa kwa muda mrefu mimi sijasikia tatizo hilo, lakini waziri anayehusika na ardhi

yupo, na naamini kama kweli kuna urasimu huo baada ya kufuata sheria kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa basi Mhe. Waziri amelisikia na atalichukulia hatua, kama upo urasimu wa namna hiyo. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, basi kwanza madhali waziri yupo anataka kujibu muache aendelee kujibu kwanza, ningesikiliza majibu ya waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na mimi naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi katika maelezo ambayo Mhe. Waziri wa Fedha ameyatoa niongezee tu kwamba kweli alichosema Mhe. Waziri wa Fedha, naungana naye ni sawasawa taratibu na sheria zipo. Lakini kwa sasa hivi naomba niseme wazi Baraza hili lielewe, na wananchi pia waelewe, kwamba sasa hatujasaini hati za ukodishwaji wa watu wa nje za *lease* kutokana na madudu mengi yaliyokuwepo. Kwa hiyo, tunafanya uhakiki wa kutosha.

Tunafanya uhakiki na kuhakikisha kwamba tumeridhika na yale ambayo tunayaangalia. Basi hakuna sababu ya mtu kutoa kupewa *lease* yake. Lakini ukiona kumechelewa maana yake kuna tatizo ambalo halijakamilika na bado tuna wasi wasi nalo. Naomba kutoa taarifa. (*Makofi*)

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu, kuhusu utaratibu kifungu cha 37 kinasema kwamba:-

> **37.** (1) Waziri, au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi. Isipokuwa kwamba, swali aliloulizwa Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine au na Mwanasheria Mkuu.

Naomba kidogo niongeze sauti yangu mnajua mwezi mtukufu huu.

Mimi sizungumzi kwa kuja kubahatisha ninachozungumza nakisimamia na hicho kitu kimeshafanyika na muwekezaji keshajenga, na waziri kama atakuwa tayari nimshauri na hivi sasa serikali inakosa mapato kutokana na *lease* imeshaandikwa iko tayari, na kitu kiko wazi mtu kanunua shamba la mtu, *lease* tu kusainiwa na hayo uzoefu umetokea kwa Mhe. Waziri aliyekuwepo ilifika

miaka miwili watu wanaambiwa hati nilizikuta kama hapo kutoka chini mpaka hapa mpaka nikaja kuulizwa swali kwenye Baraza ndio zikasainiwa hati.

Kwa hiyo, waziri hili lipo litafute, muwekezaji yupo, mimi huu mwezi wa Ramadhani nauheshimu, *lease* zimeshaandikwa bado kusainiwa sijui kalamu haijapatikana kusaini ni hilo Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, Mheshimiwa nimemsikia lakini bado tutaendelea kufuata utaratibu, na unaposaini hati hiyo ya ukodishwaji maana yake lazima uridhike. Kwa hiyo, hata kama zitakuwa zimejaa ofisini kwangu au kama utaratibu ambao anasema lakini lazima ujiridhishe kwamba hii ni hati, hata kama mtu kajenga, lakini hutoweza kuingia katika migogoro ambayo si ya lazima.

Kwa hiyo, mimi naomba atulie, aendelee kutulia na hakuna mtu atakayekosa haki yake na kila mwenye haki yake atapata muda ukishafika. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa *spirit* ambayo Mawaziri wetu wameanza kuionesha kwa kuweza kuona ni namna gani zile changamoto wanazikalia kitako na kuweza kuzirekebisha.

Kama alivyosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub katika suala zima la urasimu wa upatikanaji wa hati lakini vile vile na *lease*. Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Waziri wa Ardhi kwamba hapo nyuma kwa kweli kulikuwa na madudu mengi ambayo yalikuwa hayapendezi, na wawekezaji walisumbuliwa sana mtu tayari hati anayo hata bila ya kupewa ile *notice* ya miezi mitatu kwa mujibu wa sheria, na yeye akaweza kujieleza matokeo yake utakuta hati yake ilifutwa na wakapewa watu wengine ambao si wawekezaji. Kwa hiyo, ina maana ile ardhi imetulia.

Kwa kuwa kuna baadhi ya wawekezaji wameshahangaika kwa muda mrefu na wameshatumia *resources* nyingi kwa ajili ya kutaka kuwekeza. Je, labda kuna *time frame* ambayo Mhe. Waziri ameiweka labda katika kuweza ku- *facilitate* hawa ambao tayari wana *documents* zao ambazo zilifutwa kinyume cha sheria. Labda anaweza akanipa kwa muda gani wanaweza wakashughulikiwa haya masuala yao, ili wakaweza kuwekeza na tukaweza kuongeza ajira na kuongeza mapato ya ndani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, nakubali na hicho alichokizungumza lakini wizara yangu imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba haki ya mtu haitopotea, na mimi naomba tu nimtake kama

wapo ambao wanahisi wana usumbufu kuna kitengo chetu cha sheria mimi naomba aje pale afisini, lakini kuna kitengo cha ardhi na kama wanaona kama hawakuridhika mimi nipo kwa ajili ya wananchi.

Kwa hiyo, mimi naomba pia wafuate utaratibu kama watakuwa wanaona hawajahudumiwa vizuri basi wanifuate tu nafikiri tutakaa pamoja, tutashauriana na tutaweza ku-*solve* hizo *problems* ambazo zipo. Lakini bado naendelea kusema kwamba tutatoa hati kwa mujibu wa utaratibu na kwa mujibu wa sheria zilizopo. Ahsante.

Nam. 70

Tatizo la Upatikanaji wa Maji eneo la Tomondo

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): - Aliuliza:

Kwa kuwa lengo la serikali ni kuwapatia wananchi wake maji ya uhakika na salama.

Je, ni sababu gani zinazoendelea katika eneo la Tomondo maduka saba kwa kuchimbwa kisima kiasi cha miaka saba na kuendelea mpaka sasa hakitoi maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 70 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, eneo la Tomondo ni miongoni mwa maeneo yanayopata huduma ya maji safi na salama kupitia kisima cha Kwarara. Hata hivyo, kutokana na ongezeko la mahitaji linalochangiwa pia na ongezeko la watu hali ambayo inapelekea huduma ya maji safi na salama iwe haipatikani vizuri.

Mhe. Spika, hivyo Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na jitihada mbali mbali za kuwapatia wananchi wa maeneo hayo huduma ya maji safi na salama ikiwemo eneo la Tomondo. Miongoni mwa jitihada hizo, ni pamoja na ile ya kuchimba kisima katika eneo la Tomondo (Ziwa Maboga) kupitia mradi wa uchimbaji wa visima unaofadhiliwa na Mtawala wa Ras-al-Kheimah. Kukamilika kwa mradi huo kutaweza kutatua tatizo linalowakabili wananchi wa Tomondo pamoja na maeneo jirani.

Hivyo, Wizara yangu inamuomba Mhe. Mwakilishi na wananchi wa eneo hilo na maeneo ya jirani kuwa wastahamilivu wakati jitihada za kulipatia ufumbuzi tatizo hilo zinaendelea na kutoa mashirikiano yao katika uendelezaji wa visima hivyo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kwa kuwa kisima hichi kilichimbwa zamani sana, na kwa kuwa kimezungukwa na magugu mengi sana mpaka sasa.

(a) Huoni kuendelea kukiweka katika hali ile ni kupoteza pesa za wafadhili ambao wanatusaidia kwa nia njema.

(b) Kwa sababu hiyo hiyo, na kwa kushindwa kwa Mamlaka ya Maji kukiendesha kisima kile, huoni kama serikali inaanza kuwadharau wananchi walio wengi katika Shehia ya Tomondo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza nikubaliane kwamba kile kisima kipo lakini si muda mrefu kama ambavyo kaainisha, na hili linatokana kwamba kuna tatizo pale na mmiliki wa maeneo ya miti na *ZECO*. Lakini nafahamu kwamba *ZECO* na *ZAWA* wote wamo katika wizara yangu. Sasa si vizuri kabla ya kulimaliza hili tukaingia na huku.

Lakini hata hivyo, tumo katika jitihada za kuhakikisha kwamba harakati zote zinakamilika ya kukifunga kile kisima na kutoa huduma kwa wananchi. Aidha kwa njia kama mahakama itaamua ana itaamua kwengine, basi kutakuwa na njia mbadala ya kulifanya hilo tatizo litatuke kuwapatia wananchi maji.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kwa kuwa huu ni mwezi mtukufu wa Ramadhani wananchi wa kijiji cha Kiuyu Minungwini hivi sasa kisima ambacho kinasambaza maji katika Shehia ya Kiuyu Kigongoni na Shehia ya Kiuyu Minungwini kimeharibika.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuweza kuwasaidia wananchi wa kijiji hichi katika kipindi hichi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani, kama mnavyosaidia katika Shehia nyengine hapa Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze kuona na kuzijua jitihada za *ZAWA* katika kusaidia wananchi wake.

Pili ni vyema baada ya kutokea tatizo si kwa Kiuyu tu Minungwini, bali na kwa eneo lolote kutoa taarifa haraka kwa *ZAWA*.

Tulitoa tangazo juzi kwamba *ZAWA* itahakikisha kila Shehia ambazo hazipati maji basi yanapatikana. Lakini tulisisitiza sana Masheha watoe taarifa hizi kwa sababu ndio wanaokaa katika Shehia. Sasa ni jukumu la Shehia katika eneo la Kiuyu kutoa taarifa sahihi kwa *ZAWA* na sisi tukachukua hatua za haraka kupeleka maji si Kiuyu tu bali popote pale katika Unguja na Pemba. Ahsante sana.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu cha 59 (3).

> "Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani, atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatishatu, na Spika au Mjumbe mwengine yeyote anawezakumtakaMjumbe huyo anayesema atoe uthibitisho wa usemi wake unaohusika".

Hivi sasa wananchi wa Michamvi tokea dunia kuanza mpaka hii leo hawajapata maji tokea dunia kuanza mpaka leo hawajapata maji, anayehangaika ni Mwakilishi kupeleka gari la maji kule mnawaambia nini watu wa Michamvi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa hiyo si kuhusu utaratibu, kwa sababu umesema suala jengine, umeuliza suala lako wewe mwenyewe binafsi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ni kanuni si yangu mimi mwenyewe ni kanuni hii.

Mhe. Naibu Spika: Haina maana hiyo Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hii ni kanuni wala si msahafu, ni kanuni tuliyopewa ndani ya Baraza Mheshimiwa. Kanuni hii .

Mhe. Naibu Spika: Sawa lakini haina maana. Nisikilize basi na mimi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sawa ni kanuni hii sitaki nibadilishe sauti yangu mwezi wa Ramadhani huu. Basi tuendelee.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei): Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa serikali ina lengo zuri la kuwapatia wananchi wake maji safi hususan wa vijijini. Wananchi wangu wa kijiji cha Mgogoni na Misufini jimbo la Wawi Pemba ni muda mrefu sasa hawapati maji haya safi na salama.

Unataka kunihakikishia vipi wananchi hawa watapata maji haya safi na salama kupitia Serikali yao ya Mapinduzi Zanzibar kwa vile katika maeneo yao visima vipo tatizo ni mashine ya kusukuma maji tu. Ni lini utawapatia mashine hizo za kusukuma maji, ili maji safi yaweze kufika katika vijiji hivi vya wananchi wangu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, jukumu la msingi la wizara yangu kupitia *ZAWA* ni kuhakikisha kwamba tunafanya jitihada iwezekanavyo kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama, na kama inavyojulikana kwamba katika visima tunatia mashine na hivi vinaharibika kila wakati, na hatuchoki katika kufanya jitihada za kuhakikisha kwamba maji yanapatikana kama ulivyokuwa umekiri kwamba huna uhaba wa visima bali ni tatizo la mashine, ni vitu vya kununua, tutajipanga *inshaallah* utapata maji.

Nam. 115

Ukosefu wa Maji kwa Wananchi wa Kijiji cha Chole–Kengeja

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada zake za kusambaza huduma za maji kwa wananchi wake wa Zanzibar hadi kufikia asilimia 87 kwa mijini na asilimia 70 kwa vijijini. Hata hivyo, kwa upande wa kijiji cha Chole – Kengeja kwa muda mrefu pamoja na kuwa mabomba yameshazikwa kwenye ardhi lakini maji hayapatikani.

(a) Je, Mhe. Waziri swali hili analijua.

(b) Kama analijua ni kwa sababu gani wananchi wa kijiji cha Chole - Kengeja hawapati maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-
Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 115 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, Chole ni miongoni mwa vitongoji vilivyomo katika kijiji cha Kengeja, kimsingi kitongoji hiki kinapata huduma ya maji kutoka katika kisima

kiliopo katika maeneo ya Skuli ya Kengeja. Wizara yangu inajua kwamba hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika kitongoji hicho si ya kuridhisha kutokana na uwezo mdogo wa kisima kinachotumika kwa sasa, hata hivyo Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji tayari imeshachimba kisima katika maeneo ya Matangi Makongwe Kengeja ili kuongeza wingi wa maji katika maeneo ya Kengeja na vitongoji vyake, kwa hivi sasa hatua za uchimbaji wa kisima hicho zimekamilika na kazi ya ulazaji wa mabomba inaendelea. Kukamilika kwa kisima hicho kutawawezesha kijiji cha Kengeja na kitongoji cha Chole kupata huduma ya maji safi na salama kwa wingi. Ahsante.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kisiwa cha Chole kwa muda mrefu sana zaidi ya miaka minne bado hakipati maji, na kwa kuwa wakati huu tulionao ni mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Je, Mhe. Waziri haoni iko haja ya kufanya alau mgao kwa kipindi hichi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inaona haja hiyo, lakini pia kwa vile kazi iliyobakia sio kubwa sana ya kumalizia hichi kisima ningeomba tuonane baadae ili tukaambizana kuona namna gani tutaweza kukamilisha ili wakapata maji wananchi kwa uhakika.

Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira): Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake. Lakini katika majibu yake amekiri kwamba kisima cha Skuli ya Kengeja kina uwezo mdogo wa kusambaza maji katika maeneo hayo ya Chole. Vile vile amesema kwamba kisima kikongwe cha Mjiweni Kengeja wanachimba kisima kwa ajili ya kusambaza maji, lakini kisima kile ni cha zamani na matanki ya maji yaliopo pale makongwe.

Je, wana mpango gani kuhakikisha wanaweka tangi jipya ili kuweza kusambaza maji katika maeneo ya kijiji cha Kengeja yakiwemo Makunguu, Msalani, Mkumbi, Dikoni ili na kikiji hicho cha Chole ili kuondoa tatizo la maji katika kijiji cha Kengeja.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, hoja si kwa kuwa kitu kikongwe ili mradi tu kwa vile kitakuwa kinatumika safi na kwa maslahi ya matumizi ya binaadamu, lakini pia tunazingatia ushauri wake, tukiona ipo haja hiyo basi tutalitengeneza, kwa sababu tupo kwa ajili ya wananchi, lakini kama bado yanatumika kwa maslahi ya wananchi basi wawe nayo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hidaya.

Mhe. Maryam Thani Juma: Mhe. Naibu Spika, ninaitwa Maryam Thani Juma. Ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Kuna vijiji hivi Taifu ambacho kina mabonde linaloitwa Kuungoni ulipita upitishwaji wa kuchimba visima vya maji na katika uchimbaji wa visima hivi walipitisha barabara ambayo iliathiri mikarafuu pamoja na vipando vya wananchi.

Je, Mhe.Naibu Waziri ni kampuni gani ambayo ilishiriki kuchimba visima hivyo.

(b) Je, wananchi walilipwa fidia zao katika upitishaji wa kuchimbwa visima hivi.

Mhe. Waziri Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe.Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

a) Kweli sisi kama wizara tunachimba visima katika maeneo, na wakati tulichimba visima kwenye maeneo ambayo serikali imeyatambua. Lakini upitishwaji wa barabara ilikuwa ni kampuni nyengine na *ZAWA* ilisimamia kuchimba visima. Ninazungumza hivyo kwa sababu Taifu Kuungoni ninajua visima wapi vipo.

(b) Na sina uhakika naomba nimwambie kwamba sina uhakika kwamba wale walipojenga barabara kwamba walilipwa au hawakulipwa, lakini wenye sekta yao baadae wanaweza kutoa taarifa husika.

Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Nam. 97

Kulipwa Fidia kwa Wananchi wa Jimbo la Mgogoni

Mhe. Shehe Hamad Mattar – Aliuliza**:-**
Kwa kuwa kulipwa fidia ni haki ya kila mwananchi ambaye mali yake anayoimiliki kihalali inapochukuliwa na Serikali.

a) Je, ni lini wananchi ambao waliathirika katika ujenzi wa barabara inayotoka Wete – Konde, Mzambarau Takao – Finya, Mzambarau Karim – Mapofu kwa kubomolewa nyumba zao, kung'olewa vipando vyao, au kuathirika kutoka hatua za mwisho za ujenzi wa barabara watalipwa fidia zao ilhali Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein alishaagiza katika mkutano wake wa wananchi uliofanyika katika viwanja vya Ukunjwi Gando, Pemba.

b) Je, ni lini Serikali itaweza kuwaondolea tabu wananchi na hasa wanafunzi baina ya kijiji cha Kivuugo na Mtakuja Wingwi na vijiji jirani ambao wanahitaji kujengewa daraja katika bonde ambalo limekuwa ni kikwazo kupitia hasa wakati wa mvua kunakopelekea kuzunguka masafa marefu eneo la Maangwi na wanafunzi wa skuli ya Njuguni na Michungani Pemba kuchelewa masomo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 97 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utaratibu wa malipo wa fidia katika barabara ni kama hivi ifuatavyo:-

Ulipaji wa malipo kupisha eneo la barabara kuanza (*corridor*) na malipo yanayotokana na maharibiko ya nyumba baada ya barabara kumalizika.

Malipo yote ya majumba na vipando kwa barabara hizi za Mzambarautakao – Finya na Mzambaraukarim – Mapofu tayari yameshalipwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa barabara ya Wete – Konde malipo ya nyumba kupisha ujenzi wa barabara tayari yameshafanyika, lakini kwa malipo ya vipando kwa barabara hii bado hayajafanyika. Hata hivyo Wizara ya Ujenzi inalifahamu hilo na iko katika utaratibu wa kuwalipa wahusika.

Kwa zile nyumba ambazo ziliharibika baada ya ujenzi wa barabara kukamilika, Wizara inalifuatilia kwa karibu suala hilo kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwasogezea wananchi wake huduma ikishirikiana na Taasisi zake.

Hivyo Mhe. Naibu Spika, kwenye swali lake la pili napenda kumjibu kama ifuatavyo. Barabara za vijijini ziko katika Halmashauri za Wilaya. Hata hivyo Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji mara zote huwa inatoa mashirikiano makubwa, ushauri na msaada pale Wizara husika zinapokuwa na shughuli zake za maendeleo katika kuhakikisha wananchi wanafaidi matunda ya Serikali yao Tukufu.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Ninamshukuru Mhe.Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

a) Katika jibu lake alisema kwamba malipo ya nyumba yameshafanywa kwenye barabara hizo alizozitaja na bado malipo ya vipando. Lakini kama malipo haya yameshafanywa nisingeliweza kulileta suala hili. Kampuni zinazohusika zilisema kwamba zitalipa baada ya kumalizika barabara.

Je, yeye hajui kwamba mpaka leo kuna nyumba ambazo zimeathirika katika hatua za mwisho kujenga. Ni lini zitalipwa nyumba hizi.

b) Suala la barabara alisema Mhe. Naibu Waziri kwamba wizara yake inashirikiana na Halmashauri katika ujenzi pale inapofika wakati. Je, ataniahidi vipi kwamba utakapofika wakati wa Halmashauri kujenga barabara hiyo ambayo inayo madaraja kwenye jimbo langu hilo ataweza kutoa msaada wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la (a) kama ifuatavyo kabla sijamjibu la (b).

a) Ni kweli tunakubaliana kwamba baada ya ujenzi wa barabara kuna nyumba zimeathirika, na kama nilivyosema mwanzo. Mwanzo tulilipa zile nyumba ambazo tumepitisha ile barabara na tunajua kwamba tunadaiwa pale pesa zisizopungua milioni mia moja na thamanini na nne nukta tisa(184.9). Na kweli tushaanza kufanya utaratibu na baadae tunaanza kuzihakiki na kuwapelekea Wizara ya Fedha kwa ajili ya malipo.

Kwa hivyo tunakubali kwamba hizo fedha tunadaiwa, si fedha hizo tu bali vipando pia baadhi yake pia tunadaiwa kama nilivyosema kwenye kujibu swali lako la awali.

b) Kuhusu kushirikiana na taasisi husika kama nilivyosema katika majibu yangu ya (b) kwamba sisi tupo tayari pale ambapo hali ya nchi itakaporuhusu kifedha kushirikiana na taasisi husika katika kulijenga hilo daraja.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mohammed.

Mhe. Mohammed: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi Mohammed pia.

Wajumbe: Suleiman.

Mhe. Mjumbe Fulani: Aah! Simai Mohammed Said. Aah! huyu Suleiman.*(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Naibu Spika, leo sijui hata niseme. Sitaki niseme kitu, maana itakuja kuwa labda itakwenda kinyume na Kanuni. Mhe.Naibu Spika, mimi naitwa Suleiman Makame Ali ni Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri barabara kutoka Meli Tano kupitia njia kongwe ile; Ziwani mpaka Mzambarauni ina mashimo kama bao la soo.

Je, wizara yako ina mpango gani kuitengeneza barabara ile ili kuondosha usumbufu kwa wananchi wanaopita barabara ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake kama ifuatavyo.

Tunajua kwamba barabara ile kweli ina baadhi ya sehemu zimeharika lakini kama nilivyosema mwanzo kwamba nia yetu sisi ni kuhakikisha kuwa barabara zote hizi zinakuwa nzima na nzuri na zinapitika wakati wote. Tutashirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mfuko wa Barabara kuhakikisha kwamba pale sehemu ambapo kuna maharibiko tunazitengeneza kwa haraka ili wananchi wapate kurahisishiwa usafiri wao. Na ninamwambia kwamba Serikali yetu ina nia ya dhati katika kuhakikisha kuwa kero zote za wananchi

tunazitatua ili kuhakikisha kwamba wanafaidika na matunda matukufu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi ningependa kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Kwa kuwa wakati serikali inajenga barabara ya Dunga kutoka Jendele kule kujaa juu Mgeni Haji mpaka Dunga Mitini, wananchi waliathirika kwa njia moja au nyengine kutokana ijapokuwa serikali ilikuwa na nia njema kuwafanyia wananchi. Na hadi leo kuna majina ya orodha ya watu ambao waliahidiwa watalipwa fidia zao, wao ni wakulima na maskini kutoka eneo la Dunga Kinyongo, Ugogoni hadi Dunga Bweni kutokea kwa upande wa Mgeni Haji na hadi leo fidia zao hazijalipwa.

Je, Mhe. Naibu Waziri kwa miaka imeshapita mingi sana. Ni utaratibu gani mutaupanga ili kuweza kutekeleza hili na tayari majina yao kwa Sheha mpaka kwa Mkuu wa Wilaya yapo hadi leo ili waweze kulipwa hiyo fidia yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Nitamuomba mimi aniletee hiyo orodha ya watu, kisha tuangalie kama katika madai ya wizara yetu yapo basi tutayafanyia kazi na kuhakikisha kwamba wananchi hao wanapata haki yao. Kwani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati wowote ipo tayari kuhakikisha kuwa inawapa haki wananchi wake pale inapobidi wapate haki yao.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2016/2017

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Hivi sasa nina majina 35. Naomba niwaeleze hivi. Kwa mujibu wa ratiba yetu tupo nyuma.

Kwa hivyo kwanza sitaki mtu aniombe muda wa ziada, naomba. Usiniombe muda wa ziada tumieni kama tulivyokubaliana dakika zile zile 15, naomba sana ili twende kwa mujibu wa muda.

Vile vile naomba sana Waheshimiwa zile shukurani, sijui shangazi, mjomba, bibi, mama ziachwe, kwa sababu hazina maana katika shughuli yetu tunayoifanya. Ukitaka kushukuru wananchi wote kwa ujumla, shukuru wananchi wote kwa ujumla, mengine yapeleke huko huko nyumbani Waheshimiwa. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo sasa Waheshimiwa tunaanza na mchangiaji wetu wa mwanzo ni Mhe. Simai Mohamed Said atafuata ...

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe.Naibu Spika,

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Simai sijakuruhusu kusimama, atafuata Mhe. Suleiman Sarahan Said baada ya huyo atafuata Mhe. Ali Khamis Bakar na baada ya hapo atafuata Mhe. Bahati Khamis Kombo. (*Makofi*).

Mhe. Simai sasa ninakuruhusu.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi ningependa moja kwa moja niende katika hoja zangu.

Kwa niaba ya wananchi wangu lakini ningependa nitoe mchango wangu kwenye hii wizara husika ambayo ni muhimu kwa wananchi wetu.

Kwanza niseme tu kwamba ninampongeza sana Mhe. Waziri wa wizara hii kwa Mhe. Rais kumchagua. Katika awamu ya mwaka 2010 mpaka 2015 tulikuwa na mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, na sasa tumo katika mwaka huu kipindi cha mwaka 2015 kuelekea mwaka 2020 tuna serikali mpya na sisi wengine Wajumbe ambao bado tupo wapya.

Lakini niseme kwamba tulipoingia humu ndani tunajaribu kuona kasoro ambazo zilitokezea katika serikali iliyotoka, baina ya mwaka 2010 kuja mwaka 2015 hasa katika wizara tofauti.

Na niseme Mawaziri hawa waliokuwepo wengine sijui walikuwa na nia gani. Lakini tunajikuta sasa hivi tuna Waziri ambaye yumo katika Serikali hii peke yake, ambaye yumo ndani ya serikali pamoja na wenzake na amepewa wizara nyeti, na wizara inagusa asilimia 70 ya wananchi hapa Zanzibar.

Pia ningependa kujua huyu Mhe. Waziri mwenye kuhusika katika Wizara hii atakapokuja mbele aweze kutuhakikishia kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini pia katika kutekeleza majukumu yake na imani yake kwa Rais wetu ataweza kuyafanya kwa ukamilifu na kama alivyokula kiapo chake. Tutafurahi sana zaidi na yote ninasema kwa nia njema kabisa.

Pia niende katika suala ambalo jana kule Bara wamepitisha bajeti yao na imeanza kujadiliwa. Ningependa pia kumjuulisha kwamba tayari wao wamejipanga kwa kuongeza asilimia 10 ya kulipia hii ada ya *ten percent duty* kwenye *mobile money transfer* (tuma pesa). Na hili nina wasi wasi litaathiri wananchi wetu hasa wakulima pamoja na wavuvi na wafugaji, kwa sababu ni huduma muhimu kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ningependa Mhe. Waziri sijui atajipangaje katika suala hili. Maana yake wakati mwengine wavuvi huuza bidhaa zao wakati wapo baharini, pamoja na wakulima na wafugaji.

Pia kwenye suala la utalii wameongeza asilimia 35, pia wame-*introduce VAT* katika huduma tofauti na ambazo kwa njia moja au nyengine zinatuathiri sisi kwa upande wa Zanzibar. Kwa sababu asilimia 35 ya wageni wanaotoka Tanzania Bara wanakuja Zanzibar. Na hili kwa njia moja au nyengine linawagusa pia wizara hii husika. Ningependa kumsikiliza zaidi yeye atasemaje.

Lakini niende kwenye mchango wangu kwa haraka. Jana wakati Mjumbe mmoja anazungumza alizungumzia kuhusu maziwa ya Kiwanda cha Bakhressa. Lakini niseme mara nyingi sisi ni vizuri kama Wajumbe tukawa tupo makini kuangalia hasa baina ya wawekezaji hawa wanaofanya biashara wazalendo. Mimi kwa upeo wangu hichi Kiwanda cha Maziwa kilichojengwa huko Fumba kwa kweli kilitaka kujengwa Bara Dar es Salaam, lakini mwenye kampuni hii Said Salim Bakhressa aliamua kuja kukijenga Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, na ninachokifahamu hichi kiwanda chenye kiwango cha juu Afrika Mashariki. Kimekuwa *approved* na *TBS* na *ZBS*. Na ninajua hata ile *packing* yake ya *quality* moja ni ya hali ya juu kabisa katika Bara la Afrika. Na hivi sasa pia wanajenga kilomita mbili kutoka barabara kuu hadi kuja mpaka kwenye kiwanda.

Kwa hivyo kwa kweli huyu mwekezaji Bwana Bakhressa anafaa kupongezwa na Mungu amzidishie. Na ninampongeza Rais wetu na pia Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kwamba hichi kiwanda kimejengwa Zanzibar na Mungu awalinde wote kwa pamoja. (*Makofi*)

Mhe.Naibu Spika, lakini nikienda moja kwa moja hasa kwenye suala la *Perdue chickens*. Ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja aangalie hili suala kwa makini kwa sababu wafugaji wetu wa ndani wanazidi kuathirika. Ningependa nifahamu katika kontena moja ya kuku ambao wanaoletwa kutoka nje ya nchi ni kiasi gani cha fedha wanalipa. Kwa sababu itakuwa ni vigumu kushindana mauzo ya kuku ambao wanaoletwa na hawa wafugaji wetu, ikizingatiwa kwamba kama mtu anapata huduma hii kwa bei nafuu bandarini wakati anaingiza na wafugaji wetu huku wanazidi kuangamia. Kwa hivyo ningependa kupata taarifa zaidi ambazo za kuridhisha kabisa kwenye suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, sasa ningependa nizungumze suala la uvuvi. Nilijaribu kufanya *research* yangu jana nikaangalia kwenye mtandao. Ningependa wale ambao wanapenda kusikiliza labda Mhe. Naibu Spika, labda wachukue kalamu.

Niliangalia kwa upande wa Tanzania, *Lake Victoria* wana samaki wanakaribia 101,250 na wana boti karibu 28,470. Na wanavua sana wao kwa kutumia *nail catch* pamoja na wale dagaa.

Pia kwa Tanzania uvuvi wao karibu asilimia 85 samaki tunawapata wanatoka katika *fresh water*. Na kwa mujibu wa takwimu nilizoziona kwenye mtandao wa hizi 2013, *yellowfin tuna* yaani katika uvuvi wao wanaotumia tunapata kwenye tani elfu nne, mia moja na ishirini na nne, *bigeye tuna* 2068.679.

Halafu *soft fish* nukta saba ziro tatu na wengineo 390. Karibu ya tani 13,656. Lakini katika eneo ambalo limenifurahisha ni hili eneo la *EEZ*, ambapo kwa mujibu wa takwimu za 2013, palikuwa na mameli yanayovua yanakaribia sabini na saba ambayo yameiingizia pato karibu bilioni mbili, milioni mia nane, thamanini na saba, na mia nane na thalathini na sita na laki tatu, sawa na asilimia 79 ambayo hiyo wanayovua pamoja kwa jumla. Lakini kwa upande wa Kenya wao *inland* wanatumia sana maziwa na wanavua, samaki wao asilimia 80 wanapata katika maziwa, ambayo sasa wanakaribia chote wanachokipata kama asilimia 76 na nyengine wanapata katika hiyo *marine*. Lakini kwa takwimu zao Kenya, mpaka mwaka uliopita wana *fish ponds* 46,824, hizo ni *fish ponds* Mhe. Naibu Spika, ambazo zimejengwa katika majimbo 160.

Sasa hapa ndio kilichonishangaza Kenya wanasafirisha tani 6,742 na wateja wao wakubwa sana ni Netherland asilimia 23.9, Israel asilimia 17.9, Portugal

asilimia 11.8, *France* asilimia 8.7, Germany asilimia 8.4, Spain asilimia 5, Greece na China ndio wa mwisho. Imewaingizia bilioni 25 US *dollars* kwa mwaka 2013, 25 billion *dollars* wameweza kusafirisha samaki kwenda nje na hiyo ni mwaka 2013.

Sasa Mhe. Waziri atakapokuja ningependa kufahamu kwa upande wa Zanzibar, sisi ni kitu gani kimekuwa kigezo wakati wenzetu Bara wanafaidika, wenzetu Kenya wanapata faida, hii ni changamoto na lazima tuiangalie kwa njia ambayo tutaweza sisi kuifanya ambapo wananchi wetu waweze kuondokana na umasikini, na serikali iongeze pato lake.

Pia kuna changamoto ya *dynamite fishing*, haya mabomu yanayopigwa upande wa Pemba na Kusini mwa Unguja kuanzia Kizimkazi. Kuna tatizo la wananchi wetu ndio wanaotoboa kuwajulisha wale wakati *patrol* zinafanyika, ili watu wawe wanakuja. Kwa hivyo, ni lazima elimu iongezeke na bidii ifanyike kwamba tayari wanaharibu haya matumbawe pamoja na hizi *corals* kwa ajili ya vizazi vinavyokuja kwa miaka ya mbele, ni hatari, na lazima serikali ichukue bidii, vizazi vitakapokuja mbele vitatulaumu sisi, lazima tuwe makini, tufanye kazi ya ziada Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, pia ningependa nizungumzie suala la kilimo. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri aliwahi kuzungumza suala la *quickens* na suala la kilimo ni la msingi sana. Tuna *market* ambayo iko tayari ya biashara ya utalii, lakini pamoja na sisi sasa hivi Wazanzibari kutokana na maisha yetu yamebadilika, ulaji wa mboga mboga umeongezeka na kula matunda ya aina tofauti pia umeongezeka. Sasa ni kitu gani kifanyike cha haraka ambacho tutaweza kupata *returns* kwa haraka.

Mhe. Naibu Spika, jana nilifanya hesabu yangu kuangalia, mimi nahisi Mhe. Naibu Spika, kwa wizara hii husika kama ataweza wizara hii wachukue bidii ya kuanzisha *green houses* katika *pilot projects* huwezi ukafanya katika Mikoa ya Kusini Unguja, Pemba na Kaskazini kote, wakishaanza hizi *pilot projects* za kuzalisha mboga mboga ili kuhakikisha kwamba hizi *projects* serikali isipate hasara, waende *PBZ* wapange *plan* ya kupata pesa ambapo waanzishe kama kitengo cha *agriculture bank*, mbapo hizi fedha watakopeshwa hawa wakulima wetu wadogo wadogo, halafu tutumie wakuu wa Wilaya wetu pamoja na Halmashauri, kuhakikisha kwamba hizi *nursery* zitakazotengenezwa *green houses*, na wataalamu watakaotumika kutoka Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi waweze kusaidia hichi kilimo cha kutumia hizi *green houses* kiende, na wapande mboga mboga ambazo watataweza kuuza kwa haraka wale

wenyewe waongeze ubora wa afya zao na halafu waanze kuuza kwenye soko la utalii.

Sasa hapa Mkuu wa Wilaya pamoja na Halmashauri wahakikishe yale masoko yanakuwa tayari kwa upande wa Kusini, Kaskazini na kule katika jimbo la Mhe. Makamu wa Pili kwendea Mahonda mpaka Kiwengwa kwa Mhe. Asha Abdalla Mussa, eneo lote kutoka *Venta Club, Vera Club, Blue Bay* mpaka unamalizia huku Matemwe na kwenda juu, wanatumia mboga zaidi milioni 40 au 50 kwa siku na hizi mboga zote zinatoka Bara. Tukianzisha *green houses* wenyewe tukawasaidia wananchi wetu kwa shilingi milioni 10 tukaanza na mboga tutapata *returns* za haraka, tutaweza kusafirisha sisi mboga kuendea Bara pia, na hili linawezekana, tutumie benki zetu, rasilimali zetu na akili za watu. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ina watu wamesomeshwa miaka mingi wamesoma kule Tengeru, wamesoma Sokoine wanazijua mbegu bora zote, tuwalete watufanyie kazi, wawasaidie wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nitafurahi Mhe. Waziri atakapokuja anieleze, je, katika mawazo haya anayapokea vipi na atafanya kazi kwa mpango gani ili katika mwezi wa Disemba mwaka huu *Christmas* mboga mboga asilimia 70 zitoke Zanzibar, ahsante.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la misitu. Tuna misitu mizuri na mikubwa, tuna misitu ya Jozani, Ngezi...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una dakika nne (4) za kumalizia.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Naibu Spika, saa nyengine ninakuwa kama sisikii vizuri.
Mhe. Naibu Spika, tuna misitu ile ya Jozani na Ngezi. Hii misitu ni muhimu sana, lakini misitu hii kama ilivyounganishwa na utalii, kuna utalii ambao ni *eco-tourism* na una fedha nyingi sana, unaweza ukajenga mule maeneo madogo madogo, lakini lazima yawe na *creativity*, ubunifu na wageni pia wakalala katika hii misitu. Lakini inatumiwa bila kuharibu misitu na ni fedha nyingi Mhe. Waziri utaipata.

Mhe. Naibu Spika, unaweza kuangalia mifano kama *Dominican Republic*, hivi visiwa vilivyoko katikati mwa Canardian wametumia misitu yao kwa ajili ya fedha, lakini pia katika elimu, unawapeleka wanafunzi na kujifunza. Mfano pia ni Kisiwa cha Chumbe, hili ni eneo ambalo ni *conservation*, lakini hivi sasa wana vyumba saba, ukienda kule kujisaidia unatumia *compos*, ukiangalia kule ndani wamewafundisha kuhusu wale *giant coconut crabs* wananchi na

wanafunzi wengi wamejua. Sasa kutokana na haya misitu yetu tutumie kutoa elimu lakini wananchi waende kule wakaangalie. Pia Mhe. Waziri nakuhakikishia utapata pato kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na nakushukuru sana, naomba niishie hapo. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia juu mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Simai Mohamed, mchangiaji wetu wa pili ni Mhe. Suleiman Sarahan Said, baadae atakuja Mhe. Ali Khamis Bakar, atafuata Mhe. Bahati Khamis Kombo na baada ya hapo atakuja Dk. Makame Ali Ussi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kama ulivyoanza mwanzo na mimi nawashukuru Wazanzibari wote, Mwenyezi Mungu atujaalie tufunge Ramadhani salama wa salimini.

Mhe. Naibu Spika, na mimi napenda nichangie kidogo Wizara yetu ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na hasa kwa sababu Mhe. Waziri ni mtu ambaye naelewana naye sana, kwa hivyo nitampa muhutasari tu, kwa sababu dakika zenyewe hazitoshi.

Mhe. Naibu Spika, jana nilimnukuu Mhe. Waziri alikuwa akizungumzia sana kuhusu hali ya kujenga kwenye mabonde.

Mhe. Naibu Spika, hii hali imekuwa ya kawaida, na mimi suala hili nilikuwa nimeshaliweka katika *record* yangu, lakini kwa bahati nzuri Waziri aliliona. Mhe. Naibu Spika, watu wanalipa, neno lake analokwambia hapa ni pangu, kwa hivyo ina maana haingiliwi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kumwambia Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika hoja ambazo zipo tunasema kule, anasema haki ya kila mtu kupiga kura na wakati wa kupiga kura, kura huwa ni yake, lakini ikishakuwekwa kwenye kisanduku huwa kura sio yake tena.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa mtu anafanya vitu ambavyo haviendi pamoja na utaratibu wa serikali basi lazima serikali ichukue mkondo wake. Mtu hawezi kujenga kwenye mashamba baadae akatuletea tatizo la kuzama kwenye maji wakati wa mvua na pia akatukosesha sehemu za kulima, maeneo ya kujenga bado yapo.

Mhe. Naibu Spika, nasemea kwa upande wa Zanzibar bado tuna kilimo cha mazoea; tunalima mihogo, ndizi, mpunga na kadhalika. Tuna matatizo sana, sisi ni walaji wazuri wa mbatata, lakini kama hatujapata kiazi hata kimoja hapa Zanzibar hakipo. Sijui Mhe. Waziri hiki chakula chetu baada ya wali sasa hivi ni mbatata, au nasema wali umewekwa pembeni kwa lugha ya Kiswahili mbatata, maana yake nazungumzia viazi vya *chips* vimekuwa ndio chakula chetu, sijui waziri kafanya utafiti gani kwamba hatuwezi kuanza mashamba ya mbatata ambayo ni ya muda mfupi na chakula kitakuwa kizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, nataka kumwambia Mhe. Waziri kuhusu bahari yetu. Mhe. Naibu Spika, bahari yetu ina samaki wengi sana, lakini tatizo kubwa samaki wadogo wadogo wanavuliwa ovyo ovyo, tunabakisha kusema tu angekua mzungu angemrudisha. Samaki wadogo wadogo akina changu wanavuliwa vichanga hata kumpa mtoto hawezi kukila, hebu Mhe. Waziri, kwa sababu sina muda wa kuchambua, sijui utaratibu wa watu hawa wa kuwapa elimu na vifaa vyengine kuchukua samaki wakubwa na pweza.

Mhe. Naibu Spika, pweza wadogo wadogo ndio wanaotolewa. Tukiwa kule kwetu Vitongoji kipweza kikitoka hata huu mkono wangu hapa hakiingii, kidogo kabisa. Naomba hilo ulichukue ili tuangalie hata kama ni kufungia, tunafungia kiasi cha mwezi mmoja halafu tunawaachia watu waende wakavune vizuri zaidi. Hilo lilikuwa ni jengine.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia tena suala la mifugo. Mifugo kwetu bado hatuna ardhi ya kulisha mifugo, bado ng'ombe ni wa kuchukua na kusafirisha, lakini inavyoonekana bado tatizo la ng'ombe nafikiri serikali imeweka vikwazo vya wanaoleta ng'ombe kutoka Bara. Bado ng'ombe, mbuzi ufugaji huu hatuuwezi kwa sababu hatuna maeneo, na hata kuleta tu basi imekuwa tatizo, inaonekana ng'ombe wengi wanakuja kwa njia ya magendo kuliko hata wanaoletwa kwa njia ya halali.

Kuna maeneo napitapita kama kule Nyamanzi wanavyoniambia wale jamaa kwamba Nyamanzi na Dar es Salaam unaiona pale, lakini sijui lile chinjio letu sisi tumeliweka kizungumkuti. Kwa hivyo, sijui kama kungekuwa na utaratibu ama wa kuchukua pale Nyamanzi, kwa sababu ni pafupi, na tukawapa watu vibali vya ng'ombe na mbuzi wakawa wengi wa kuleta ambao wana uhakika wa kutuletea nyama.

Mhe. Naibu Spika, skukuu keshokutwa utaikuta nyama ya ng'ombe kilo shilingi 15,000, ambapo itakuwa hali sio nzuri, kwa watu ambao tunawategemea. Nataka ujue kwamba kilimo na uvuvi kama tutakuwa tunakula

vizuri basi hospitali tutawapunguzia mzigo, wengi wanaokwenda pale ni njaa. Mtu hajala nyama wala chochote kwa bei kubwa zilizopo. Kwa hivyo, ninachokisema ni kwamba matatizo mengi pale ya Wizara ya Afya pia tunachangia sisi Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba sana ulitizame hili, ili wananchi waweze kula vizuri na waweze kukaa katika hali nzuri na chakula kipatikane kwa bei rahisi.

Nakumbuka katika hotuba yako hivi karibuni uliwahi kusema kwamba *Insha Allah* baada ya miaka miwili pengine itakuwa chakula hatuagizi tena nje, nafikiri sana ni mchele labda tunaweza kufanya jitihada kubwa za kupata. Pia na mimi niseme kwamba tunapiga kelele, kwamba naangalia huko watu wa nje wanasema mashelisheli na muhogo bei ghali. Sijui tuna utaratibu gani hata kama sio serikali, tumewatengeneza watu wa aina gani wa kutupelekea hizi bidhaa na kuwatafuta ma-*agents* kule, tunatafuta ma-*agents* wa karafuu hapa, kwa nini tusiwatafute ma-*agents* wa mashelisheli, mihogo, ndizi tumesema vyakula vyetu vizuri hebu tufanye utafiti viangaliwe vitu hivyo.

Mhe. Naibu Spika, pia nilikuwa naangalia hapa Zanzibar tuna bahari kubwa sana ya kutisha, lakini wizara yako haijanunua maboti ya nguvu ya kuvulia, wala wewe hujajitayarisha na *cold room* ambayo ina uwezo wa ku- *store* samaki, hatuna ulazima wa kuuza ndani, lakini una uhakika umepanga samaki wa aina zote unazowajua katika wizara yako, tusitegemee tu kuwapa kila mtu hii bahari ya nje, lakini wizara kwa kuonesha muelekeo ingenunua boti za nguvu na ikawa na *cold room* yake ya kuweza kuweka samaki hata wa kuuza nje.

Mhe. Naibu Spika, samaki wa kwetu watu bado wanakuja kuwavua bure bure. Kwa hivyo, ningeshauri sana kama zamani, wizara za uvuvi zilikuwa na boti kubwa sio kubwa sana, lakini sasa hivi ziongeze viwango meli hasa ikiwezekana zitafutwe.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nasema kuhusu uingizwaji wa bidhaa ambao umekuwa na maneno mengi, ya kwamba tunakula hivi na hivi. Mhe. Naibu Spika, *cancer* imekuwa nyingi hapa kwetu, wanavyosema watabiri ni sababu ya vyakula. Sijui kwa suala hili tumejipangaje, sio kwa sababu meli inakuja kontena nimepakia, udhibiti hasa wa hivi vyakula. Maana yake tunaambiwa eti *basmati* sijui *plastic* sijui kitu gani. Kimefanyiwa utafiti wapi, kama mnatulisha *plastics* si mtwambie kwamba hii *plastic* hiki kitu gani mtu akitaka kula ale mwenyewe. Lakini mnatwambia *basmati*, sijui imenyooka, sijui nini.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hivi vyakula viangaliwe vya kutosha ili visitumalize, maana yake vitatumaliza. Kwa sababu mtu akila, hasa mjamzito anayekula na yule mtoto pia anaathirika zaidi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri mngeliangalia kwa kina sana. Kwa sababu sitaki nimkere Mhe. Spika, leo kakasirika kweli kweli kwa sababu ya muda. Mhe. Naibu Spika, ningeshauri hilo litizamwe kwa kina.

Mhe. Naibu Spika, kuna mashamba ambayo kwa hapa kwetu yameingia maji ya chumvi. Maji hayo imekua sasa ni kama kawaida ya bamvua likiwa kubwa maji ya chumvi yanaingia. Serikali kwa kupitia wizara yako sijui imejipangaje ili kuyatizama mashamba haya kama yatakuwa hayana uwezekano wa kulimwa basi kitumike kilimo cha chumvi au vilimo vyengine vinavyoweza kutumia chumvi. Kama uwezekano wa kuyazuia maji haya upo basi utafutwe utafiti wa kina ili maji haya yasiingie, kwa sababu yanaingia kwa mazowea tu. Kwa hivyo, kama ingekuwa tunaweza kuyamiliki kama pale Chake Chake, kwangu, kuna mashamba mengi kweli kweli yameingia maji, watu wanasikitika na nilikuomba wewe, kwamba nataka tukijaaliwa, nakuomba hasa suala hili.

Mhe. Raza nilizungumza naye na Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji nilizungumza naye, na wewe nakwambia na wewe ndiye utakuwa mtu mkubwa twende tukayaangalie yale mashamba na ikiwezekana Mhe. Naibu Spika, tuwape ahsante tu, kila wakati wa mchele unapolimwa tuwape hata vipolo viwili viwili kwa ule msimu angalau na wao waambiwe kama wanakula wali hata kama ni mapembe, lakini waambiwe hali ni hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nasema hivi tulikuwa tuna shimo letu la Mwanakwerekwe. Mhe. Naibu Spika, sijalifikiria sana hili shimo kwamba bado ni adui yetu. Mimi naweza kusema shimo hili linaweza kuingia kwenye maliasili pengine kutokana na hali iliyokwishajiweka. Shimo hili mimi naweza kusema ni hazina yetu, kwa sababu limeachwa kama lilivyo, lakini sijui kama serikali imefanya utafiti wa kina wa kulipeleka chini na kuangalia kima chake cha chini ambapo ukitoa udongo linaweza kuwa na kina gani, ikiwezekana kwa nini lisitanuliwe likaweza ku-*store* maji yale ya mvua yasiende kwenye majumba likaweza kujaa kwa kina, na tukalipima mvua gani ambazo zinaweza zikatuathiri, halafu baadae tukaweza kulijengea mabomba na tukaweka ma-*reserve tanks*, hata pale Mwanakwerekwe juu ma-*reserve tanks* makubwa kuanzia chini mpaka juu, na *pumps* zake, ili tukaweza kuyatizama kwamba kama yatakuwa yamejaa kwa nini tusiyapandishe kule.

Sisi tunataka *irrigation*, tunataka mambo mengi. Zanzibar ikikosa maji miezi mitatu huwa inanuka vumbi mpaka inakuwa kiama, wala maji pa kutoa hatuna, kwa sababu maji ya bahari ni adui, yanaua, maji hatuna wala mito hatuna tena.

Mhe. Naibu Spika, ile barabara ya pale haijawa sababu, hata barabara ng'oa ikiwezekana itazungushwa pahala pengine, liwekwe shimo ambalo litakuwa na uwezo wa kubeba maji. Tatizo kubwa pale ni kuingia kwa maji katika majumba, kama litaweza kufanyiwa ukarabati wa kutosha, na sijui limefanyiwa utafiti na nchi ngapi wakatusaidia maarifa lile shimo likatumika kwa wizara ya kilimo kama itakuwa kwa maji ya kunywa halifai, lakini likafanyiwa vitu ambavyo vitatusaidia sana katika maisha yetu.

Mhe. Naibu Spika, lile sio jambo la kudharau, lile tukiliharibu tukilifukia na linafukilika, nina wasi wasi ni robo tatu sasa hivi ndio limekwenda chini, ningekutaka ulitizame kwa kina lisiwe adui lile shimo. Inawezekana kama ni Mwenyezi Mungu katugaia lile shimo kwamba liwe riziki yetu, kwa sababu halitoi maji chini, ni maji ya ku-*store*. Kwa hivyo, tungelitafuta tukalitizama kwa ukweli litatusaidia namna gani.

Mhe. Naibu Spika, kwenye hii Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi hatuna viwanda. Mheshimiwa maembe Pemba yanapukutika, yanapangwa kwa mafungu, watoto wanacheza mpira. Tunaambiwa tu leo sijui atakuja kununua nani na nani, *juice* hizi tunazokunywa tunaambiwa kila siku zina mashaka, maembe mazuri yako pale. Kwa sababu ni kama zile karafuu, karafuu zilivyokuwa hazina bei watu walikuwa wakizikata wakifanya kuni, na sasa hivi miembe mtu anauza kwa ajili ya milango, lakini embe itakapokuwa na thamani basi hawezi kuukata tena muembe. Kwa hivyo, ningeshauri sana viwanda vya *juice* vitatusaidia kututuliza roho, kwa sababu hatuna viwanda hata vidogo vidogo.

Mhe. Naibu Spika, lakini nakwambia tatizo kubwa ni kwamba tusiwaachie wananchi au hawa wafanyabiashara kila jambo wafanye wao. Serikali ingekaa na udhibiti wake, na baadae ikaachia huru, akiona unakwenda upande unarudi.

Mhe. Waziri ulishazungumza masuala ya maghala, lakini bado unalizungumzia tena, chakula cha serikali bado kinahitajika, ni lazima serikali ijipange, tunaangalia hali halisi ilivyo. Kwa kweli vyakula vinavyotoka nje ya nchi bado ni biashara, haviji kwa upeo na wala haviji kwa sababu ya bei.

Mhe. Naibu Spika, leo nilikwambia habari ya mbatata, mbatata inafika kilo shilingi 3,000 wakati mbatata inafika kilo shingi 500, yote ni sababu ya tatizo

la ulimaji wetu ni mdogo. Sisi tunategemea Dar es Salaam, upepo mdogo tu wa siku tatu tu basi nyama kilo shilingi 20,000, mbatata kilo shilingi 10,000 na kila kitu. Kwa hivyo, ningekushauri sana ungeweka zizi kubwa la ng'ombe lisilopungua ng'ombe 1,000 kwenda mbele kwa kila mwezi, wengine wakaleta lakini na wewe *store* yako unayo. Ungetafuta pesa Mhe. Waziri hata za kukopa benki ukaweka wale ng'ombe, tukahakikisha kwa sababu ni mradi wa serikali na mradi mdogo basi pesa utapunguziwa hata asilimia moja, lakini ukawa na zizi la ng'ombe ambalo lina uwezo mkubwa wa kuhimili mwezi mzima tukatafuta maisha mengine.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu walimaji wa mbatata ningeshauri sasa hivi mbatata hazipo kwa sababu *chips* hakuna. Kwa hivyo, ningeshauri sana kwamba tutafute vitu ambavyo vina uwezo wa *speed* katika hali halisi Mheshimiwa siku moja tu mtu mmoja tu kama hajaleta kitu kidogo tu basi Zanzibar inahaha, inakuwa ni nyepesi ya kuhaha Ramadhani watu wanakuwa na hofu, ikimaliza Ramadhani sikukuu wanakuwa na hofu tatizo hatuna stoo ya kutosha ya Serikali tukaamua kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu wanapiga kelele sana kuhusu habari ya Sukari, viwanda vya sukari tulikuwa navyo lakini sasa viwanda vyenyewe havifanyi kazi sehemu za miwa tunazo, mashamba mengi lakini bado tumetafsiri vyengine.

Mhe. Naibu Spika, nataka uangalie Zanzibar ya mwaka 1970 itizame ilivyokuwa na viwanda, angalia hapo Maruhubi viwanda vyote vilikuwepo na vyengine vilikuwepo sasa hivi tunashindwa nini, na sana ni Wizara ya Kilimo ndio inayokuwa na uhai wa binadamu Mheshimiwa, hii ndio Wizara mama katika mambo ya ubinadamu ukiachia Wizara ya Afya na mambo mengine lakini na hii inasaidia sana.

Kwa hivyo Mheshimiwa mimi ningeshauri sana katika hali ambayo inakuwa ya kawaida, basi tuwe na vitu vyetu hatutetereki kabisa, kama alivyosema Mheshimiwa Simai hapa, wasomi tunao sana lakini biashara zetu Mhe. Naibu Spika, bado madaktari wetu hawana usafiri, hawana pikipiki halafu sasa inachosha, kwa sababu mtu anakwenda kumtizama ng'ombe mmoja ng'ombe wenyewe laki tatu maana yake ni wale ng'ombe waliokuwa hawakui.

Mhe. Naibu Spika, kama ng'ombe wale hawatufai basi yule mwenye ng'ombe tumpe na mwengine tutizame faida yake atamwacha mwenyewe yule, si lazima ukampokonye, mwambie chukua huyu na huyu anakama lita ishirini huyu anakama lita mbili au lita moja, mwenyewe atamuacha Mheshimiwa atamuuza.

Kwa hivyo ningeshauri kama wapo watu ambao unawahisi kama hawa ni wafugaji tuwape wale ng'ombe, kwa kuwajaribu Mheshimiwa, enzi za mtakato unazikumbuka, enzi za Chamanangwe unazikumbuka, maziwa pale yalikuwa baada ya binadamu wanapewa paka, leo maziwa inakuwa tatizo hospitali hakuna maziwa, mgonjwa gani ambaye hapati maziwa akapona…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika tatu malizia.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mheshimiwa naunga mkono hoja asilimia mia, nilikuwa nakuogopa sana kwa hayo, Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kusema machache katika hotuba hii ya Waziri wa Kilimo, Uvuvi, Mifugo na Maliasili.

Kabla ya kuendelea nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha siku ya leo tukakutana hapa tukiwa wazima na *Allah* atujaalie Ramadhani zetu ziwe *maqbool*.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kumshukuru Balozi Seif Ali Iddi kwa kutenga muda ambao alikwenda kisiwani Pemba kuwafariji wale wote ambao walifikwa na maafa, na yeye pia akanipatia na mimi nafasi ile kuweza kuungana naye.
Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kama ilivyo desturi nije kwenye suala la kilimo. Tunajua kama suala la kilimo ni uti wa mgongo wa taifa, ambao unatupelekea wananchi kupata huduma hii kwa kujikwamua na matatizo madogo madogo.Vile vile na kuifanyia Serikali kupata mapato yake kwa kupitia Wizara hii.

Kule kisiwani Pemba wakulima wanajitolea kwa ajili ya kupambana na suala hili, jambo ambalo linawasaidia katika kukwamua hali zao za umasikini na kujipatia kipato. La kusikitisha Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya wananchi ambao wanawarudisha nyuma wenziwao katika hali ya kuwaharibia vipando vyao kama kuwang'olea mihogo, kuwakatia miti yao na baadhi ya vitu vingine.
Nimuombe Mhe. Waziri kwamba, je, suala hili kupitia Wizara yake na kushirikiana na Serikali analiangaliaje kwa wale ambao wanawaathiri wenziwao kwa hali moja au nyengine kuwarudisha nyuma kwa kuwaharibia vipando vyao pamoja na maliasili ambazo zimeshakuwepo, kwa mfano kama mikarafuu na mambo mengine. Vile vile anawaangaliaje watu hawa ambao walishapata haya maafa watawafariji vipi.

Mhe. Naibu Spika, jana la kusikitisha ndani ya jimbo langu nilipata taarifa kwamba kuna wapiga kura kule wananchi wangu watano wameng'olewa mihogo, wameng'olewa viazi vyao licha ya kwamba huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwa kweli mimi nalaani sana vitendo vile. Naiomba Serikali ikishirikiana na Wizara hii iwasake wale wahalifu wote popote walipo, na hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Mhe. Naibu Spika, nikija kwenye maliasili. Sote ni mashahidi kule Kisiwani Pemba kuna msitu wa Ngezi ambao ni mkubwa na wa aina yake; una vivutio vingi vya utalii, lakini msitu ule mara kwa mara tunasikia kunatokezea hali ambayo wananchi waliokuwa hawaipendelei kheri Wizara hii na Serikali wanauchoma moto mara kwa mara kuiathiri rasilimali hii tuliyokuwa nayo.

Nimuombe Mhe. Waziri aliangalie hili tatizo, ni watu gani hawa wanaojitokeza na baada ya kwishapatikana vile vile wachukuliwe hatua dhidi yao, kwa sababu hawaipendelei kheri nchi hii na vile vitu vyetu ambavyo vinatupelekea kupata maendeleo kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, nikija kwenye suala la uvuvi sote ni mashahidi juzi nililigusia na hapa ndio pahali pake. Kule Tumbe ndani ya Jimbo langu kuna soko kubwa ambalo liligharimu mamilioni ya pesa za Serikali kwa ajili ya kujengwa soko lile, sasa hivi limekaa tu kama gofu. Nimuombe Mhe. Waziri akumbuke kwamba hii Wizara nani alikuwa nayo, inawezekana ikawa ni hujuma ambazo zilishafanikishwa huko nyuma kwa kupitia huyu Waziri aliyekuwepo, pengine hili soko aone kwamba halifanyi kazi zake na kuifanyia Serikali kupata mahitaji yake.

Nimuombe aliangalie, Wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Masoko ili hili soko lifanye kazi, na kama imeshindikana basi wampe Mhe. Haji Omar Kheri tuweke wana vikosi vyetu pale vya KMKM kama itakuwa hili soko la samaki limeharibika, basi tuweke pale vijana wetu waweze kutulinda sisi na mali zetu *inshaallah*.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kwenye Wizara hii ya Uvuvi tuangalie kwamba kuna wavuvi wadogo wadogo ambao wanatumia rasilimali za kuziharibu ndani ya bahari, kwa mfano kuna uharibifu wa matumbawe, kuna uharibifu wa samaki wanavua kwa kutumia nyavu au bunduki ambazo hazistahiki, wanaharibu samaki na matumbawe. Sijui suala hili analiangaliaje Mhe. Waziri katika wale watu ambao wanaharibu hizi rasilimali zilizopo.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo sina mengi nilitaka zaidi nizungumzie haya mambo mawili matatu hususan hili ambalo limenikwaza kutokana na hizi hujuma ambazo zinafanyika kule Kisiwani Pemba, kwa kweli hali ni nzito, na si kwenye jimbo langu tu hata jana nimekaa kwenye saa nne nimeangalia *ZBC* nimewaona Kamanda wa Polisi kule Kusini wanakwenda kukagua shamba la mikarafuu la mpiga kura mmoja pamoja na ndizi nyingi sana zimekatwa.

Kwa hivyo niwaombe Serikali, kwa kushirikiana na hii Wizara hebu jamani tuone kwamba hali halisi sasa hivi ya kule kisiwani Pemba imekuwa nzito, Serikali ijipange kuwachukulia hatua hawa ambao wote wanaathiri kwa njia moja au nyengine.

Baada ya kusema hayo mimi naiunga mkono hii hotuba kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi asubuhi hii nikaweza kuchangia, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutufikisha hapa tukiwa wazima wa afya.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Kilimo pamoja na timu yake yote walioweza kukaa pamoja na kuitunga hotuba yake iliyo nzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja katika suala la kilimo kwa kweli kilimo cha mpunga kwa mwaka huu 2016 wananchi wengi wameathirika katika sehemu mbali mbali, lakini tukiangalia hasa wananchi wale ambao wanalima katika sehemu za juu, ambazo haziingii maji zile sehemu wale wananchi wanahitaji kwenda kuangaliwa na kufikiriwa jinsi gani ya kusaidiwa. Kwa sababu wananchi kile kilimo chao cha mpunga wengi ndio wanachokitegemea, na baadhi ya miaka ya nyuma wananchi walikuwa wakiharibikiwa kama hivi basi Serikali ilikuwa inawatengea kiasi fulani angalau cha mchele kuweza kusaidiwa. Kwa hivyo na mimi nimuombe Mhe. Waziri kwamba hawa wananchi ambao wameharibikiwa na vipando vyao, basi awaonee huruma na aweze kuwatengea kiasi chochote kile cha kuweza kuwasaidia.

Mhe. Spika, vile vile twende katika suala la kilimo cha muhogo. Muhogo wananchi hususan katika Shehia zetu za Pemba wanalima sana kibiashara, sasa biashara zile wao wakilima wanazileta hapa Unguja, wakati mwengine biashara ya muhogo na ndizi inakutana sokoni baina ya wao wananchi kutoka kisiwa cha Pemba na wananchi kutoka sehemu nyengine. Sasa Mhe. Waziri ni vyema

wakatafutiwa soko maalum, la kupeleka hizi bidhaa zao ili hizi bidhaa zikiletwa hapa zisikutane wale wananchi waweze kupata tija zaidi ya zile biashara zao.
Mhe. Waziri, vile vile kilimo cha muhogo tunaweza kukisarifu kwa aina tofauti, tunapiga ukali, tunapika biashara za chipsi yaani unapikika kama vile maandazi, keki lakini wananchi kwa kukosa taaluma basi wanashindwa kufanya hivyo, inabidi wauze muhogo tu, sasa kwa kuuza vile vile tu ni tatizo kwa wananchi, wanahitaji hawa wakulima wapewe taaluma na pia wasaidiwe zile mashine za kusagishia nafaka, ili waweze kusagisha unga wao na badala ya kuuza muhogo waweze kuuza unga, au vile vile waweze kufanya biashara yoyote ambayo itabadilisha, ili waweze kunufaika wenyewe kwa mahitaji yao.

Mhe. Waziri na ndizi vile vile, embe halikadhalika, embe tunaweza kuipika kama fani ya ubuyu kwa kutumia taaluma zetu wanawake tunazozijua, kwa hivyo ni vyema hizi embe tukatafuta wataalamu na wao wakaweza kusaidiwa ili kufanyiwa angalau ile fani ya ubuyu, wakauziwa wananchi wakaangalia hapa Zanzibar, hii embe kupikwa kama aina ya ubuyu likoje.

Kwa kweli ni chakula kizuri sana na wananchi wao wenyewe Mhe. Waziri basi watakipenda na tutaweza kuuza katika masoko ya dunia yaliyoko ulimwenguni, tusiache embe zikaharibika, embe zina thamani, embe ina tija sana sana lakini wananchi wanakosa taaluma.Mhe. Waziri nakuomba sana taaluma hizi utufanyie ili wananchi waweze kufaidika.

Mhe. Waziri, vile vile nimeona katika kitabu chako kuna baadhi ya sehemu ambazo wananchi wanalima kilimo cha mpunga wa kumwagilia maji, namimi nikuombe katika Jimbo langu eneo la Mgagadu/Kimbuni pale ni pahali pazuri sana na wanahitaji wananchi kuchimbiwa kisima ili waweze kumwagilia maji katika mashamba yao, lakini bila ya utaalamu hawatoweza kufaidika.

Kwa sababu hivi karibuni tu tumepita pale tumeona eneo dogo ambalo limefanyiwa majaribio, lakini majaribio yale hawakufanyiwa kwa wakati sasa kukosekana kwa ule wakati wenyewe vile vile inasababisha kilimo hichi kutopata tija nzuri kwa wananchi, lakini tukitaka wananchi wapate tija nzuri, kwanza tuwasimamie waweze kulimiwa kwa wakati, wapewe pembejeo kwa wakati na zile mbegu ambazo walikuwa wanalima kwa muda mrefu waweze kubadilisha, sasa tunakwenda na wakati zile mbegu za zamani hazikubali tena katika mashamba yale. Tokea enzi na enzi mashamba yale wanalima wazazi wetu, hayajapumzika hata mwaka mmoja, zikikosekana pembejeo, wakikosa kulima kwa wakati basi hawavuni kabisa, mfano ni mwaka huu wananchi hawavuni kutokana na taaluma tunazikosa.

Mhe. Waziri nikiendelea katika suala la uvuvi hapa kidogo nataka unifahamishe zaidi kuhusu ukataji wa leseni na vyombo vya kuvulia, tunajua kwamba mvuvi yeyote anatakiwa akate leseni yake yeye mwenyewe binafsi pamoja na leseni ya chombo chake, ili kile chombo chake kikipotea kitajulikana hichi chombo ni namba ngapi na kinatoka katika Shehiya gani, lakini baadhi ya wavuvi wamekuwa wabishi.

Mfano, mtu anatoka katika bandari ya Nungu anakwenda katika bandari ya Mkoani pale kuna Mkuu wa Diko akifika pale anamuuliza, je, mzee unatoka sehemu gani, natoka sehemu fulani, lete leseni zako pamoja na barua yako ya Sheha atakuwa mbishi na atakuwa yale anayoambiwa hayataki kabisa. Kupelekea Mkuu wa diko akamwambia kwamba ikiwa huna leseni na ikiwa huna hata barua ya Sheha basi hapa uondoke, sasa hili kidogo linakuwa ni tatizo.

Na vile vile mvuvi yule yule anapofika katika lile soko anatakiwa pale alipe ile asilimia iliyowekwa na soko, analeta ubishi anasema yeye leseni yake inamlinda, na popote anaweza kuuza biashara yake, tunajua kwamba popote anaweza kuuza biashara yake, lakini kutokana na ule utaratibu uliowekwa na lile soko lenyewe sio kuwa auze popote.

Kwa hivyo Mhe. Waziri naomba atakapokuja kutathmini hotuba yake utuelekeze jinsi gani ya wale wananchi wanaokwenda kuvua katika zile bandari ambazo ziko karibu nao, kwa faida yetu sisi na kwa faida yao wenyewe, ili wasiweze kuzozana na wale makarani wa soko na makarani wa Diko waliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, kwa leo mimi sitokuwa na mengi ila naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniruhusu na mimi niwe mmoja kati ya wachangiaji wa Wizara hii adhimu, Wizara muhimu sana, wizara inayotupa chakula na kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi.

Kwanza kabisa nianze kwa suala dogo, namuuliza Mhe. Waziri kulikuwa na mpango wa kuiwezesha karafuu yetu iwe na nembo maalum, yaani hati miliki maalum kama zilivyo kawaha kutoka Ethiopia na kwengineko, kwamba wanakuwa na nembo maalum ambayo ina *bar code* na kuonesha *quality* ya kitu chenyewe, sasa ningependa nijue imefikia wapi hatua ile, najua yeye ni

mpya sana, lakini hayo mambo yalianzishwa na sijui wamefikia wapi, nimeuliza nisije nikasahau.

Mhe. Naibu Spika, sasa niingie kwanza nianze na hii bajeti, kwa kweli hii bajeti nimeipitia nimeuona ni nzuri na ni *smart* kwa maana ipo *specific*, ipo *manageable*, iko *accurate*, iko *relative* na iko *time bound*, kutokana na hiyo nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa siku chache alizopewa madaraka ya kuwa Waziri ameweza kutembelea sehemu mbali mbali. Nimemuona kwenye *TV* pamoja na Naibu wake Waziri, nasema kwa utaratibu huu ambao umeuanza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Kilimo nadhani hatua ya kimaendeleo ya kilimo kama vilivyo vilimo vya wenzetu itapatikana.

Mhe. Waziri kwanza nieleze tena mengine masononeko yangu. Wakati wizara na wakulima wanafanya bidii ya kulima, wanapoteza muda wanalima, watu wanakwenda wanakata mazao bila ya kujua kwamba na wao wenyewe wanaathirika, kwa sababu wanapunguza mazao kama ndizi ilikuwa ziwe tani 10, tumeikata migomba isiyopungua tani mbili maana yake tani nane, wanaikata bila ya sababu eti kwa sababu za kisiasa. Hawa sijui tuwaite wezi, maana mwizi akikamatwa anashtakiwa au tuwaite wahalifu. Maana yake ukichuma mazao machanga unashtakiwa, ukiiba kuku utashtakiwa lakini hawa wanaokata mazao ya wakulima kila siku hawa wanaachiwa, aa, nadhani hawa hawafai hata kukaa katika dunia hii.

Nashauri Wizara ya Kilimo ikishirikiana na vyombo vya usalama vichukue hatua kali sana dhidi ya watu hawa, hawa ni wahalifu. Kama wanaweza kukata mazao kwa chuki zao mwisho wake wataua.

Sasa niende kwenye kilimo. Katika nchi yetu kama zilivyo nchi nyengine duniani kwa kweli maendeleo ya kilimo yanazoroteshwa na mawazo yetu wenyewe wanadamu, yaani ile *mindset* yetu ndio inayozorotesha kilimo. Kwa sababu *technology* zipo, kwa maana ya taaluma mbali mbali, lakini bado wakulima wengine wanakuwa hawakubali kuzifuata.

Kilimo hapa nchini kwetu kimeanza siku nyingi sana, mabwana shamba, hao wakulima wameanza siku nyingi na kimekwenda daraja kwa daraja hadi kufikia hivi sasa. Uzalishaji uliokuwa miaka ya 1960 sio uzalishaji ulioko sasa hivi, kwa vyovyote vile umeongezeka kwa mahitaji yetu ya chakula.

Kweli tunaambiwa pengine asilimia 70 ni mchele, tunaagiza lakini nasema zaidi ya asilimia 70 ya chakula chetu tunakitoa wenyewe hapa kutokana na ndizi, mihogo hiyo tunayolima na mazao mbali mbali. Kitu chengine cha

kushangaza ni kwamba pamoja na bidii zote zinazoendelea hizi, kulikuwa na miradi hapa mradi wa muhogo kule ulifanya kazi nzuri sana, walikuwa wanashirikiana na Wanigeria wanaleta mbegu. Hapa zinafanywa tafiti mbali mbali ikiwepo Kizimbani kama ni Makao Makuu. Utafiti ule nadhani umepungua kasi, kasi iliyokuwepo siku zile nadhani sio ya sasa hivi.

Kulikuwa na *fertilizer programme* Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna *fertilizer programme* ambayo ilikuwa inakwenda shambani kumfahamisha mkulima namna ya kulima kwa kutumia mbolea, usipotumia mbolea inakuwaje, ukitumia mbolea kidogo inakuwaje, ukitumia mbegu bora inakuwaje, linakuwepo shamba la mfano, matokeo yake yanaonekana, huku kutumia mbolea na madawa na kila kitu inakuwa hivi, inakuja kama *graph,* mazao yalivyokuwa yanaota. Utaratibu ule uliwavutia sana wakulima, lakini sasa sidhani kama unaendelea.

Kulikuwa na utafiti wa mpunga,kulikuwa na mwanamama fulani yeye alikuwa anafanya utafiti wa mpunga, mambegu mengi mengi kayakusanya na mbegu hizo zikaanza kutoka tukapewa wakulima, zile zilizopasi, kwa sababu huwezi kutoa tu mbegu yoyote.

Nafikiri utafiti huo umepungua, naishauri sana wizara iziendeleze hizi tafiti, isirudi nyuma kwa tafiti zilizofanyika, lakini iziendeleze tafiti hizi.

Utafiti katika kilimo ni muhimu sana, bila ya utafiti hakuna kilimo. Katika utafiti huo napendekeza sana utafiti huo uziangalie zile *factors* au viashiria vya maendeleo ya kilimo, ambao nikizitaja kwa ufupi tu hapa kuna zile *social factors,* ambazo hizi zinakufahamisha kabisa kwamba kuna wakulima aina kadhaa, kuna mkulima yule wa kwanza ambaye yeye ukimpelekea taaluma atakusikiliza na atafuata, hawa wanaitwa ni *adopters.*

Halafu kuna wakulima ambao wao hukaa kidogo wakasubiri wenzao wafanye, na wao waige hawa wanaitwa *early adopters.* Halafu kuna wakulima wengine wao kwanza wanakaa baadae watakuja wakishaona wenzao wanafaidi ndio wanaifanya hiyo kazi, na wale wanaitwa *late majority,* ambao ndio wengi, lakini kuna *laggards,* wao hata uwapelekee hawataki kusikiliza. Sasa hawa lazima unapopeleka utaalamu wako uwajue, *categories* hizi za wakulima, bila ya hivyo ukichungulia tu *blanket recommendation* wanavyoita, ukatoa taaluma yako kwa kila mtu, wengine hawafahamu, hawataki, wengine wako hivi basi utafeli. Tafiti lazima zifanyike ili ma-*groups* ya wakulima waendewe kwa mujibu wa ma-*groups* yao.

Hapa kitu chengine kilichonisononesha hapa mkulima mzuri sana Mhe. Masoud, anasema mbolea mbovu haijawahi kutokea, na huyu anajua ni mbovu kweli, na kuwapa wakulima mbolea mbovu ni kuwazorotesha, kuwapotosha. Utafiti wa kina ufanywe kama mbolea mbovu kweli basi isitumike. Nitatoa sababu ya kutumia mbolea mbovu si kutumia mbolea mbovu tu, hata ku-*overdose*, ukitumia *overdose* mbolea kwenye ardhi basi unaiua ardhi. Kuna kitu kinaitwa *redox action* Mhe. Spika, hii *redox action* maana yake ni *reduction* na *oxidation.* Maana yake *oxygen* ikipunguzwa chini ya ardhi pale kwenye mimea inatokezea tatizo la *toxicity*, yaani zile *ferous sulphates* ambazo ziko *available* kuchukuliwa na mmea zinakuwa *ferric,* zikiwa *ferric* zinakuwa *toxic* na mmea hasa mpunga unapotokezea namna hiyo kwenye *waterlogging,* utaona umetia mbolea lakini bado unakuwa wa manjano.

Sasa umanjano ule unasababishwa na sumu, kama utauong'oa mmea ule ukautizama utakuta mizizi imeoza. Basi watu wengine wanaona mmea umekuwa manjano anautia mambolea, sasa mambolea mengi kama yale yanaharibu ardhi. Mbolea ile inakwenda chini ya ardhi inakwenda kwenye *underground water pollution,* maji yale yakichimbiwa kisima kutumia. Mfano mdogo ulitokezea hapa Kinyasini pale, Kinyasini kuna sheli ya mafuta nafikiri Wizara ya Maji sijui walitizame hili jambo kuna sheli ya mafuta ile imejengwa, pale chini skuli wamechimba kisima, mafuta yaliyoko huku yamepatikana kwenye kisima kile kuonesha huko chini kuna *capillary movement*; maji kwenda chini kufika mahala ambapo yanakusanyika *water table* na kufanya *toxicity* kama hizo.

Marekani waliangalia sana matumizi ya *chemical fertilizer* miaka ya 1980/1990 huko wakataka kupiga marufuku matumizi ya mbolea za chumvi chumvi, hizi *chemical fertilizer,* wakaanzisha mradi unaitwa *LISA Low Input Sustainable Agriculture*, akachaguliwa *coordinator* mkuu wa kule Marekani afanye hivyo, na sababu zao wakasema kwamba ma-*chemical fertilizers* haya yanaweza yakasababisha *underground water pollution*. Halafu wakasema ni *uneconomic* kwa sababu ya kuwa *expensive.* Sasa wakaendesha mradi huo. Mradi ule ulikuja ukafeli, kwa sababu haiwezekani kutumia hizi mbolea za asili, hizi mbolea za takataka huwezi kuzitumia kwa sababu unatakiwa utumie nyingi sana, na hata uzalishaji wake utakuwa si mzuri.

Kwa hivyo wakagundua kwamba inawezekana wakaja wakasababisha njaa Marekani, wakarudia pale pale kwenye *fertilizer,* lakini wakasisitiza kufanya *research* ya kutosha, *soil analysis,* kuchunguza udongo kuona kama pana mahitaji gani ya mbolea hii. Hii (*NPK)* ni *Nitrogen, Phosphorus* na *Potassium* kuitia tu pahala penye tofauti ya rutba unaweza pia ukaua wazi. Lazima ufanye

soil analysis ujue *nitrogen* itatakiwa kiasi gani, *phosphorus* itatakiwa kiasi gani na *potassium* itatakiwa kiasi gani kwenye mmea ili mmea wake uje. Kwa sababu kila mmoja katika hii ina kazi yake, kuna nyengine zinapunguza mizizi tu, kuna nyengine zinakuza ule ukijani, kuna nyengine zinakuza mazao kwa wingi. Kwa hivyo ukizitumia kwa *blanket recomendation* tunavyofanya sasa hivi nadhani tutaendelea hivi hivi mazao kidogo.

Jambo jengine la kusikitisha wakulima wetu wanafanya kazi kubwa, analima eka yake moja mpunga mfano tu, lakini ana eka ya migomba, ana eka ya mihogo, anashindwa kuhudumia. Anaweza akatumia laki tatu kwenye shamba hilo lakini anachokipata hata hamsini elfu hazifiki, ni matatizo makubwa sana.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika tatu.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Sijasema hata mifugo, sijasema hata uvuvi. Lakini sasa kwa sababu muda wangu na mimi nataka kuheshimu muda Mhe. Naibu Spika, ninauheshimu sana muda, kwa hivyo mimi niseme tu kwamba napongeza sana wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo wote na nawaambia kwamba mumepata waziri safi kabisa, mwenye ujuzi sana wa siku nyingi katika mambo haya ya kilimo, kwa sababu yeye mwenyewe katoka kwenye mizizi hiyo hiyo ya kilimo.

Kwa hivyo tumshaurini sana vizuri, ili atupe ule muongozo unaotakiwa tulete mabadiliko katika kilimo. Wenzetu hapo hapo Asia hapo huu mpunga wanazalisha maziwa, wanafanya maziwa ya mpunga, na ni maziwa wanasema yana *shelf life* kubwa yanaweza yakakaa muda mrefu zaidi hayajaharibika kuliko haya maziwa yetu.

Si hivyo tu, mpunga huu kula yale makuvi ukishayapeta yale yanatumika ama kulishia wanyama au kutengeneza mafuta. Pia mpunga huo huo wenzetu Japan wanatengeneza *wine*, ni nzuri kabisa inaitwa *sake wine*. Kwa hivyo kuna mambo mengi ambayo yanaweza kupatikana kwenye zao moja, lakini hatujaweza kutumia, tutafute, ninafikiri kuna *food value chain* hiyo tuitumieni vizuri ili kuongeza mapato. Maana ukimuongezea mkulima kama kapata mpunga, akapata mafuta ya kupikia humo humo, akapata na makuvi ya kuwalishia wanyama tunaongeza tija. Kwa hivyo tuitumieni sana hii *food chain* ili tuweze kufanikisha kilimo.

Baada ya kusema hayo niseme kwamba mikarafuu imepandwa siku nyingi sana, tangu enzi ya *dieback*, kila siku inapandwa mikarafuu kwa mamilioni

lakini ingekuwa inaota basi *wallahi* ingekuwa tuna mikarafuu mingi sana. Nafikiri kuna tatizo la huduma tuliangalie.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa muda huu, wote kuzungumza. Naipongeza sana Wizara ya Kilimo kuna wataalamu wengi sana, wazuri kabisa, naomba tufanye bidii sana, tuwe na kilimo cha kisasa kama wenzetu tuzalishe mazao kama wenzetu. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Shehe Hamad Matar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii nami nikaongeza mchangio wangu.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaendelea na lolote kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu, lakini kabla sijaenda kuchangia naomba nitamke kwamba hotuba hii na bajeti naiunga mkono mia juu ya mia. Kwa sababu nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitaiunga mkono na kuipitisha bajeti hii, nikizingatia katika maisha yangu Wizara ya Kilimo ndio wizara niliyoanza nayo maisha kwa kufanya kazi kwa muda wa miaka 20, kwa hivyo nina kila sababu. Hazitatokea wizara nyengine ambayo nimeitumikia muda kama huo.

Niende moja kwa moja michangio yangu Mhe. Naibu Spika, kuanzia kilimo. Kwanza nampongeza Mhe. Rais kwa kumchagua Mhe. Waziri wa Kilimo kutoka Chama cha ADC. Ni imani yake kubwa Rais kwa Mheshimiwa huyu kwamba Wizara hii ataifanyia inavyopasa.

Pia niendelee kushukuru Mashirika ya Kimataifa na Kitaifa ambayo yanaisaidia wizara hii, wanaisaidia serikali hii katika kuwaletea maendeleo wananchi wake. Hii itavunja kile kilio cha wapinzani kusema kwamba wapinzani wameondoa misaada yao, ushahidi unaonekana humu, mashirika ambayo yanaweza na yanaendelea kusaidia Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Niende mchango wangu katika kilimo, kila mmoja anajua kwamba kilimo ndio uhai hata kwa yule mnyama mdogo tunamwita funza, lakini kilimo katika nchi yetu kinatuongezea pato la taifa kwa asilimia 31. Kwa hivyo kilimo hiki ni kweli kila mmoja lazima atakizungumzia. Kwa kuwa muda ni mdogo, mimi nitazungumzia machache tu. Kilimo tunasema kwamba tukiendeleze lakini kilimo hiki kinakabiliwa na changamoto nyingi, tukizungumza masuala ya matrekta hayo yamezungumzwa.

Kumbukumbu zangu mara nyingi sana serikali husema kwamba tutatilia mkazo katika kilimo hiki kwa kuagiza matrekta, na kweli matrekta yanaagiziwa,

matrekta yanaletwa hapa kwa ndege kutoka Libya lakini matrekta yale hata miaka 2 sikuona kufanya kazi. Matokeo yake yamelala chini ya miembe tunaendelea na tatizo lile.

Kwa hivyo na sasa tunasikia kuna kampuni hii ambayo serikali imetia mkataba nayo, nayo nina wasi wasi sana. Nina wasi wasi kwa sababu mengi yashaletwa *Ford* hayo, matrekta ambayo yalikaa nchini humo ni matrekta ya *Ford* peke yake. Lakini haya matrekta yanayokuja zama hizi kwa kweli naona ni ubabaishaji. Naiomba Wizara ya Kilimo kupitia serikali itakapowaona kampuni matrekta haya yawe na ubora, tunapiga kelele kwamba tuna matrekta lakini inakuwa ni tatizo. Trekta moja linatembea wilaya nzima, kilimo kitakwenda vipi? Trekta hilo moja leo utakwenda unaambiwa limekatika hichi, linakatika hichi kila siku, madereva wanakwenda makarakana kutengeneza trekta. Kwa kweli hapa hatutokisaidia kilimo katika kukifanikisha jambo ambalo ni muhimu sana. Kwa hivyo naishauri sana serikali kiwanda hiki tulichokubaliana mkataba huu isije ikawa tunawasaidia wenzetu kutia fedha sisi tunabakia kuwa nchi yetu ni ya kutupia mali mbovu. Kwa hivyo hilo suala nalishauri sana kwa serikali.

Lakini twende kwenye pembejeo, kama tunataka tuendeleze hicho kilimo vizuri pembejeo nazo hazitoshi. Haiwezekani kwamba jimbo zima ukapewa pakti 7 za mbolea utafanyaje na tunaambiwa tubadilike *tusilime tulivyozoea tutumie mbolea*, sasa mbolea ndio hiyo. Kwa hivyo haiwezekani jimbo zima kupewa pakti 7 za mbolea, na wakati mwengine mbegu ukienda unaambiwa hamna lazima upande kwa wakati sio apande tu. Matokeo yake tutakuwa tunachukua mpunga, tunakwenda kuweka ardhi hakuna kinachopatikana.

Pia ukiachia pembejeo hawa mabwana shamba na mabibi shamba ambao wapo vijijini hawatoshi, kweli chuo kila siku kinafundisha lakini hatimaye sijui wanakwendea wapi. Bwana shamba mmoja au bibi shamba mmoja anaweza akapangiwa sehemu zinafika 5, tena pengine mwanamke hana hata usafiri atahudumia vipi, matokeo yake atapewa jina la bwana shamba au bibi shamba lakini hakuna kinachofanyika cha maendeleo. Bibi shamba au bwana shamba ninavyojua anatakiwa awe karibu na wakulima wake aweze kutoa mifano na kuonesha ikiwezekana na yeye awe na shamba yake, na ni vizuri awe na shamba yake mule katika jimbo lake aoneshe mfano. Lakini pia kuwashauri wale wakulima ambao wamo ndani ya jimbo lake, hili ni tatizo ambalo kuwa halipatikani ipasavyo. Ninaomba sana Mhe. Waziri wasomi hawa awatumie.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo ina wataalamu wengi sana, lakini wakati mwengine nashangaa na hata kwa serikali kwa ujumla, kila mtu anayekwenda

kusoma nje kuongeza ujuzi anaporudi hapelekwi mashambani kama ni wa kilimo au kama ni wa elimu au nyengine anabaki ofisini, ile elimu inayokwenda kuchotwa kule irudishwe kwa wananchi ili iweze kuleta tija, lakini kinyume chake inapelekwa katika sehemu za maofisi anaweza kuwa bosi huyu, bosi huyu mwisho haipatikani.

Aliyeko shambani ni yule yule mwenye elimu ndogo, na elimu ni muhimu kwenye kila jambo. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika kama tunataka kupiga hatua katika kilimo twende kitaalamu, na hicho kilimo kwa sasa ninachokishauri mimi hii serikali ilivyosema kwamba kilimo cha umwagiliaji maji. Kilimo cha umwagiliaji maji ni kilimo ambacho pekee ndio mkombozi kwa kuweza kupata chakula katika nchi yetu, na kuweka akiba ya chakula, kwani hayo maghala tunayotaka kuyajenga kwa ajili ya hifadhi ya chakula cha taifa basi kitatokana kupitia kilimo cha umwagiliaji maji. Kwa kilimo cha kutegemea mvua hatutoki kabisa, kwa sababu leo tunaona sasa hivi nchi yetu hivi sasa ilikuwa ni kipindi cha mchoo, lakini mvua iko wapi, mwezi mzima hakuna mvua hapa, ni sehemu chache ambazo zinapata mvua.

Kwa hivyo, kilimo cha umwagiliaji maji kifanye kwa vitendo, kila bajeti kinazungumza kilimo cha umwagiliaji maji, lakini hakuna maendeleo makubwa yanayopatikana, hatua inaendelea lakini bado haitoshi, hatua ni ndogo, kipewe kipaumbele.

Mhe. Naibu Spika, itakapoendelea kupewa kipaumbele, na mimi nashauri kwa Mhe. Waziri kuna bonde kubwa kule Msaani katika jimbo langu kila nikipita lile bonde naliona kwamba linafaa kwa umwagiliaji maji, kama vile unavyoikuta Upenja linawezekana bonde lile kufanywa kilimo cha umwagiliaji maji tutaweza kuvuna mpunga kwa wingi pale, haya matikiti tutaweza kuvuna pale, mboga mboga tutaweza kuzalisha kupitia kilimo cha umwagiliaji maji, hata matunda mengine madogo madogo tunaweza kupata pale. Kwa hiyo, nashauri sana Mhe. Waziri huu mradi utakapokuja na bonde la Msaani katika Jimbo la Mgogoni liangaliwe sana, wakulima wangu pale watafaidika na vijana watapata ajira kwa wingi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri atakapokuja aniweke sawa, aliposema kwamba watajenga ghala la kuhifadhia chakula na kununua mchele. Mchele huu utatokea wapi, na je, atanunua kwa wakulima au tunanunua kutoka nje. Imani yangu ni kwamba wananchi watakaposikia kuna mambo kama haya ya kujengwa ghala na wataweza kuuza mipunga yao basi itatia hamasa katika uzalishaji wa mpunga huo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja nashauri sana, naomba anieleze kwamba mchele huu utatokea wapi.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ni kuhusu takwimu. Takwimu ni muhimu kwa maendeleo, na ni muhimu kwa kila jambo ambalo litaweza kutujia, kwa mfano wananchi wanapoambiwa wafanye sensa basi huwa ina maana yake utapopanga mipango ya maendeleo, lakini takwimu pia vile vile katika mambo mengine ya kitaifa. Nina wasi wasi hizi takwimu zilizomo humu za uzalishaji zinawekwa kwenye meza, nina wasi wasi Mhe. Waziri, pengine watendaji wake wamepiga mahesabu ya *percent* kwa sababu ya kusema hivyo sidhani kama kuna wakulima waliofikiwa kama wazalishaji wakaenda kuulizwa na kuchukuliwa takwimu zao wakajulikana, hawafikiwi wakulima…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika tano, malizia.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Kwa hivyo, naomba hizi takwimu ziangaliwe vyema. Mhe. Naibu Spika, niende suala la kuhifadhi mashamba ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, mashamba ya serikali tunayo lakini naona nina mashaka nayo, kama mfano, mashamba ya mipira. Mashamba ya mipira yapo hapa tokea 1977 kuanzishwa kilimo na mimi ikiwa ni mmojawapo ambaye nilikuwa nalima tokea shilingi 10. Lakini mashamba haya sasa hivi sijui mwenyewe ni nani, tunaambiwa ni serikali, hakuna mwekezaji lakini ni faida gani tunapata katika mashamba haya. Lengo la kuanzishwa kilimo hiki cha mpira ilikuwa ni kusaidia uchumi wa nchi hii na kusaidia zao la karafuu, lakini kinyume chake naona tunaitumia ardhi ile imebaki kama ni pori tu, lakini mashamba haya vile vile mimi naona sijui mwenyewe ni nani kwa sababu humo humo mna mipira, humo humo watu wanapanda mikarafuu. Je, shamba hili ni la serikali au la mtu binafsi? Kwa ushahidi kabisa yapo mashamba hayo yameanza kupandwa miche ya mikarafuu, ni watu ambao wanadai kuwa ni ya kwao. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atakapokuja aniambie mashamba haya bado ni ya wananchi au ni ya serikali, na niliwahi kuona harakati za kupimwa mashamba haya, je, yana hati?

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri atakapokuja anijibu mashamba haya yamekodishwa kwa muda gani, na mashamba haya je yana mkataba wa kukodishwa? Kama yana mkataba naomba tuone mkataba huu na ni wa muda gani, na kiasi gani serikali inapata kwa kila mwaka?

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo ni kubwa sana, na muda wetu ni mdogo, lakini hata hivyo naomba sana Wizara ya Kilimo katika masuala ya wajasiriamali. Kuhusu ufugaji wa nyuki naomba uangaliwe sana, tutaweza kupata fedha za kigeni za ndani, inakuwaje leo tuletewe asali kutoka nje, lakini asali ya Pemba na Unguja ni zao ambalo linashika nambari katika masoko ya

kimataifa. Kwa hiyo, tuitumie fursa hii kwa wazalishaji wetu ambao tunao ndani ya nchi, tusikubali kuletewa asali kutoka nje wakati yetu sisi inapata sifa inakuwaje.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna kilimo cha ufugaji wa samaki kimeanzishwa, nauliza wataalamu hawa je wapo? Pia vile vile Mhe. Naibu Spika, kuhusu wakulima wa mboga mboga hawa ni watu ambao wana umuhimu kwa nafasi yao, hivyo naomba sana waangaliwe lakini ukulima huu unafanywa kwa kubahatisha, hakuna hata uchunguzi wa udongo.

Mheshimiwa mwenzangu aliyepita hapa sasa hivi amezungumzia masuala ya udongo na mimi naunga mkono suala hilo, kwamba lazima vilimo vyetu viangaliwe udongo huu unahitaji nini na nini. Inawezekana ardhi hii iko kamili lakini tumezoea kwamba tutie mbolea, kumbe haihitajiki, matokeo yake mti ule unadumaa. Kwa hivyo, uchunguzi wa udongo uwepo.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile niende kwenye masuala ya mwani. Zao la mwani ni zao ambalo lilianzishwa katika nchi yetu hii tokea 1981, na mwaka huu na mimi nilianza kuonja chakula cha mwani na leo pia nimekula tena chakula cha mwani, jana nimepewa *parcel* ile nimekula mwani. Kwa hivyo, imani yangu kwamba na wananchi waelezwe umuhimu wa mwani maana bado wanajua kukamata fedha tu, lakini hebu waambiwe ni mambo mengi sana yametajwa katika faida zinazopatikana kwenye *parcel* niliyopewa jana kuhusu mwani. Kwa hivyo, wananchi nao waelimishwe waweze kutumia…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana naomba niunge mkono hoja hii kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Mgogoni, naunga mkono mia juu ya mia na wizara ipewe makisio yake kama ilivyopanga.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi asubuhi ya leo nikaweza kuchangia kwenye hotuba hii kwa yale ambayo na mimi nahisi yanaweza kusaidia katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, naomba moja kwa moja nisipoteze muda sana, niwashukuru tu Mhe. Waziri na Naibu Waziri pamoja na wafanyakazi wote wa wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wameanza kuifanya katika awamu hii. Ni kweli hotuba ni nzuri na inaonesha kuwa kazi imeanza.

Mhe. Naibu Spika, lakini moja kwa moja mimi nitaanza kugusia katika suala zima la kushuka kwa pato la taifa kwenye wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba Mhe. Waziri hali hii nahisi ni moja katika kipimo ambacho sasa hivi kipo mbele yake na watendaji wake kutokana na awamu zilizopita. Kwa hiyo, kushuka kwa kiwango hicho mpaka kufikia asilimia 19.2 katika kipindi cha 2015, nadhani Mhe. Waziri ana kazi sasa ya kujipima katika kutekeleza hili. Kupandisha ili kuona kwamba kilimo kinaendelea kubakia kama ni uti wa mgongo katika nchi yetu. Lakini naamini kwa waziri huyu na watendaji alionao, na wataalamu waliopo, pindipo tukiweza kwenda sambamba na bajeti ambazo tumepitisha hapa wakaweza kupewa kwa wakati, na kama itasimamiwa vyema na wataalamu ambao wamesheheni katika wizara hii, basi naamini ukweli tunaweza tukafikia kuona sasa tunaweza tukapandisha pato zaidi, ijapokuwa kuna sababu ambazo zimetajwa kuwa zimepelekea kushusha pato hili ambalo limeonekana.

Vile vile nimuombe Mhe. Waziri kwamba ukweli pamoja na hizo lakini bado tuangalie kufanya uchunguzi kuona kuna sababu nyengine zipi ambazo zinaweza zikapelekea kushusha pato kwa wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme katika kulishauri jambo hili nadhani serikali kupitia wizara husika pamoja na wananchi wa Zanzibar ambao ni wakulima, ni vyema sasa tubadilishe mitazamo yetu. Ni kweli bado hatujawa na mikazo na mikakati ambayo ina uhalisia.

Takwimu zinazotolewa nadhani ni nzuri sana, lakini baadhi ya wakati unaweza ukasema wakati mwengine tunaweza tukatayarisha takwimu ambazo zinaweza zikaonekana ni nzuri, lakini ukienda kwenye uhalisia tukapata jibu tofauti. Naomba sasa Mhe. Waziri tufanye kazi nyengine ya ziada kuona tunabadilisha mitazamo katika shughuli zetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiangalia kwa mfano tukija kwenye *level* ya wakulima, kwa sasa wakulima wanaweza wakawa na malalamiko mengi juu ya huduma wanazozipata kupitia wizara au wataalamu wake. Lakini ukweli ni kwamba unaweza ukamuwezesha mkulima na mfugaji hatimaye kile ambacho amekipata asiweze kukitumia vizuri na badala yake akafanya mambo mengine na tija isiweze kuonekana kwenye lile lengo ambalo limekusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, sitaki nitaje mifano mingi lakini hiyo ndio picha iliyopo, tukienda kwenye uhalisia utaweza kugundua vitu kama hivyo vinaweza

vikaonekana. Lakini si hilo tu kwa upande wa watendaji pia na sisi kuna matatizo yetu au kuna mapungufu yetu ambayo miongoni mwao tunayo.

Mhe. Waziri ningeomba sasa tufanye mkakati kuona na wale watendaji wetu wanakuwa na miradi, kwani miradi yetu mingi imeanzisha mashamba darasa lakini pia na wafanyakazi nao wawe mstari wa mbele katika kuunga mkono juhudi hizi, ili kuona tunapandisha pato letu katika nchi yetu. Itakuwa ni ajabu sana kwamba mfanyakazi ni mtoa huduma za mifugo, leo inafika wakati yeye hana mfugo hata mmoja. Ni jambo ambalo kwa kweli ukifuatilia tunaweza tukaligundua hili linaweza kuwepo, lakini vile vile na mkulima naye basi mtaalamu ambaye anatoa huduma za kilimo ni vyema na yeye aonekane ana *plot* ambayo itaweza kumfanya anapopeleka ile *new technology* kwa wakulima wetu basi waweze kuona huyu aliyeniambia amedhamiria au ana jambo ambalo analisema la ukweli. Nadhani hili linaweza likatusaidia sana.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka Afisa Mdhamini mmoja Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi ameshatangulia alikuwa na mkakati sana katika kulisimamia jambo hili, alikuwa analaani sana kuona mtumishi wa serikali yuko ndani ya Wizara ya Kilimo lakini hana hata *plot* au hana hata kuku wa kuweza kufuga, mkulima yeye ndio anaendeleza shughuli hizo kwa kiwango kikubwa zaidi. Lakini vile vile sambamba na hilo naomba kwa upande wa sekta ya mifugo pia nadhani mifano kama hiyo ipo.

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja niruke hapo niende katika kilimo cha mwani. Katika nchi yetu sasa hivi tumeona wananchi wengi hasa walioko pembezoni mwa bahari wamekuwa wamejiwekeza sana katika shughuli za kilimo cha mwani, ambapo kwa miaka mingi imeonekana kimeweza kuleta tija sana katika nchi yetu, na kupunguza umasikini kwa kiwango kikubwa. Lakini vile vile bei za mwani nadhani hali ya soko kwa sasa hivi si nzuri, lazima tuseme kweli na wakulima wetu wameanza kubadilisha mitazamo ya kufanya shughuli nyengine ambazo ni tofauti na kilimo hiki cha mwani. Jambo ambalo kwa kiwango kikubwa lilisaidia sana kupunguza kero za familia katika nchi yetu hususan katika Jimbo langu la Micheweni, wanawake wengi waliweza kujisaidia maisha yao kupitia kilimo hiki cha mwani. Lakini sasa hivi imeonekana hali inaanza kusimama kutokana na shughuli hizi kushuka kwa soko la bei ya mwani.

Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2010 mwani ulinunuliwa kwa shilingi 250, lakini kadri ilivyokwenda mwaka 2014 tuliona kwamba bei ya mwani ilifika mpaka shilingi 400, mwaka 2014 hiyo hiyo bei ya mwani ilifika mpaka shilingi 500 lakini mwaka 2015 faraja zaidi kwa wakulima wa mwani iliweze

kuongezeka kufikia bei ya shilingi 700. Kwa kweli hali hii iliweza kuwatia hamasa zaidi wakulima wetu hasa wengine wanaolima matikiti na mboga mboga basi waliweza kuachia wakaelekeza nguvu zao katika kilimo cha mwani.

Mhe. Naibu Spika, kule kwetu katika Jimbo la Micheweni hata ambao walikuwa wanahusika zaidi katika kuharibu mazingira pengine ya mikoko pamoja na mawe, basi waliacha shughuli hizi na wakaelekeza nguvu zao katika kilimo cha mwani. Hali kwa sasa mpaka ninapozungumza imekuwa ni tofauti baada ya Disemba 2015 sasa bei imeshuka mpaka kufikia shilingi 300, na mwaka huu 2016 kunaonekana sasa maghala ya kuhifadhia mwani yamepungua, hamna kitu, bei imeongezeka shilingi 400 kwa baadhi ya kampuni na baadhi ya kampuni nyengine zimenunua shilingi 500. Lakini vile vile ukiangalia kuna kampuni nyengine ambazo zilikuwa zikifanya ubia katika ku-*invest* shughuli hizi kwenye manunuzi ya mwani, sasa wamebadilisha mitazamo na wameacha shughuli hizo. Kwa mfano, naomba kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika nizitaje kampuni ambazo kwa sasa zinaendelea kusaidia nchi yetu katika kuwasaidia wakulima wetu angalau kwa bei hiyo ndogo ni Kampuni ya *Seaweed Corporation*, *Zan Tour* na *Zan Air*. Lakini vile vile katika kampuni nyengine ambazo tulikuwa nazo ni maarufu na zilifanya kazi nzuri, kwa mfano kulikuwa na kampuni ambayo tunaita *Diri, Tawakal SM. Rashid* wote hawa wameshaacha shughuli hizi hawanunui tena mwani.

Kwa hiyo, sasa wananchi wetu wanaendelea kurudi tena katika umasikini ambao unashamiri kwa kiwango kikubwa zaidi. Naomba Mhe. Waziri kwa juhudi yako na maarifa yako, naamini unaweza ukatafuta mbadala wake tuweze kuona tunaokoa maisha ya wananchi wetu ili waweze kupiga hatua katika kupambana na janga zima la umasikini.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hilo naomba niingie katika tafiti pamoja na sera za kilimo.

Mhe. Naibu Spika, ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waweze kupitisha kwa kauli moja katika shughuli hii au katika bajeti ya tafiti pamoja na sera za kilimo, ili kuona waweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Lakini vile vile naomba kwa upande mmoja wa watendaji, basi na wao waweze kutuonesha kwamba hizi fedha ambazo zitatoka waweze kuzitumia kwa vile ambavyo imekusudiwa, na hizo tafiti ambazo zitafanyika tumekuwa tuna mazoea baadhi ya tafiti zinafanywa, lakini mwisho zinamaliza kwenye madroo na haziendi kule ambako kunakusudiwa zikaweza kuleta matokeo, na hatimaye hatua zikaweza kuchukuliwa.

Tumegundua kwa mfano katika kipindi kilichopita mwaka 2015, katika Wilaya ya Micheweni ambayo nilikuwa kipindi hicho niko mimi mwenyewe naongoza, kulifanyika tafiti ya kuangalia uwezekano wa kuweza kumuhuisha mbuzi zaidi katika maeneo ya maweni kwenye jimbo langu la Micheweni, kuonekana kwamba tunaweza kumuimarisha zaidi mbuzi, lakini na kuangalia pia kuongeza mfugaji katika shughuli hizi ambazo anazifanya. Lakini utafiti huo ulisimamiwa na Chuo cha Kilimo Kizimbani, na hadi leo hatuna majibu ambayo ya tafiti hizi ambazo zimefanywa, na wananchi wameweza kuuliza tumefikia wapi, mambo kama haya nadhani kwa kiasi fulani yanaweza yakawavunja moyo, na kuona kwamba ule muda ambao wananchi walioupoteza katika kuuliza maswali mengi pasi na kuwa na malipo yoyote haikuleta tija. Na vile vile kuna utafiti mdogo wa Mradi wa Mbuzi wa vijana katika Wilaya ya Micheweni, katika shehia chache lakini hadi sasa hivi hatuna majibu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa zimebakia dakika nne.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Naibu Spika, kwa haraka haraka katika programu ya miundombinu na masoko, fedha nyingi tumeziona IFAD wametoa, SMZ wametoa fedha nyingi lakini mkakati unaonekana kwamba sasa hivi hata hapa Zanzibar mambo mengi tunategemea wenzetu kutoka Tanzania Bara. Kwa mfano mboga mboga tunaagizia Bara, maziwa, Bakhressa anahitaji maziwa hamna, ng'ombe tunaagiza Tanzania Bara na vile vile tukija moja kwa moja katika upandishaji wa ng'ombe kwa shindano yaani kuna matatizo makubwa ambayo tumeweza kuyaona.

Mhe. Naibu Spika, naomba niishauri Wizara, basi kwa vile muda wangu utakuwa ni mdogo lakini baadae nitachangia japo kwa maandishi kuona kwamba naweza kukabiliana na hilo. Vile vile napenda kutoa ushauri suala zima la mradi wa MIVARF. Huu mradi ni mzuri ni miradi mingi ya Serikali na inawekeza fedha nyingi katika nchi yetu lakini bado hatujawatendea haki baadhi ya wananchi. Kwa mfano mradi huu katika Wilaya ya Micheweni umeweza kutengeneza barabara za ndani katika maeneo mbali mbali ya vijijini lakini la kushangaza na la kusikitisha maeneo ambayo wanaharibu mazingira kwa kiwango kikubwa ni maeneo Jimbo langu la Micheweni, barabara mbovu na wanaendelea kuchukua rasimali hiyo katika kuimarisha katika maeneo mengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa hili mimi niseme kwamba naiomba Wizara ya Mhe. Waziri, iniahidi kwamba sasa na Jimbo la Micheweni kwa kupigia mradi huu itaweza kusaidia katika kuona kwamba barabara za kule zinafanyiwa

marakebisho, nazo ziweze kupitisha hususan katika kipindi hiki cha mvua. Na pindipo Mhe. Waziri, mimi nadhani ni kufanikiwa inaweza ikaja ikaleta wananchi wakaweza kutekeleza sera ambazo zile sizo za Chama cha Mapinduzi. Naomba sana Mhe. Naibu Waziri, kwa umahiri wako na usikivu wako unisaidie ndani ya Jimbo langu la Micheweni. Hali ni aibu, rasilimali za Micheweni zinatoweka, za misitu, mawe mengi, fedha nyingi unazipata kupitia Wizara hii kutoka Jimbo langu la Micheweni, lakini hadi sasa mashimo mengi, barabara ni mbovu hazipitiki na ni aibu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwa muda huo mchache niombe tu kwamba na mimi niseme naiunga mkono hoja hii au hotuba hii kwa asilimia mia moja ili waweze kuleta tija katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru Mheshimiwa. Sasa mchangiaji anayefuata ni Mhe. Mtumwa Suleiman Makame na baada ya Mhe. Mtumwa Suleiman Makame nimesema atachangia Mhe. Mtumwa Peya Yussuf na baada ya hapo atachangia Mhe. Hassan Khamis. Mhe. Mtumwa karibu.

Mhe. Mtumwa Suleiman Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mchango huu. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa ulimwengu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima.

Mhe. Naibu Spika, na mimi naungana na wenzangu kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kilimo. Mhe. Naibu Spika, mimi nachangia sekta ya kilimo cha mpunga. Mhe. Waziri, kama unavyojua kuna aina mbili ya kilimo, aina moja kilimo cha umwagiliaji maji na kilimo cha asili.

Mhe. Naibu Spika, kilimo cha asili ni kilimo cha kutegemea mvua ya masika. Kilimo hiki Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi kirefu wakulima wengi wanakosa kupata mazao ya kutosha; kwa sababu kilimo hiki kinalimwa ambao msimu wa kupanda unakuwa umeshapiga. Aidha, mpando huu unatakiwa wananchi wapande mwezi wa Disemba na hatimae wanalimiwa mwezi wa Disemba au Januari. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, wananchi wengi wanakuwa hawapati mavuno mazuri. Cha kusikitisha zaidi kwa kule Mkoa wangu wa Kaskazini Unguja kuna maeneo mabonde kama haya ni Mto wa Pwani, Mbuzini, Kijambani, Kilombero na Kichanga, wakulima hawa wanalima ukulima wa kutegemea mvua ya masika.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya, kama nilivyoeleza kwamba ukulima huu unachelewa kulimiwa na hata hivyo ukeshalimiwa kile kipando chako pia

kinakuwa hakileti rutba nzuri, kwa sababu baada ya kwisha kulimiwa unahitaji upate dawa ya gugu na badala ya kupata dawa ya gugu unahitaji mbolea. Aidha, dawa zile za gugu zinakuwa kidogo na bahati mbaya ile kidogo yenyewe inayoletwa pia inakuwa ni mbaya kabisa. Mwananchi anapotumia dawa hii kwa kutegemea kupata mazuri bahati mbaya mazao yale yanakuwa yanaharibika kabisa, kwa sababu ule mpunga badala ya kutia dawa mpunga ule unakufa kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nina masikitiko makubwa sana kwa wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini hasa kutokana na Mkoa ule wanawake ndio wanaolima kilimo hiki cha mpunga asilimia 100 juu ya mia. Wanaume wengi wanakaa mabarazani au kwenye vimaskani wanasafiri, wapo pale pale kwenye maskani zao, lakini wanawake ukifika wakati wa kulima Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, nakuomba utembelee eneo la Mkwajuni njia ya Nungwi, utawakuta wanawake wanavyohangaika wanaparamia magari makubwa kwenda kufanya kilimo cha mpunga.

Bahati mbaya wananchi hawa nauli wanakopa kwa kutegemea baada ya kwisha kuvuna auze mpunga apate pesa ya kulipa nauli. Bahati mbaya Mhe. Naibu Spika, mwananchi yule mpunga havuni na huku anakuwa ana deni, maskini ya mungu dhalili, watoto wanamhitaji mama yule yule, baba anamhitaji mama yule yule, lakini matokeo yake hali halisi kilimo hicho kwa kweli kinatufanyia matatizo.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri, kwa vile alivyopania na hotuba yake nzuri ya kusema kwamba atakiendeleza kilimo hiki, namuomba Mhe. Waziri kwamba kilimo hiki akipe kipaumbele tuwalimie wananchi kwa wakati utakapofika mwezi wa Disemba kwa mbegu zile zilizokuwa zina ladha nzuri za bashasha kwa sababu tawi la mpunga wa ringa, supa, mpunga wa kibawa cha kia la ngawa na kuna mpunga wa wamba. Mpunga huo utaula Mhe. Naibu Spika, bila ya samaki, kwa sababu ni mpunga wenye ladha na laini, kuliko hizi mbegu zetu tunazoletewa za *super* India, *super* bikemi, kama sehemu iliyokuwa haina maji mpunga ule huwezi kuuvuna.

Mhe. Waziri, nakuomba tena ukipe kipaumbele kilimo hiki cha asili, kilicho cha asili hatuwezi tukakiacha kwa sababu tunaambiwa kwamba mambo mengi tuyarejeshe mambo ya asili; kwa hivyo Mhe. Waziri, baba angu unayajua mambo ya kizamani nakuomba suala hili usiliache. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo naingia kwenye sekta ya misitu. Kule Chaani Masingini kuna eneo lililokuwa linapandwa miti, miti ile sisi wanawake

wa eneo lile la Chaani, Pale, Donge, kipindi kile cha nyuma tulifaidika sana kwa kupata kuni na pia tulipata hata kununuwa herini za dhahabu. Kwa sababu tulikuwa tunaenda kule kutafuta kuni na tunanunuwa magogo yale tunafanya makaa, binafsi yangu mimi niliwahi kufanya tani za mkaa. Kwa hivyo ilikuwa tunafaidika, lakini bahati mbaya msitu ule sasa hivi hakuna limebakia jangwa tupu. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri, eneo lile la Chaani Masingini alitembelee na alikague ajue tatizo lake nini ule msitu ule auendeleze, ili wananchi wa eneo lile na wao wapate ajira.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo mfupi kwa niaba yangu mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi na wanawake wa mkoa wa Kaskazini Unguja, naiunga mkono hotuba hii mia juu ya mia.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana kwa mchango wako mzuri Mhe. Mtumwa na kuwatetea wanawake; sasa ninampa nafasi Mhe. Mtumwa Peya Yussuf na baada ya Mhe. Mtumwa Peya Yussuf na baada ya Mhe. Mtumwa Peya Yussuf atakuja Mhe. Hassan Khamis na baada ya hapo tutampa nafasi Mhe. Abdalla Ali Kombo,

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi kuichangia hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima na kuweza kusimama kuichangia hotuba hii ya Wizara ya Kilimo.

Mhe. Naibu Spika, pia nampongeza Mhe. Waziri, pamoja na wasaidizi wake kwa kuiandaa vizuri hotuba hii iliyobeba masuala mengi. Mimi naanza na suala la ufugaji.

Mhe: Naibu Spika, wananchi wengi wanajishughulisha na suala hili la ufugaji; kuna wananchi wanafuga kuku, kunafugwa ng'ombe, na kunafugwa na mbuzi. Lakini ukiangalia Mhe. Naibu Spika, katika maeneo yetu wafugaji hawa kwa kweli wanafuga lakini kipato chao ni kidogo sana. Kwa sababu ukiangalia katika maeneo mengi hawa wataalamu wa mifugo hasa hakuna. Aidha, unaweza ukaona eneo refu sana ndipo ukampata huyu mtaalamu wa mifugo.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo unawakuta wafugaji hawa wanafuga lakini hatma wake wanakula hasara. Kwa sababu hata ile mifugo imepata maradhi wanahangaika sana kutafuta wataalamu hawa na inashindikana unawakuta wananchi wetu wanakata tamaa wanaacha kufanya shughuli za ufugaji wakati ambao ndizo zinazowapatia kipato. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri, kwa

makusudi mazima waandae hawa madaktari ambao wana shughuli hizi za mifugo waweze kuwa karibu na wananchi ili wanapopata matatizo ya mifugo yao, basi waweze kusaidiwa.

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba ya Mhe. Waziri, inaonesha kwamba kuna uzalishaji wa samaki umeongezeka kutoka tano 32,974 hadi 34,104, lakini bado Mhe. Naibu Spika, ukiangalia ongezeko hili la samaki lakini bado pia samaki imekuwa ni adimu. Kwa sababu unaweza kwenda sokoni wewe mwenyewe ukashindwa na ukarudi kitoweo usinunuwe.

Mhe: Naibu Spika, mimi natoa ushauri, katika Mkoa wa kaskazini au katika Jimbo langu la Bumbwini; kuna eneo kubwa sana liko Bumbwini Mafufuni limepakana na kambi ya Magereza. Bonde hili hapo zamani lilikuwa linalimwa chumvi na kulimwa samaki, lakini hili bonde kwa sasa hivi imekuwa halitumiki ipasavyo kwa sababu ni sehemu ndogo tu wananchi wanatumia kwa ufugaji huu wa samaki. Niiombe Serikali tuwasomeshe vijana wetu na tuweze kuliboresha bonde hili ili vijana hawa wanaweza kufanya kazi ile pale ya ufugaji wa samaki tukapata samaki wa kutosha lakini pia tunaweza kupuguza tatizo la ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, lakini ukiangalia ndani ya ukanda wa pwani vijana wetu wanaoishi maeneo yale wanajishughulisha na masuala ya uvuvi, lakini ukiangalia uvuvi wenyewe wanaoufanya Mhe. Naibu Spika, ni uvuvi mdogo, kwa sababu utawakuta vijana wanachonga kidau chao au kingarawa tunasema cha muembe, ngarawa ile wanaingia watu wawili, wanakwenda baharini kutwa na pengine wamejikaza wamepata nduaro wao mmoja au wawili wanarudi nyumbani. Kwa kweli inakuwa haikidhi haja wala haitoshelezi. Nimuombe Mhe. Waziri, achukuwe juhudi za makusudi kutafuta maboti makubwa nakuweza kuwezeshwa vijana hata kama watakaopeshwa lakini waweze kwenda kwenye bahari ya kina kirefu na waweze kwenda kuvua uvuvi ambao utaweza kuwapatia tija wao pamoja na familia zao.

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba hii ya Mhe. Waziri imezungumzia suala la ununuzi wa mbegu ya mpunga tani 228, tani 128 zimezalishwa hapa Zanzibar na tani 100 zimenunuliwa kutoka Bara. Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri, aniambie kwamba ni mbegu gani ambazo zimenunuliwa za mpunga kutoka Tanzania Bara. Na pia naomba nimuulize, kuna mbegu ya mpunga ambayo ilikuwa inatwa *NERICA*, mbegu hii iliambiwa inaweza kuota pahala popote na pia inazaa sana, kipato chake ni kikubwa ambapo mwananchi au mkulima atalima mbegu hii. Lakini Mhe. Naibu Spika, mbegu hii sijui kwa kweli imepotelea wapi, kwa sababu hatuioni wala hatujui iko wapi. Kwa hiyo

namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja kusimama aniambie mbegu hii imepotelea wapi.

Mhe. Naibu Spika, katika Mkoa wangu wa Kaskazini pia watu wengi nao wanajishughulisha na suala la kilimo. Lakini ukiangalia wanasumbuka sana kama walivyozungumza wenzangu suala la mbolea lakini pia na swali la dawa. Na katika eneo langu la Bumbwini wananchi wengi wanajishughulisha na kilimo ni watu wazima, wanapohitaji mbolea au wanapohitaji dawa inabidi waende masafa marefu. Aidha, waifuate Mahonda au waifuate Donge na hawa ni watu wazima ambao wanafanya shughuli hizi, anaweza kutoka pale mtu akenda Mahonda kwa mbolea pengine anaifuata kilo tatu au kilo nne ni masafa marefu sana. Nimuombe Mhe. Waziri, eneo la Mangapwani kuna kituo pale cha mifugo.

Niombe hizi pembejeo kwa ukanda wa Bumbwini lisogezwe pale inaweza ikawarahisishia kazi hii usumbufu ukawaondoshea wananchi wa Bumbwini, Mangapwani mpaka Mfenesini. Kwa hiyo namuomba Mhe.Waziri, suala hili aliangalie kwa kina kuweza kuwaondoshea usumbufu wakulima wetu wa ukanda wa Bumbwini.

Mhe. Naibu Spika, kuna wananchi ambao wanalima mpunga kwenye bonde la kiwanda cha sukari na bonde hili kwa kweli lina mgogoro siku nyingi sana baina ya muwekezaji na wakulima. Mimi nimuombe tu Mhe.Waziri, yale maeneo ambayo kwa sasa hivi hayakulimwa miwa basi kuna haja maeneo yale wapewe wananchi waendeleze kilimo chao cha mpunga. Hapo muwekezaji atakapokuwa tayari basi warejeshewe wenyewe kwa kuendelea kulima miwa, lakini pale inapokuwa bado yasikae wazi maeneo haya wapewe wananchi ili waweze kuendeleza kilimo chao hiki cha mpunga.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, imesomesha vijana wengi sana kwenye Chuo kila pale cha Kizimbani, lakini vijana hawa wengi wao bado wapo hawajaajiriwa mpaka hivi sasa. Namuomba Mhe. Waziri, atakaposimama aniambie tu je, vijana hawa kuna mpango gani na lini wanaweza wakaajiriwa. Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa niaba yangu na wananchi wenzangu wa Jimbo la Bumbwini naiunga mkono hotuba hii ya Wizara ya Kilimo kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mtumwa Peya Yussuf kwa kujali sana muda, sasa mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hassan na baada ya Mhe. Hassan atakuja Mhe. Abdalla Ali Kombo baada ya Mhe. Abdalla Ali Kombo atafuata Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kwanza nachukuwa fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri, kwa kutuletea hotuba ya bajeti nzuri, kitabu chake kina kurasa 125 lakini nitaanza kwa kusoma maneno katika kitabu chake ambacho kilichoandikwa maneno mazuri, sijui *implementation* ya maneno hayo.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu chake ukurasa wa 4(2) ukuaji na mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa. Mhe. Naibu Spika, sekta ya kilimo bado inaendelea kuwa ni tegemeo kwa uchumi wa Zanzibar ambapo inatoa mchango mkubwa katika kujikimu kimaisha na kupatikana kwa chakula na lishe bora. Maneno mazuri sana yamepangika lakini tuangalie haya maneno yana ukweli gani.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nitaanza kutoa lile lengo la mchango wa bajeti ya hotuba. Lengo langu ni kujenga si kubomoa, lakini pia ili... kwa sababu Waziri huyu ni mzoefu basi najuwa tutapomwambia na akitusikiliza ataweza kutoa huduma bora kwa wananchi. Tukimwambia na akitusikiliza ataweza kuwa Waziri bora atakayeweza kuwahudumia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni nchi ya mapinduzi na lengo kuu la mapinduzi ilikuwa ni kuondosha udhalilishaji na kuwainua wanyonge kimaisha. *Slogan* ya Mapinduzi inasema hii ni nchi ya wakwezi na wakulima. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ yeye juzi aliiongeza akasema na wavuvi. Kwa hivyo, *slogan* ya Mapinduzi hii ni nchi ya wakwezi, wakulima na wavuvi.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo ina jukumu la kilimo, uvuvi na ufugaji. Nitaanza bajeti yangu kwa kilimo. Sisi Zanzibar chakula kikubwa tunachokula ni mchele, lakini tunategemea kwa mwaka tani 80,000 ndio mahitaji. Sisi wenyewe tunazalisha tani 15,000 au 16,000 kwa mwaka. Hivi karibuni hapa ilikuja *project* ikaitwa kuzalisha mpunga wa *NERICA* kama sikosei, wakulima wote wa Zanzibar wakwezi na wavuvi tulifurahi tukasema *Alhamdulillah* sasa jibu la shida yetu limekuja.

Mhe. Rais anayeongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tulimuona katika majukwaa, katika matrekta akiwa anaonesha uso wa bashasha kwamba sasa jibu la njaa ya Zanzibar limepatikana. Lakini sijui kitu gani kilitokezea, maneno yalikuwa mazuri lakini *project* hii ilifeli mpaka hivi leo Zanzibar mpunga huu wa *NERICA* hatuuoni. *Project* hii imekufa na hatujaona *impact* ya *project* hii ambayo tunaamini wazi kwamba wataalamu wa Wizara ya Kilimo

ambao wapo wengi na inaongoza kwa kuwa na wataalamu. Kwa hivyo, anapokuja Mhe. Waziri anijibu kwa nini *project* hii walii-*launch* wakiwa bado hawajafanya utafiti uliokamilika na kuwadanganya wananchi hatimae kuwapa matumaini aliyokuwa siyo na yameleta hatari kubwa kwao. Wamefika pahali hawaiamini tena Wizara ya Kilimo na wanaona kwamba hawasaidiwi na wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, sio siri ukienda sokoni utasikitika kwamba Zanzibar tunahitaji *carrot*, pilipili boga, vitu vyote vya mboga mboga lakini vitu hivi vyote vinatoka Bara; unajiuliza ndugu zetu vijana wanahangaika na ajira nchi hii kumbe ajira zipo kwenye kilimo na Wizara ya Kilimo ipo. Hapa tunataka kuipitishia pesa chungunzima lakini hujui wizara hii inafanya nini na ina wataalamu wengi. Sasa Mhe. Waziri anambie wana mpango au mkakati gani wa kuhakikisha hizi mboga mboga tunazotumia Zanzibar angalau asilimia 50, ziwe zinazalishwa Zanzibar. Naomba anijibu.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwetu shamba ya Mchangani ni maarufu sana kwa kuzalisha embe shomari ambazo zinaongoza duniani kwa ubora na utamu. Watu wa kule Mchangani msimu wa embe tunakuwa matajiri, lakini zamani siku hizi ule utajiri wetu umepungua. Kwa sababu zamani embe hizi ilikuwa wazee wangu wanachukua wanasafirisha Oman lakini siku hizi embe hizi zina wadudu na karibu miaka 10 wadudu hawa Wizara ya Kilimo wameshindwa kuwatafutia tiba. Wazee wangu kule wamekuwa wanakula hasara kwa embe zile, hakuna kiwanda chochote kile ambacho kinaweza kufanya juisi, embe zile hazisafirishiki nje kutokana na wadudu.

Nchi za wenzetu kwa mfano Mali walikuwa na tatizo hilo tayari wameshalisahau kwa sababu wameweza kulitibu, hata Dar es Salaam hapo limeweza kutibiwa, lakini bado Zanzibar tatizo la wadudu wa embe limekuwa kubwa na linaathiri, linawa-*cost* wakulima wetu wa embe hawapati kuuza embe zao nje hatimae embe zile zinaoza. Naomba Mhe Waziri aniambie ana mpango gani wa kumaliza tatizo la wadudu wa embe Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika kuna uvuvi. Nina masikitiko makubwa sana Mhehsimiwa, maana yake ninaona tabu. Zanzibar ni nchi iliyozungukwa na bahari lakini huwezi kuamini samaki amekuwa ghali kuliko kitu chochote duniani. Cha ajabu zaidi hapo si mbali, kuna mtu ana mafriji 27 anauza samaki kutoka nje ya nchi. Mheshimiwa hii ni aibu kubwa, nchi ya kisiwa imezungukwa na bahari, wavuvi wapo wengi, wako tayari kuvua lakini zana hawana, ujuzi hawana, hatimae wanapofanya hii kazi wameshachoka lakini hawana chengine cha kufanya sasa samaki tumekuwa tunaagiza nje.

Mhe. Naibu Spika, hii ni aibu kubwa, nataka aniambie Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuhakikisha vijana wetu hii ajira ya uvuvi wanaitumia vizuri na inawaondoshea umasikini. Kwa sababu wako tayari kulima lakini hawana nyezo, hawana utaalamu na leo hii tayari matajiri wameshaichukua sekta ya uvuvi katika kuagizia samaki. Anijibu Mhe. Waziri wa Kilimo.

Mhe. Naibu Spika, kadhalika Wizara ya Kilimo inahamasisha uvuvi wa bahari kuu, lakini hata sheria ya bahari kuu Zanzibar hatuna. Sasa aniambie Mhe. Waziri lini sheria ya Bahari Kuu wakati serikali inahamasisha uvuvi wa bahari kuu ataileta Barazani tuje tuipitishe.

Nikiendelea hapo hapo kwenye uvuvi Tanzania na Zanzibar ikiwemo Japani na nchi nyengine zilizoendelea, ndipo zinapoiba samaki kwa wingi kwa sababu hatuna zana za kuwaona wale wezi wa samaki. Nakumbuka Mhe. Rais John Pombe Magufuli tangu alipokuwa waziri alikamata meli nyingi zinaiba samaki. Mhe. Waziri pia anijibu tatizo la uvuvi haramu bado lipo Zanzibar na linaendelea na linatuathiri, ana mpango gani wa kumaliza tatizo hili hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naingia katika ufugaji. Nina masikitiko makubwa sana wafugaji wapo, vijana wengi hawana ajira wako tayari kufuga lakini *outcome* yake sasa tumekuwa maziwa pia tunaagiza kutoka nje. Kuna kampuni 26 Zanzibar zote zinaingiza maziwa kutoka Dubai na kwengine wakati Zanzibar wafugaji wapo wako tayari lakini hawana utaalamu, hawana nyezo hawawezeshwi wapo wapo tu. Nyama tunaagiza kutoka nje, kuku kutoka nje, hebu anambie Mhe. Waziri wana mpango gani wa kuwezesha hii sekta ya ufugaji Zanzibar angalau kama ilivyokuwa zamani.

Mimi nakumbuka zamani kulikuwa na vibanda vya vinauzwa maziwa, kuku walikuwepo wanauzwa, kila kitu kilikuwepo lakini leo tumeshashindwa tumefikia wakati tunaagiza kutoka nje. Kuna *Perdue fish* hapa aliyefika miezi minane iliyopita analetwa Zanzibar kuja kuliwa. Mimi si mtaalamu wa afya lakini nafikiri hata kiafya si wazuri. Kwa hivyo, Mhe. Waziri anijibu.

Vile vile kuna hii Sekta ya Maliasili. Juzi Mhe. Waziri alisema *statistic* ya minazi Zanzibar imebakia 3,000 na yote kama sikosei imeshakuwa mipevu. Sasa wana *project* ya kuwazuwia wanaokata minazi lakini bado kila siku nikitupa jicho minazi Zanzibar inakatwa kuliko kitu chochote. Sasa aniambie wana mpango gani wa kuzuwia kikweli kweli sio kiuongo uongo ukataji wa minazi Zanzibar na mpaka hii leo watu wangapi wameshawafikisha

mahakamani na kuwafunga wanaokata minazi. Kadhalika wana mpango gani wa uzalishaji wa minazi mipya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar azma ya Mapinduzi ni kuokoa wakulima, wakwezi na wavuvi lakini hebu Mhe. Waziri anambie hii wizara yake ndio inayobeba kila kitu na watu hawa bado masikini. Maana yake nchi hii mkulima ndie masikini, mvuvi, mfugaji, sasa ana mpango gani wa kuwaokoa hawa watu na umasikini. Leo hii mkulima akiumwa pesa ya hospitali hana lazima achangiwe na ukoo wake. Leo hii mkulima akiumwa mtoto wake pesa ya kumpeleka hospitali hana lazima achangiwe, mkulima huyu watoto wake hawaendi skuli vizuri kwa sababu uwezo hana na *Mapinduzi Slogan* imemzungumza nambari moja ni mkulima, mkwezi na mvuvi. Lakini watu hawa ndio masikini katika nchi yao ya Mapinduzi iliyofanya Mapinduzi kwa lengo la kuwatetea wao.
Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wizara hii ndio wizara mama kwa Zanzibar, lakini mimi...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika nne.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wakwezi na wakulima wa Jimbo langu la Welezo wana Mapinduzi nitaunga mkono hoja asilimia 50, asilimia 50 namuwekea Mhe. Waziri anijibu maswali yangu kwa kina kwa vile wizara hii maneno ya kisasa ndio mpango mzima, tunaweza tukenda kwenye kura hasa kama hajatujibu sekta nzima ya mpunga wa *NERICA*, kwa sababu tulifurahia sote lakini ulikuwa hauna *outcome*.

Mhe. Naibu Spika, kwa maana hiyo, naomba majibu yasiwe ya kisiasa. Namjua ni mzoefu, anipe majibu yanayotekelezeka ili tuweze kumpitishia bajeti yake kama sio hivyo tumejipanga kwa vile tunaogopa siku moja tusije tukakosa kuletewa chakula ndani ya nchi na hapa chakula hakilimwi na wizara tumemkabidhi yeye mzoefu tukashindwa kula nchini lazima atujibu. Kama sio hivyo tunaweza tukaenda kwenye kura kwa hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache kama nilivyosema naunga mkono hoja hii asilimia 50 na 50 namuachia baada ya kujibiwa masuala yangu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwaombe sana *list* niliyonayo ni kubwa sana na ratiba inatwambia leo tumalize kwa sababu leo tunatakiwa tuanze na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Sasa naomba wale wengine tayari nawashukuru sana wameniletea habari wamesema wanaandika

watapeleka kwa maandishi na wengine wengi wajitokeze kupeleka kwa maandishi ili tuweze kwenda na wakati. Nawaomba sana Waheshimiwa.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako dakika zangu mbili baadae unipe. Mimi napenda kuwasifu wakulima wetu hasa wa mpunga, nawasifu kwamba ni watu ambao ni wachambuzi wa hasara na faida. Nazungumza haya kwa sababu jana tumesema kwa nini wanapanda miwa katika mabonde ya mpunga.

Mhe. Naibu Spika, gharama zimekuwa kubwa sana za ukulima wa mpunga katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kwa mfano, kuchimba kwa trekta hekta moja ingekuwa serikali inayo trekta ni shilingi 25,000 *private* ni shilingi 40,000 na kuburuga ndio hivyo hivyo. Kupanda shilingi 12,000 au 13,000 kupalilia karibu shilingi 40,000, kuvuna shilingi 20,000, mbegu 30,000. Kuna mbolea shilingi 10, 000 kama itapatikana kuna na mbolea tena shilingi 10 kama itapatikana, kuna dawa kama itapatikana, imefikia muda lita moja sasa hivi wanagawana wakulima wawili. Kuna usafiri ukitizama kuna zaidi ya shilingi 200,000 kwa hekta kwa gharama za serikali je, ingekuwa *private*.

Kwa hivyo, wakulima kukimbia kilimo hiki wakaanza kupanda mihogo zao ambalo serikali soko liko tayari, miwa soko liko tayari sio watu wa kulaumiwa, wa kulaumiwa hapa ni serikali yetu ambayo inashindwa kuweka pembejeo kwa wakati na vitu vyengine. Kwa hivyo, wakulima wasilaumiwe kuacha kupanda mpunga wakachukua mazao mengine.

Mhe. Naibu Spika, lawama yote hiyo, Tanzania Bara wanavuna tani 1.5, Asia tani 4.4, Zanzibar ni tani 1 kwa hekta na hiyo unaigawa tena kwa 2.5 tutapata kama 400 na 400 hizi zinakuja kama hakuna mvua, mafuriko, hakuna jua, na vitu vyengine vingi. Kwa hivyo, ni kwamba huu ukulima unaonekana moja kwa moja hauna faida.

Katika hili naiomba serikali kwa sababu haina uwezo wa kuwasaidia wakulima hawa kipembejeo na kwenye *private* hakwendeki, basi wakulima wetu waachiwe kutumia mabonde haya kwa vilimo vyengine vyote ambavyo vinaleta faida, hapo watakapoona mpunga una faida kwenye mabonde watarudi.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo akija hapa atupe uzalishaji wa mwani kwa hekta moja, gharama zake, faida kwa hekta na mwisho atupe ushauri wake. Kwa sababu maneno yamekuwa mengi kuhusiana na ukulima wa mwani sasa ana wataalamu wengi lakini pia atupe picha

ukulima huu ukoje ili wananchi wa Zanzibar Unguja na Pemba wajue kuuacha ama kuukamata.

Jengine wenzangu wamezungumzia mbegu ya mpunga ya *NERICA*. Mheshimiwa mimi ni mtu mmoja ambae natoka maweni kwetu Kusini huko, sijawahi kuona mpunga ukipandwa maweni na kuna *nursery* iliwekwa Makunduchi kwa ajili ya mbegu ya mpunga huu. Ninavyofahamu mimi maweni iwe Makunduchi, Micheweni ni maeneo ya kupanda mbaazi, kwa kwetu Kusini Viazi Tona na vitu vingine. Pia *nursery* ya mbegu hii iliyowekwa Bambi wasiofahamu Bambi ni sehemu ambayo inatoa viazi vitamu pamoja na vitu vingine. Sasa wakati tunafanya tafiti ya vitu hivi bora tunyamaze kimya tusiwaambie watu na hasa kwa sababu tunaitwa wataalamu.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri akija hapa atupe maelezo kwa kina kama wenzangu walivyozungumza mbegu hii ikoje na sasa hivi iko wapi. Kitu ambacho kimeniuma zaidi kuachwa Mhe. Rais asubuhi anaitangaza mbegu hii ambayo kwa kweli haikutufikisha popote. Ni aibu kwa wataalamu wetu kumzunguusha Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwenye hotuba ya Rais ukurasa wa 28 wizara hii imezungumzia kuimarisha badhi ya mazao pamoja na viungo. Ningependa Mhe. Waziri wa Kilimo akija hapa atujuilishe ama atwambie viungo hivi viko wapi, kuna pilipili manga, hiliki, kungu manga, tangawizi, kuna na mazao ya alizeti; atwambie mazao haya yako wapi na idadi za hekta.

Mhe. Naibu Spika, fahamu yangu Zanzibar inaitwa *spice island* (nchi ya viungo) nchi inayonukia vizuri lakini ukweli wa mambo hatuna viungo. Kuna viji-*plot* vidogo vidogo vya watu binafsi Ndunduke, Kizimbani na maeneo mengine ya Magharibi lakini Kizimbani hasa kama ni wizara basi hatuna. Kwa hivyo, namuomba waziri akija atutajie hizi hekta ziko wapi na kaimarisha wapi kwengine.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katika kitabu chake anasema kwamba ana miche 24,278 ya *spice*. Sasa swali langu ni wapi na miche hii ya aina gani imepandwa. Kwa ufupi Mhe. Naibu Spika, hatuna viungo katika nchi yetu lakini Mhe. Waziri akija atatusaidia zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kwenye hotuba ya Rais Wizara iliyokuwa ya mifugo wakati huo ilitamka na nai- *support*.

Wizara ya Kilimo na Mifugo inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa ardhi kutokana na kuogezeka kwa idadi ya watu na kupanuka kwa shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mhe. Naibu Spika, huu kweli wa mambo sasa hivi Zanzibar hatuna maeneo ya kilimo, ukitizama Fuoni Wilaya ya Magharibi mote mna nyumba kuna vitu vyengine sasa hivi huwezi kulima tena minazi kama alivyosema mwenzangu yote tumeikataka. Kwa maana hiyo kwa hali halisi na kwa nia njema na kwa dhati yangu naishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika muda unaokuja kutafuta wataalamu wa nje na ndani ya Zanzibar kufanya *research*, kuiondosha tena hii Wizara ya Kilimo na kuleta Wizara ya Bahari.

Nazungumza haya kwa sababu Mhe. Naibu Spika, bahari iko hapo nyuma iko huku, bahari iko kila *corner*. Tuna - *resource* za kutosha ambazo zipo kwenye bahari na ingekuwa samaki wanafanya mikutano basi nadhani wangekuwa wako hivi hivi wanauliza huko duniani kweli kuna wavuvi. Sasa cha muhimu kwetu sisi ni kutafuta zana za kutafutia samaki hawa. Lakini ukitizama kwa Wizara ya Kilimo tena Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi hiki tija haipo na hata ukitizama kitabu hiki katika michangio ya serikali yote iko *billow* 50 hiki hapa sio mimi. Mazao yenyewe hamna kwa hivyo naishauri tena serikali tuanze Wizara ya Bahari kilimo iwe kituo tu cha kwenda kufanyia mazao mengine lakini sio wizara ambayo kwa kweli itakuwa haina tija kwa hapo baadae.

Mwisho kutoka na hali hii namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo akija haja na hali halisi ameisikia nimuulize lile eneo letu la Makurunge lipo wapi? Ili tupate muda kwa sababu hatuna ardhi ya kutosha twende kwenye eneo letu ambalo tulipewa liko wapi lina idadi ya hekta ngapi na kama lipo na kama halipo liko wapi limekwenda wapi na kwa nini.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukuwa fursa hii kwanza kukushukuru na mimi kunipa nafasi kidogo kuchangia moja, mbili katika Wizara ya Kilimo, nashukuru sana. Lakini leo si siku kwa sababu wachangiaji ni wengi mimi nataka niende mbio mbio.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika mchango wangu leo inajikita hasa kwenye zao moja tu la karafuu. Mhe. Naibu Spika, mimi nampongeza sana waziri na namsifu na napenda kuchukuwa fursa hii kusema kwamba ana wakati mzuri wa kuyatekeleza yale aliyoyaandika. Mimi nasema kwa upande wangu na ni vyema sote tukampa mashirikiano waziri, ili kutekeleza yale aliyoyaandika

katika kitabu hiki ili kama kuna jengine mwakani tukaja kumuuliza tukawa na uhakika, kwamba wewe ulituahidi utafanya hili lakini hujafanya. Lakini ni vyema tukamchangia mawazo baadae tukaja kumuuliza.

Mhe. Naibu Spika, mimi niko katika kufungu chao walichokitaja hapa cha Kuongeza uzalishaji na kuimarisha ubora wa zao la karafuu. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua sisi karafuu ndio zao muhimu katika nchi hii. Lakini tukubali sote kwamba mikarafuu kwa asilimia kubwa imeanza kupotea na nasema itaendelea kupotea ikiwa hatua za dharura hazitachukuliwa na tutachukuaje Mhe. Naibu Spika, hatua za dharura.

Mimi ushauri wangu kwa wizara ni kuimarisha zaidi Idara ya Utafiti. Kwa sababu hapa nimeona kwamba wamezalisha miche mingi wameeleza na wamegawa miche na wameweza kuzalisha miche 241,300/=, kwa Pemba ni miche 106350/= kwa Unguja na kuifanya jumla ya miche hiyo iwe 347650/=. Lakini miche imegaiwa tayari mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri baada ya kwisha kugawa hii miche kuipeleka kwenye vitalu je, kuna utafiti wowote uliokwisha kufanywa wa kuhakikisha kwamba hii miche iliyopelekwa imeshika, imestawi na inaendeleaje. Kwa sababu hapa ili tuweze kuitunza vizuri hii miche ni lazima tufanye utafiti wa kilimo kutoka miche yenyewe udongo, maji na mengineyo ili kuhakikisha kama hii miche yetu baada ya kuipanda inakuwa.

Je, jambo hili linafanyika maafisa wake, wataalamu wake wamelifanya na kama hawajalifanya kwa nini hawajalifanya. Kwa sababu kama hawajalifanya itakuwa ni sawa sawa na uliechukuwa kitu au ulichukuwa jiwe ukenda kulirembea kwenye bahari hukuti kitu na maslahi yake hupati chochote. Kwa hiyo, ili tufanikiwe ni lazima tuhakikishe kwamba wataalam baada ya kuigawa miche hii wanarudi mashambani kwa wakulima kufanya utafiti kwa kina kujua kama kweli miche hii inakuwa, inakubali na imestawi kama inavyostahiki katika mashamba waliyoipeleka. Hili Mhe. Naibu Spika, nataka jibu vizuri kidogo.

Pia kuna huo mkakati wenyewe wa kuongeza hilo zao. Kama tunavyojua baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 Serikali iliyachukuwa mashamba na ikayakata hekta ikawapa wananchi hekta tatu tatu. Lengo la serikali ilikuwa ni kuyatengeneza na kuyastawisha yale mashamba yawe kwa ajili ya wananchi. Lakini je, tujiulize mpaka leo mashamba haya waliopewa wananchi bado yako hai, mikarafuu imo na kama haimo kwa sababu gani haimo.

Mhe. Naibu Spika, jibu naweza kujisaidia mwenyewe kwa sababu ni jambo ninalolijua. Tatizo lililotokea hapa ni kwamba baada ya serikali kuihamisha Idara ya Mashamba ya Serikali kutoka Idara ya Ardhi kuipeleka Wizara ya Kilimo iliipeleka kwa nia safi kwa mambo matatu au manne.

(1) Kuongeza ufanishi
(2) Kuongeza makusanyo

Kuoengeza idadi ya hiyo mikarafuu yenyewe, kwa sababu iliona kwamba ardhi wao watashughulika na ardhi tu. Lakini ikenda kilimo itakuwa ina wataalamu ambao watasaidia kuiendeleza hiyo, mikarafuu.

Mhe. Naibu Spika, cha kushangaza hawa... nisamehewe kidogo kama nitatumia lugha itakayokuwa haijaridhisha niseje kupigwa kanuni kwamba wanasema "Tutachungaje ng'ombe na wakati maziwa tunapata". Namaanisha haya kwa sababu wao wanachokifanya ukifika msimu wa kukodisha mashamba wanakodisha mashamba lakini hakuna kitengo ambacho kimewekwa maalum cha kuyasafishia na kuyaendeleza hayo mashamba yenyewe.

Sasa Mhe. Waziri utakapokuja nitaomba uniambie je, hiki kitengo cha kuyahudumia mashamba ya mikarafuu yaliko chini ya Idara ya Mashamba ya Serikali kipo kama hakipo ni kwa sababu gani hakipo. Mimi najua ukusanyaji wa mapato umekuwa na unaashiria hivyo. Tunawapongeza sana watu wa Wizara ya Kilimo kupitia Idara yao ya Mashamba kwa kazi nzuri wanayoifanya, hongereni sana. Lakini hili moja la utunzaji kwa nini hatulioni matokeo yake, kwa hivyo Mhe. Waziri mimi nataka jibu hili.

Pia jambo jengine nilikuwa nataka nijue kwamba kwa nini hiki kifungu cha matengenezo ya karakana cha shilingi bilioni tatu, milioni mia tatu na thamanini na mbili laki nne na sabini mbili elfu huoni kwamba ni vizuri kifungu hiki kikafanyiwa kasma kwa mipango yenu wenyewe na mkakipeleka kwenye Idara ya Utafiti utakipa nguvu, ili kuweza kukuza lengo hili la kuiendeleza hii mikarafuu.

Kwa sababu zao la karafuu ndio zao lililokuwa linategemewa katika nchi hii. Leo tukiliacha kama hatujalifanyia bidii ya makusudi tukalipa nguvu tutafika pahala tutakuja kujilaumu wenzetu leo Indonesia sisi ndio tulikuwa wazalishaji wazuri wakubwa wa zao la karafuu. Lakini leo kwa Zanzibar sijui ni nchi ya ngapi, ubora wa karafuu yetu upo ni jambo la kushukuru tunafurahi lakini uzalishaji kwa nini ushuke.

Mimi namshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni kiongozi wa kupigiwa mfano ni muokozi wa sisi wakulima wa karafuu wa Pemba kwa kutupa asilimia 80%, Mwenyezi Mungu amjaalie ampe hekima na busara, ana imani ya kweli na sisi. Kwa hiyo, mimi nasema na naiomba sana wizara imani aliyoionesha Mhe. Rais kwa kukuteuwa wewe Mhe. Waziri ana imani kwamba jambo hili utaweza kulisimamia vizuri na mimi nakuomba uendeleze juhudi zako za kulisimamia zao la karafuu liendee kuwa uti wa mgongo wa taifa hili.

Mhe. Naibu Spika, mimi nashauri kwamba Wizara ya Kilimo kupitia idara yake ya mashamba ya serikali yaendelee kubakia na mashamba yake makubwa tu yale waliyokuwa nayo zamani, yale mashamba waliyopewa raia ambayo wanasema kwamba kisheria walitakiwa wakamilishe taratibu wawatake wananchi wakamilishe taratibu wayarudhishe kwa wananchi haraka, wananchi tuwawekee masharti ya kuyatunza na kuyaenzi wayapande mikarafuu. Kwa sababu Wizara na Idara ya misitu ambayo mashamba hayo yako chini yake hayana uwezo wa kuyapanda mashamba haya, wenye uwezo wa kuyapanda mashamba haya ni wananchi.

Kwa hiyo, mimi naomba sana Mheshimiwa suala hili ulichukuwe na ulifanyie kazi na uitake idara yako ya misitu ambayo ndiyo inayosimamia mashamba haya kwamba watoe mashamba kwa wananchi, ili ile azma ya kuzalisha miche ipatikane, iende mashambani ikapandwe na tija baada ya miaka mitano, saba ianze kuonekana. Wananchi wanaopewa mashamba wapewe masharti kwamba lazima ndani ya kipindi maalum uwe shamba lako ulijaze mikarafuu au kama ya minazi ijazwe minazi.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumaliza nilikuwa nasisitiza na mimi kama wenzangu idara inazalisha miche ya mikarafuu, inagawa miche ya mikarafuu lakini kwa nini sioni kugawa miche ya minazi na tuna tatizo la upungufu wa minazi. Wewe mwenyewe umekiri kwamba Zanzibar minazi inapotea kwa nini tusiweke minazi ya makusudi wa kuirejesha minazi ambayo imepotea.

Mhe. Naibu spika, mimi sitaki niseme sana natoa nafasi kwa wenzangu. Lakini baada ya haya napenda kutamka wazi kwamba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia na nawaomba wenzangu waiunge mkono tumpe jukumu waziri na wasaidizi wake wafanye kazi mwakani, tuje tuwahoji kama hawakufikia malengo. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi hii nilikuwa na mambo madogo madogo tu hasa baada ya michango mizuri ya Waheshimiwa walionitangulia.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitoe pongezi sana Mhe. Naibu Spika, kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wote wa Zanzibar kwa kuisaidia nchi kuondoa lile pengo la chakula kwa mfano tunaambiwa kwenye mbunga au kwenye mchele asilimia ishirini ndio inazalishwa hapa na hiyo thamanini ndio inayotoka nje na mpunga wetu tunaupenda, mtamu, mzuri ingawa una matatizo tu ya uzalishaji wake.

Lakini *full security* ya nchi Mhe. Naibu Spika, inatokana hasa na haya mazao mengine ndizi, muhogo, mashelisheli hiyo ndiyo *full security* hasa yetu tunajua kwamba mchele ndio *number one.* Lakini Ramadhani kama hii wapo wanaofutari wali, lakini uongo mtu asipopenda muhogo, ndizi, boga na hayo *alhamdullilah* hayaagizwi nje. Kwa hiyo, kwa kiwango fulani tunawashukuru sana wazalishaji wetu wadogo wadogo.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mambo ya msingi sana katika wizara hii ambayo yamejumuisha kilimo chenyewe au mazao, mifugo, uvuvi, maliasili na misitu pamoja. Ni masuala matatu mimi nimeyaweka pamoja.

(1) Uzalishaji yaani *Production*
(2) Utafiti
(3) Elimu kwa wafugaji, wakulima na wazalishaji wadogo wadogo kwa jumla

Sasa haya mambo mawili ya utafiti na elimu kwa wakulima na wafugaji haya ni ya wizara yenyewe. Kwa hivyo, haya Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri haya ni mambo ya msingi ya wizara na haya hayana budi lazima wizara iyasimamie.

Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa nne kwenye kiambatanisho cha 1 na kwenye ukurasa wa nne alitoa *trend* ya uzalishaji mazao kwa nchi yetu na inafurahisha na *trend* hii inaonesha kwamba yamekuwa mazao yanaongezeka kataja mazao yote kataja kwa ujumla, *trend* inaonesha yanaongezeka. Lakini sasa pale alichotoa ni tani tu hatuoni yamezalishwa kwa eneo gani yaani hapa ingekuwa vyema Mhe. Waziri akatwambia hili ongezeko au haya mazao yaliyozalishwa mfano nasema nachukuwa mmoja tu zao la viazi vikuu limeongezeka kutoka tani 2115.85 mwaka 2004 hadi kufikia tani 2808.5 mwaka 2015. Mahindi kutoka tani 1558.5 mwaka 2014 hadi 2826.8 mwaka 2015. Lakini kwenye eneo gani?

Sasa ingekuwa vizuri sana Mhe. Waziri angetwambia hapa. Eneo linalozalishwa ni hekta na kilichopatikana *production* hekta fulani. Halafu akatupa wastani sasa *minimum yield per unit area*. Yaani eneo la uzalishaji linalozalishwa kwa eneo fulani. Hapa tutampima Mhe. Waziri kwamba kweli kakitoa kilimo chetu kutoka mfano nasema mpunga wa umwagiliaji maji, *potential* ni *tons* nane mara mbili kwa mwaka kwa hekta. Sasa tutampima Mhe. Waziri baada ya miaka mitano Mheshimiwa kaweza ku- *achieve* hii. Hili ndilo suala la msingi sana.

Mhe. Waziri mimi simlaumu yeye. Mimi ninawalaumu rafiki zangu kwamba hili ninafikiri kidogo hawakumuongoza vizuri Mhe. Waziri. Kwa sababu hili ni suala la msingi kabisa. Kipimo cha uzalishaji ni kuonesha *yield per unit area* kwa kiwango gani unazalisha kwa eneo. Hapa ndiyo tutakupima Mhe. Waziri baada ya miaka mitano, umetoka hapa, umetuweka hapa na si hapo tu, hata kwenye ng'ombe wa maziwa.

Ng'ombe wa maziwa tunam-*judge*, ng'ombe huyu anatoa lita ishirini kwa siku, huyu lita kumi kwa siku. Ndiyo tunamchagua yule ng'ombe mzuri sana ndipo tunawapa wakulima. Sasa nilikuwa ninahisi hili kidogo Mheshimiwa ningemuomba sana alirekebishe. Na nimefurahi sana kwamba kuna tafiti za takwimu za mazao ya kuweza kufanya *estimate*, wamesema wamepata msaada wa *FAO*, wao wanaita *small area estimate*. Ninafikiri itasaidi sana. Mabwana shamba hao, maafisa ugani hao walioko katika Wilaya wakitumia njia hii ndiyo bwana shamba hasa. Lazima aweze kukisia. Kwa eneo hili hapa mpunga uliozalishwa ni kiasi gani.

Mheshimiwa naomba niende haraka haraka. Pili kwenye ukurasa wa 6, umetwambia kwamba kunaonesha kumekuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya nishati ya kuni. Ni kweli kwa sababu watu wetu bado wengi wanategemea kutumia kuni kwa kupikia. Sasa nilitaka kumuuliza Mhe. Waziri tu. Je, msitu ndiyo tunaomaliza. *What is the way forward*?

Kulikuwa na programu huko nyuma za kilimo mseto za kuchanganya. Je, programu ile ilikuwa *pilot project* na zimeanza vizuri. Ndiyo unaona mashamba ya mivinje yapo, mashamba ya mikaratusi na nini. Je, programu ile inaendeaje. Msitu tunaumaliza. Wakulima wetu tunawashauri nini. Ninafikiri ingekuwa vizuri Mhe.Waziri akaja akatueleza.

Mheshimiwa tuna matatizo makubwa sana ya udhibiti wa nzi kwenye ukurasa wa 20 kalizungumza hili, "udhibiti wa nzi waharibu wa matunda". Kwa kweli kwenye embe Mhe. Hassan kazungumza, sasa kwenye mapapai. Si nzi tu lakini

kuna *meals bug* wale kwenye mpapai, minanasi na hasa baya zaidi kwenye mpapai. Sasa kwa kweli mapapai mengi yameathirika. Sijui Wizara, ninajua inalijua lakini tunawaongoza vipi wakulima wetu. Ndiyo yale niliyoyaeleza zile kazi za msingi za wizara *(plan plantation).* Ni suala muhimu sana tuelekeze ipasavyo wakulima wetu wachukue njia gani za kuwadhibiti.

Mheshimiwa kwenye ukurasa wa 20 huo Mhe. Waziri kaelezea kwamba tumeingiza au pwani pale wamekagua tani elfu sita, mia nne sabini nukta tano za mboga mboga, matunda na nafaka. Leo ni jambo la kawaida pale inakuja *Flying Horse.* Kuna *trays* au *cartons* za tungule. Sasa wale maafisa wetu (*Producers Inspectors)* pale pwani wanadhibiti kweli au wanapitisha tu biashara. Hatukatai, hatuwezi kuzalisha hapa tungule ipasavyo, mabilingani na vyenginevyo. Lakini bado suala la udhibiti. Kama si hivyo Mhe. Naibu Spika, kama walivyoingia *cassava meal bugs* na walivyoingia wadudu wengine waharibifu, tulikuwa tunachukua mipera kutoka nje ya nchi, tumeyaleta hapa, mipera yote imeugua hasa ile tunayosema mipera ya Thailand (makubwa yale), basi mengine mpaka ukiacha mipera yetu ya asili.

Sasa suala la udhibiti pale bandari na *airport* Mhe. Naibu Spika, wa mimea ni suala la msingi. Ningemuomba sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hili ajitahidi sana alidhibiti. Bado Zanzibar tuwe *safe* na maradhi ya minazi haya, yale ya *yellow motor virus*. Bagamoyo hapo minazi yote utaona kule juu imeungua kama imepigwa na radi, si radi ndiyo maradhi yale. Sasa kama tunaingiza nazi na tunaingiza na miche ya minazi Zanzibar, hiyo minazi iliyobaki nayo itakuja kwenda zake. Kwa hivyo ninakuomba sana Mhe. Waziri hili maafisa wetu walisimamie ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 35 napongeza sana suala la kuwaendeleza wanafunzi wetu kwenye fani mbali mbali za kilimo. Wamezungumza hapa kuna *PhD* moja, *MC* tano, *DC* kumi na moja zipo mafunzoni. Ni suala zuri na mimi ninaliunga mkono mbali ya *Diploma* na *certificate*. Lakini ninataka kujua tu. Je, hawa maana munasema wizara wenyewe, hawa wanalipiwa na Mfuko wa Elimu ya juu au munawalipia wenyewe. Nilikuwa ninataka kufahamu tu kama maana yake mfuko wa Elimu ya juu wanalipa au kama munawalipia wenyewe, kwa nini mulipie wenyewe na Mfuko wa Elimu ya Juu upo, ili nyinyi mu-*save* pesa zitumike kwengine.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 73 kumezungumziwa suala la uvuvi bahari kuu. Na nimefurahishwa sana kwenye jadweli pale imeonesha *projection* yenu mwakani munatarajia kukusanya bilioni moja kutokana na mauzo ya leseni. Ni suala zuri lakini nilitaka kufahamu mwaka uliopita labda *trend* tu kwa miaka

mitatu minne ilikuwaje. Kwa sababu tumepata salamu kidogo mambo hayakuwa mazuri. Kulikuwa kidogo na mizozo kati ya baadhi ya *prospectives*, wale wanaotaka kuleta meli na wizara, ilikuwa kama kidogo kuna kushutumiana.

Sasa ningeomba sana. Wapo ambao wao ndiyo *volunteers* wa suala hili la uvuvi wa bahari kuu la wao ndio waliowashawishi hao watu walete meli. Sasa kumekuwa na mgogoro ndani, na matokeo yake wale ma-*urgents* wao wakasema aah! sisi tunaacha hii kazi. Lakini wana uchungu na nchi yao kwa sababu wengi ni Wazanzibari hawa watu. Kwa hivyo ningekuomba Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hili suala ulitazame, tuone kwamba tuna- *prospect* kwenye uvuvi wa bahari kuu. Na hawa wenye meli, ma-agent wapo tayari kutusaidia katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 26 unazungumzia suala zima la miche iliyooteshwa. Nimefurahi sana na inafurahisha sana vitalu vyetu vimezalisha miche milioni moja, laki nne, thamanini elfu mia mbili ishirini na nne kwa miche mbali mbali. Inafurahisha sana na miche kwa kweli inachukuliwa sana, *alhamdulillah* watu wanapanda ipasavyo. Sasa mimi naomba kidogo Mhe. Naibu Spika, kumuomba Mhe. Waziri afanye kama mpango wa *follow up mission.* Ndiyo miche inachukuliwa inapandwa lakini inatunzwa, inashughulikiwa, inapaliliwa.

Utakuta kama ile ya *budding*, michungwa ya *budding* au zamani tunaita kwa jina la Binti Juma, baada chini kuna mlimau, juu kuna mchungwa hayatolewi yale machipukizi basi mingi inageuka milimau. Na badala yake baada ya kutarajia michungwa unapata milimau na hiyo ni mingi sana. Ukichukulia miche ya michungwa tokea 19*18's* huko iliyopandwa Zanzibar hii. Ninafikiri ingekuwa hivyo viwanda *juice* anavyozungumza Mhe. Waziri vingekuwa vingi sana Zanzibar. Lakini kwa kweli mingi imekufa, mingi haikushughulikiwa. Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri afanye utaratibu wa *follow up mission* kwa hawa mabwana mashamba au maafisa ugani wake. Tujue kweli ile miche iliyopandwa mingapi mizima na mingapi mibovu.

Mhe. Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 65 Mhe. Waziri kazungumza suala zima la uvamizi wa maeneo yote ya kilimo, maeneo mengi ya kilimo, ni ukweli. Leo ukipita kwenye mabonde ya mpunga Mhe. Naibu Spika, utakuta viwanda vya matofali kwenye mabonde ya mpunga, pale Kijitoupele tu, nenda Mwera na kwengineko mwingi barabarani, watu wamemega ardhi wamefanya viwanda vya saruji...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika nne, malizia.

Mhe. Mwinyihaji Mwadini Makame: Naam!

Mhe. Naibu Spika: Malizia umekibaza dakika kama nne au tano hivi.

Mhe. Mwinyihaji Mwadini Makame: Ninakushukuru, ahsante sana ninamalizia.

Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Naibu Spika, tujue hawa vijana vile wamepewa na nani. Wamepewa kihalali au watu wanavamia tu. Kwa kweli kidogo haipendezi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema suala la muhimu sana na wenzangu wamezungumza suala la uzalishaji mbegu. Tumeambiwa kwamba watazalisha *tons* mia mbili hamsini za mbegu za mpunga kutoka kwa wakulima na kwa mikataba. Mimi nilikuwa ninajiuliza. Hivyo kweli Wizara ya Kilimo mabonde yetu tuliyonayo Mhe. Naibu Spika, kama Cheju. Chukulia Cheju kwa mpunga wa juu, Kibokwa, Kibonongwa, Chaani huko tushindwe kuzalisha *tons* mia mbili hamsini. Hatukatai wacha tufanye *contract farming* na watu wazalishe, lakini mbegu zile za wakulima wengine zinachanganyika, huipati ile *pure pride*. Sasa ningemuomba sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri suala la uzalishaji mbegu *at primarily level*, zile *seed sip*, (mbegu za msingi) azalishe mwenyewe kwa kutumia wataalamu wake. Inawezekana kabisa hilo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa ningemuomba sana alisimamie sana suala la ukodishaji mashamba ya serikali. Kidogo tunasikia kwenye redio mashamba ya mikarafuu, mashamba ya midoreani, mashamba ya serikali yanakodishwa. Lakini ukenda pale kama haipendezi kwa kweli. Ninafikiri munanifahamu ninachotaka kukisema, wanakwenda watu wanapewa karatasi tu, anakabidhiwa tu mashamba. Tunamelalamikiwa sana na watu hasa kwenye kizio cha Kizimbani, Machui huko na kwengine. Kidogo kuna hali isiyopendezesha. Ningeomba kama mnada iwe mnada kweli.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuiomba sana serikali suala la pembejeo. Suala la pembejeo ni suala la msingi sana kwa wakulima na hasa mbolea. Huwezi kumwambia mkulima wa mpunga azalishe mpunga ipasavyo kama humpatii mbolea inayostahiki na wamezungumza Waheshimiwa hapa. Mbolea tunayotaka hasa kwenye ukuzaji ni mbili tu, ni *"N"* na *"P"*, yaani *Nitrogen Source* na *Phosphate Source* na *urea* na hiyo tunayozungumza

phosphate. Hizo mbili kwa kweli ziende kwa mujibu wa maeneo ambayo tunataka kupanda mpunga. Bila ya mbolea kwa mpunga kwa kweli, maana yake utafiti umeonesha una-*duplicate* mazao yale kwa eneo. Sasa bila ya mbolea kwenye mpunga, mahindi na hasa nafaka, huwa kweli unajihangaisha bure. Hivyo ningeomba sana wizara ilisimamie hili ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, nimejitahidi nilikuwa na *points* ndogo ndogo nyingi hizi. Lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri, kwa kweli kitabu kizuri, mambo madogo madogo tu ya kuwekwa sawa. Ninaamini na sisi kama Wawakilishi tutachangia, tutashajihisha kuweza kufanya kilimo chetu kiwe kizuri.

Mhe. Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ninakushukuru. Mhe. Hamza Hassa Juma naomba sana utumie muda mchache sana, jitahidi kama unavyoweza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kama kawaida yangu nitajitahidi nitumie muda mfupi.

Ninawapongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote. Kwa hivyo ninakuja moja kwa moja kwenye hotuba. Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nianze na mchango wangu katika eneo ambalo wenzangu wameligusia la mpunga wa *NERICA*. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mimi katika watu ninaosikitika sana kwenye eneo hili ni mimi, kwa sababu kwa kweli mimi baada ya kupata taarifa kuwa kuna mpunga wa *NERICA* ambao utalimwa mpaka nyuma ya nyumba. Basi mimi nimejitahidi kuwahamasisha watu wangu, nikawaambia sasa maeneo yao wayaweke vizuri kwa ajili ya kulima mpunga. Lakini matokeo yake mpunga ule, kwa wakulima waliowahi kulima hizo siku mbili tatu, wamesema mpunga wenyewe hata *taste* yake haipendezi, sijui mgumu na nini, wameuwacha kabisa.

Kwa hivyo inaonesha hatukufanya utafiti wa kutosha. Sasa ninadhani Mhe. Naibu Spika, Mhe.Waziri akija aje atwambie basi je, ule utafiti wao walioufanya ulikuwa una changamoto gani na je, ule mpango kama unaendelea, utaendelea kwa utaratibu gani na kama unaachwa, utaachwa kwa utaratibu gani.

La pili Mhe.Naibu Spika, kitu ambacho chengine kwa kweli sikuridhika nacho sana katika hili suala zima la programu ya maendeleo ya mifugo. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli programu ya maendeleo ya mifugo labda ninukuu kwenye

ukurasa wa 37. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ametwambia, "Programu ya Maendeleo ya Mifugo jukumu lake kubwa ni kuendeleza sekta za mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake. Programu hii imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni programu ya uzalishaji wa mifugo na programu ya utabibu wa mifugo".

Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu nimezungumza jinsi mipango ya serikali yetu wakati mwengine haiangalii sana mahitaji ya wananchi wetu. Mhe.Naibu Spika, Zanzibar sasa hivi moja katika kilio kikubwa cha vijana wetu mpaka watu wazima ni suala la ajira. Mhe. Naibu Spika, laiti kama ingelikuwa wizara hii haya maneno waliyotueleza kwenye vitabu yangekuwa yanatekelezwa kwa vitendo, basi sisi tungekuwa hatuna tatizo la ajira. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, programu hii ya mifugo kwa kipindi kile cha nyuma ilikuwa ikichangiwa mpaka na ile programu ya *TASAF*. Mhe. Naibu Spika, wananchi waliitikia wito wakafuga kuku wengi sana. Matokezeo yake, ndipo pale niliposema programu zetu wakati mwengine haziangalii mahitaji ya wananchi. Mhe. Naibu Spika, wafugaji wa kuku walikuwa ni wengi na hasa akinamama. Walikuwa matatizo yao mengi madogo madogo ya matumizi yao ya nyumbani walikuwa wanajisaidia kupitia ufugaji wa kuku.

Mhe. Naibu Spika, hata mimi katika jimbo langu nilikuwa na programu ya ufugaji wa kuku. Baada ya kuanza kuruhusu, serikali kuingiza hawa kuku maarufu wanaitwa *Perdue*. Na ninaomba radhi kwa kusema neno *Perdue*, kumbe hii *Perdue* ni jina la kampuni fulani inayoleta hawa kuku. Kwa hivyo tunapozungumzia *Perdue*, hatuzungumzii labda tatizo la kampuni, tunazungumzia uingizwaji wa kuku kutoka nje ya nchi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ndiyo nikasema kwamba hichi kitabu kwa haya maelezo aliyoeleza Mhe. Waziri yapo *negative*, siyo hasa yale malengo yaliyokusudiwa. Kwa sababu kama ingelikuwa ni hivyo programu hii ya kuendeleza mifugo ingelikuwa inalinda soko la ndani kama wanavyofanya wenzetu Tanzania Bara katika suala la sukari na vitu vyengine, hata kuku.

Wenzetu Tanzania Bara hawaruhusu kuingizwa kuku kule. Leo hapa tumeruhusu na hata kama mfano tungekuwa tunaruhusu kuingiza kuku, kungekuwa kwa masharti maalum. Kama mahitaji makubwa kwenye mahoteli, wangeruhusiwa wale kuku wauzwe kwenye mahoteli tu lakini katika soko la kawaida waachiwe wananchi wetu waweze kujitafutia ajira.

Mhe. Naibu Spika, matokezeo yake kushindwa kudhibiti soko hili la ndani la ufugaji wa kuku. Mhe. Naibu Spika, wafugaji wengi wameacha na ufugaji wa kuku kwa sababu ukiangalia bei ya paja nono, kwa kweli yule mfugaji hawezi akaingia katika soko la ushindani. Wenzetu Marekani huwezi ukaingiza bidhaa ambayo wao wanazalisha, watakupandishia bei na hata wale wafugaji wao kule Marekani wenzetu wanavyofanya, kama mfano yameingia maradhi au kuna changamoto yoyote wanawafidia wakulima wao au wafugaji wao ili waweze kuendelea na shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, leo tumeruhusu uingizwaji wa kuku, matokeo yake ajira ya watu wote ambao waliokuwa wanafuga kuku, pamoja na kwamba humu umezungumziwa ufugaji umeongezeka lakini bado siyo kama kile kiwango ambacho tulichotarajia. Mimi ninadhani hii elimu ambayo inayotolewa kwa hawa wafugaji, ingelitolewa wale wakafundishwa namna ya kufuga kuku bora wakafanana na wale kuku kubwa. Siyo wale kuku ambayo tunaoneshwa katika mitandao ya kijamii wanapigwa sindano.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, bado ninaomba serikali yetu ipige marufu kuingizwa nchini kuku hawa wanaotoka nje ambao wanakaa zaidi ya miezi minane, kumi huko; yapo baharini mpaka wanafika kwetu ili wananchi wetu hawa, warudi katika kuendeleza kilimo chao hiki cha ufugaji wa kuku.

Hapa hapa Mhe. Naibu Spika, nimekuja nimeangalia hata katika zile fedha ambazo waliingiziwa kwenye hichi kipindi kilichokuja. Hii programu ya ufugaji wa kuku ya maendeleo ya mifugo, nimejaribu kuangalia ukurasa wa 43 wa hichi kitabu katika hii programu ndogo ambayo wao kwenye fedha ambazo walizotegemea kuzipata. Kwa kweli wamepata asilimia 18 tu. Hivyo hapa usitegemee kwamba labda tungelikuwa na maendeleo haya ambayo tuliyokusudia.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa madawa ya mifugo. Vile vile tumepata karibu asilimia 18. Kwa hivyo hii inadhihirisha kwamba hii mipango yetu tunaizungumza kwenye vitabu lakini kwenye uhalisia *financial*, kwa kweli hayendi sambamba. Matokeo yake wananchi wetu inaposomwa bajeti na Mhe. Waziri wanajenga matumaini lakini katika utekelezaji kwa kweli hakuna matumaini yoyote.

Mhe. Naibu Spika, ninakuja katika suala la samaki. Mhe.Naibu Spika, sasa hivi tumepiga kelele kuhusu suala la *perdue* wa kuku, sasa hivi wanakuja *perdue* wa samaki, kwa kweli ni aibu kubwa katika nchi tuliyozungukwa na bahari pembe

zote. Hapa ikilia paaa! Huna pakukimbilia lazima upitie baharini, tumezungukwa na samaki.

Kuna Mhe. Mjumbe mmoja katika kipindi kilichopita alisema kuna samaki wameshaota ndevu na mvi na hawajawahi kuvuliwa wapo Zanzibar wamezunguka visiwa vya Zanzibar. Leo tunaagizia samaki kutoka nje. Mwenzangu kazungumza kuna mtu ana kontena 27. Leo ina maana hapa tunakuja kuuwa soko la wavuvi wetu.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi wafugaji wamekuwa wapiga virungu na wavuvi watakuja kuwa wapiga virungu. Kwa kweli suala hili mimi silikubali. Naomba Mhe. Waziri aje alitolee kauli hapa. Sisi tunavyotaka hawa samaki wasiingie nchini, kama samaki wanaingia nchini basi wawe samaki katika utaratibu maalum na kitoke kibali maalum, kama kuna mapungufu kwenye mahoteli. Maana yake wananchi huku hawana shida ya kuletewa samaki kutoka nje, wananchi wetu wanataka wale samaki *fresh* kama hao wenye mahoteli wanataka hao samaki kutoka nje, basi kitoke kibali maalum kwa waziri tena kwa *condition*, ikisha-*feed* lile soko basi wazuwie. Lakini tusije tukawatengenezea utaratibu wa kisheria ikawa sasa na wao waingize samaki huku, hii mipango yetu yote ya kuendeleza uvuvi na mengine yote itakuja ku-*fall*.

Mhe. Naibu Spika, kipindi cha nyuma kwenye miaka ya 2008/2009 tulipata semina moja kubwa sana Mhe.Naibu Spika, kuhusu programu ya kuwaendeleza wavuvi wadogo wadogo na iliandaliwa programu maalum. Kuna wale *Minai Conservation Area,* kuna *Pemba Channel Conservation Area* na huku kuna *PEPCA, MIMCA* sijui na nani wale.

Mhe. Naibu Spika, hawa wavuvi wetu wadogo wadogo walifika pahala wakaweza kuji- *organize* wenyewe, walikuwa wa- *organize* na Idara ya Uvuvi na sheria yao Mhe. Naibu Spika, iko wazi kabisa. Waliweza ku- *organize* vizuri wakawa tayari wanavua na wanalinda wenyewe yale maeneo. Ilikua inafika pahala wizara haipati tabu, wenyewe wananchi katika vijiji wanawalinda wale wavuvi haramu wanaokuja. Lakini leo Mhe. Naibu Spika, mpango ule labda Mhe. Waziri akija aniambie. Mpango ule kulikuwa kuna fedha ambazo zilikuwa zinapatikana kwa kupitia katika zile hifadhi, fedha zile zilikua zinakwenda wizarani halafu zinarudi tena kwa wale wafugaji kuwasaidia katika mambo madogo madogo wanapopata changamoto.

Kwa mfano, wengine walikua wanafika pahala wanakwenda wanakuta nyavu zao zimechukuliwa na meli, wanarejeshewa kwa kupitia mpango ule, wengine

pengine labda vidau vyao vimepata matatizo wanapewa pembejeo mbali mbali. Lakini leo mpango ule kwa kweli ukikutana na wale wavuvi wanalalamika sana, inaonesha hii Idara ya Uvuvi sasa hivi iko jina tu, ina maana hata kazi yake haifanyi. Nimejaribu kuangalia katika bajeti, hata hiyo bajeti yenyewe Mhe. Naibu Spika, kwa kweli haipendezi sana.

Mhe. Naibu Spika, nilijaribu kuivuta sheria. Nilikwenda kule katika *library* yetu, nilijaribu kuangalia ile sheria yetu ya uvuvi, sheria hii tuliipitisha mwaka 2010 na ilikua ina maelezo mazuri sana Mhe. Naibu Spika, nilijaribu kuangalia. Namuomba Mhe. Waziri pia na yeye ajaribu kufanya *reference* katika hiyo sheria, kifungu cha 6 kilikua kinasema;

> *"A director who shall be a professional officer in fishery and appointed by the president"*

Mhe. Naibu Spika, hebu tuulize huyu Mkurugenzi ambaye kwa mujibu wa sheria tumemtaja awe ni *professional*, hii taaluma yake anaitumia vizuri, tunataka tupate tu kujua. Kwa sababu yeye ndiye aliyetuandalia ile programu ya mwanzo, lakini programu hii haifanyi kazi vizuri, lakini bado nilipojaribu kwenda mimi nikauliza kuna tatizo gani.

Mhe. Naibu Spika, hii sheria imekuja kuvurugwa na kanuni, hizi kanuni walizokuja kuzitengeneza ina maana wamempopotoa mbawa, wamempopotoa nguvu ina maana leo baada ya yale maswali ya uvuvi kushughulikiwa na Mkurugenzi leo yanashughulikiwa na Katibu Kuu.

Mhe. Naibu Spika, hakuna sheria yoyote iliyoweka masharti ya kusema Katibu Mkuu awe na *profession* ya aina gani. Lakini tunapopitisha Wakurugenzi tunaweka na *professions* zao, kwa sababu tunategemea kutakuwa na *output* pale ambapo tutategemea kuipata. Mimi nimeshashiriki katika zoezi la kutoa maboti, kutoa nyavu na vitu mbali mbali mpaka mafriji yale.

Mhe. Naibu Spika, wavuvi kwa mara ya mwanzo wengine walinunuliwa simu kwa kupitia mpango huu. Yuko baharini kapata matatizo anapiga simu haloo, watu wanakwenda kumsaidia. Sasa hivi mpango huu umekufa.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka katika programu hii kulikuwa kuna maboti kama sikosei yalikuwa sijui 10 au 12, maboti ya doria yale. Hebu Mhe. Waziri akija aniambie ni mangapi yako mazima sasa hivi. Hii programu imekufa *total*. Mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, tuache siasa kwenye kazi, mimi nafikiri wizara hii kwa kuwa kwa muda wa miaka mitano walikuwa wanayo wenzetu CUF, inaonesha hawa walikwenda kuiua kwa makusudi, kwa sababu hawa

wavuvi wadogo wadogo ndio wapiga kura wetu. Mimi najinasibu ni mzaliwa wa Chaani, lakini asili yangu Makunduchi baharini. Asili yangu Pwani Mchangani baharini. Leo wananchi hawa ukenda wanalalamika, yaani kwa kweli hakuna utaratibu.

Sasa mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hii kanuni anaifanyia marekebisho waziri, naomba arudi kwenye kanuni aangalie yale maeneo ambayo mli- *over look* hii sheria, mrudi ili sheria iweze kufanyakazi yake, na amina tutaweza kufanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii kama nilivyosema ingejitahidi basi tatizo la ajira Zanzibar lingekua hakuna. Wajumbe wenzangu wamezungumza sasa hivi, kila siku ukenda pale bandarini kuna meli zinaleta mboga mboga zinaingizwa katika mahoteli. Kwa nini hatuna programu maalum ya kuweza kuwaandaa wakulima wetu wakaweza kulima hizi mboga mboga tukapeleka katika mahoteli yetu mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, hii ni Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na wameeleza humu katika kitabu chao, kutokana na muda sitopata kunukuu kwamba kuna maeneo ya kilimo yalianza kupungua. Mhe. Naibu Spika, ukiangalia sasa hivi, hekta tatu tatu ambazo alitupa Mzee Karume kwa ajili ya kilimo, sasa hivi hekta zile tunajenga halafu leo utegemee mazao yataongezeka, tutegemee kupungua. Kwa kweli Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi sijui wanafanya nini. Ukiangalia ukataji wa miti, Mhe. Waziri kazungumzia suala la minazi jinsi inavyokatwa. Mimi namshukuru sana na ninampongeza na aendelee na msimamo.

Mhe. Naibu Spika, kitu ninachotaka ni kwamba kama kweli Mhe. Waziri anakusudia kupiga marufuku ukataji wa minazi, basi avifunge viwanda vyote vinavyotumia mbao za minazi, vyenginevyo Mhe. Naibu Spika, hakuna suala litakaloweza kufanikiwa.

Jengine Mhe. Naibu Spika, hapa karibu tutakuwa hatupati mashelisheli, mafenesi wala hatupati chochote, kwa sababu ukenda kwenye hivyo viwanda vya kuchonga mbao, mali ghafi yao kubwa ndio hiyo mifenesi, mishelisheli, sijui miti gani. Itafikia pahala tutaagizia kila kitu hapa, tutakuwa kila siku tunakwenda hospitali sukari, *pressure* sijui nini na nini kwa sababu hatuli mazao yale yaliyokua ya asili.

Vile vile Mhe. Naibu Spika. Nimeshakuona hizo dakika zangu 5 nitamalizia sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika: Zimebaki tatu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Tatu. Haya. Mhe. Naibu Spika, bado maeneo ya kilimo yanajengwa, ukiangalia mabonde ya mpunga. Sasa hivi utafikiria serikali haipo. Leo unaukuta mpunga unalimwa, basi wakati wa jua kali unakuta tayari *foundation* za nyumba. Hawa Maafisa wa Kilimo wanafanya nini, hawa mipango miji wanafanyakazi gani.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kama nilivyosema kama hii wizara yetu ingefanyakazi yake vizuri, basi tatizo la ajira lingekuwa hakuna.

Mhe. Naibu Spika, mimi na wewe tulikwenda China katika msafara maalum. Kimoja ambacho Wachina walituambia. Sisi tuliwauliza nyinyi mmefanya mbinu gani mpaka mkawa mnapiga maendeleo ya kasi. Wakasema sisi tumeacha maneno tunapiga kazi. Sasa hebu na sisi tuwache maneno tupige kazi. Wao wakatuambia Zanzibar mkijitahidi katika zao la karafuu, mkijitahidi katika suala zima la uvuvi, basi wakasema Zanzibar hamtohitaji msaada wa mtu yeyote kutoka nje.

Mimi naomba Mhe. Naibu Spika, nakuomba sana Mhe. Waziri hebu fanya mawasiliano na Balozi wa China, akupe programu zile za kutusaidia uwapeleke vijana wakasome kule miaka mitatu au minne, wakirudi tuje tupate hiyo programu ya wao kuendeleza huo uvuvi ambao walituambia wao. Na hili pia naomba, bila ya kuwa na benki za kisekta kwa kutegemea mabenki haya ya biashara, basi tusitegemee kwamba wakulima wetu, wafugaji wetu na wavuvi wetu kama wataweza kuokoka.

Mhe. Naibu Spika, China kuna *Agriculture Bank*, kuna *Fisherman Bank*, kuna *Construction Bank* yaani kila taasisi, wenzetu wameandalia benki zao kwa ajili ya kuweza ku-*facilitate* na kuweza kutoa *capital* ambazo zinamasharti maalum ya riba, ambapo riba yake inakuwa sio kubwa malipo, yanachukua muda mrefu kwa ajili ya kuweza kuwasaidia wale wakulima wetu.

Mhe. Naibu Spika, jengine la kumalizia. Kwa kweli mimi naendelea tena kusikitika, haiwezekani serikali yetu na leo tunataka tupate kauli ya serikali. Haiwezekani sisi tunapitisha bajeti ya kilimo, wakulima wameshalima halafu leo wanatokea wendawazimu wanakwenda kuwakatia mazao yao.

Mhe. Naibu Spika, hapa leo tunataka serikali itupe kauli. Tuko *serious*, vyenginevyo hii bajeti itakuwa ile amezembea ng'ombe wa mbele anachezea

bakora ng'ombe wa nyuma. Hii bajeti tutazuwia mpaka tuambiwe serikali itachukua hatua gani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuukata mwembe wako mwenyewe kama huna kibali cha Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi basi huruhusiwi, na kama unaruhusiwa basi lazima ulipe. Leo watu wamekuwa kama wendawazimu, usiku watu wamelala Ramadhani hii anakoroma keshapiga uji wake asubuhi migomba haipo, unakwenda huko mpunga haupo. Mhe. Naibu Spika, tunasema kwa uchungu... *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, malizia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, tunasema kwa uchungu hatua zichukuliwe. Mhe. Naibu Spika, hotuba hii naiunga mkono kwa asilimia 40, ili nipate kauli ya serikali, lakini na yale masuala yangu niliyomuuliza Mhe. Waziri niweza kupata majibu ya uhakika. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nimembakiza mchangiaji mmoja na ameniomba sana kwa sababu hajawahi kabisa kuchangia na nimempa fursa hii kwa heshima yake, ili na yeye aweze kuchangia ni kwa dakika tano tu, naye ni Mhe. Said Omar Said wa Wingwi.

Kwa hivyo, baada ya kuondoka hapa mimi leo nimemaliza kwa siku ya leo, nitampisha Mhe. Spika, atakuja kuendelea. Kwa hivyo, baada ya kuondoka hapa Mhe. Spika, ataendelea na Mhe. Said Omar Said na wengine. Nawashukuru kwa leo.

(Hapa Mhe. Spika, alikalia kiti)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea. Naomba sasa nimpe Mhe. Said Omar Said ili amalizie mchango kwa upande wa Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Said Omar Saidi dakika tano tu tafadhali tumia.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataalla* kwa kuniwezesha kufika hapa na kuipata nafasi hii kwa wakati huu.

Mimi nichukuwe nafasi hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii pia nimshukuru Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa hotuba yake hii aliyoitoa, ambapo hotuba hii ikisikiwa na Wazanzibari, kwa sababu wako katika *attention* kwamba hotuba hii ni ya Wazanzibari na ni

maisha ya kila siku ya Wazanzibari. Kwa hivyo, Wazanzibari waliposikia hotuba hii wakati anasoma Mhe. Waziri walikaa *attention* wakafunga maduka, wakaacha kuuza na kununua kwa ajili ya kusikiliza hotuba hii.

Mhe. Spikwa, kwa kuwa muda haupo nataka na mimi niungane na mwenzangu aliyekaa kitako muda huu, kwanza kujua kwamba uchumi wa Zanzibar unatokana na kilimo, yaliyofuatia yote ya utalii na mengineyo yote yamekuja mbele ya kilimo, kilimo ndio peke yake kwa Zanzibar. Sasa kutokana na taarifa iliomo humu ya Mhe. Waziri kama walivyotangulia wajumbe wanzangu, kama tuliokopiana. Ingekua ataitimiza kama alivyoeleza humu basi ingekuwa hakuna tena tatizo la ajira hapa Zanzibar.

Kwa maana hiyo mimi kwa ufupi tu ningemuomba Mhe. Waziri ili kwa kuleta msukomo kwa wakulima wetu wa Zanzibar, basi atuletee kule majimboni mwetu wataalamu wazalendo. Kwa sababu wataalamu wako wa aina mbili, kuna watu wanaosoma kwa ajili ya watu. Sasa watu wanaosoma kwa ajili ya watu, mara zote utawakuta ndani ya jamii ya watu, wanakuwa na mazungumzo ya pamoja, wanaelekezana mambo yao mbali mbali. Lakini wale ambao wanasoma kwa ajili yao wenyewe tu, basi wale wanakua mbali na jamii na wale utawakuta katika sehemu za *VIP* tu.

Sasa wataalamu hawa ndio wanaotumiwa na malengo wanayopelekewa kwenye jamii hawaonekani, mnapelekewa watalamu lakini sio wazalendo. Kwa hivyo, tunaomba kila jimbo wapelekwe wataalamu walio wazalendo. Pia serikali ipanuwe wigo wa taaluma kwa wakulima, wakulima wote wahakikishiwe kupewa taaluma ya vilimo vya aina yoyote wanavyovilima.

Jengine Mhe. Spika, serikali itekeleze kwa dhati ununuzi wa matrekta. Sisi wawakilishi sote tulipokua tuko kwenye kampeni tulitumia ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwamba mtakapoiweka madarakani Serikali ya Chama cha Mapinduzi, basi kwa watu wa kilimo watafaidika kwa matrekta. Kwa hivyo, tunaomba sana hii serikali itekeleze ile ahadi tuliyoitoa kwa wananchi majimboni mote Zanzibar tuliitukia ilani ile. Sasa ilani ile isiwe ya ovyo. Tunaomba sana Mhe. Waziri anunuwe matrekta kuwapelekea wakulima wetu, wakulima wetu wameshachoka kulima kwa kutumia majembe ya mkono. Jamani kutokea mababu zetu mpaka leo bado tu, miaka 50 watu wanatumia majembe ya mkono mpaka leo jamani, watu wameshachoka tena.

Mhe. Waziri wazee wetu wameshachoka tena kulima kwa jembo la mkono, wameifanyia kazi serikali hii kwa muda mrefu. Sasa ni wakati wa wizara kujitutumua ikawasaidia wazee, angalau kuwapelekea matrekta na pia

kuwapelekea mbolea, kwa sababu ardhi ni hizo hizo zinazolimwa tokea miaka hiyo, kiasi karne zilizopita. Sijui karne 20 zilizopita ardhi ni hiyo hiyo wala haitiwi mbolea, mkulima wetu baada ya kulima kwa nguvu zake, wala sio nguvu hakuna mkulima mwenye nguvu, ni kwa juhudi zake tu. Baada ya kutumia juhudi zake pesa aliyoipata ananunulia mbegu, kila mkulima wa kule Pemba sijui huku Unguja, lakini kule baada ya juhudi akishalima mtu. Kwa mfano muhogo basi pesa atakazozipata ananunulia mbegu, sasa ni zipi atakazonunulia mbolea hazipo tena na ardhi ni hiyo hiyo.

Kwa hivyo, siku zote wanapanda na kisiki kama ujiti huu wa hii *microphone* ninayozungumzia ndio kinavyokua hakikui zaidi ya hapa. Hii ni kutokana na ardhi haina rutuba. Kisiki hiki kilichopandwa chenye kimo cha hiki kipazasauti ninachozungumzia, basi ndipo hapo hapo mwaka mzima kiko pale pale, kama kitatoa vidole viwili au vitatu, lakini hiki hakiwi tena kisiki cha kupanda tena baadae.

Kwa hivyo, tunaomba sana mbolea katika majimbo yote na hususan katika Jimbo la Wingwi, wananchi wangu mimi wa jimbo la Wingi kwa kuwa ile ardhi haikubali tena hulazimika kuondoka, kwa mfano Kijichame ninakokaa mimi, Sizini, Wingwi, Mjini Wingwi wote hao wanatoka …

Mhe. Spika: Naomba umalize Mheshimiwa dakika zako tano.

Mhe. Said Omar Said: Wote hao wanatoka kwa kwenda kulima jimbo la Gando, baada ya hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kuna tatizo kidogo la wakati kwa sababu kusudio langu ni kwamba Mhe. Waziri ilikuwa aje aanze kujibu hoja zenu kuanzia saa 7.00 lakini bado hajapata huo muda na tuna kama mawaziri wanne. Pia wanahitaji kuchangia, sasa mimi ningewaomba Waheshimiwa Mawaziri wale ambao nitawaita kwa ajili ya kutoa michango wajaribu kwa kadiri itakavyowezekana watumie muda mfupi sana kuchangia na waende kwenye mambo ya msingi tu, ili baadae tuje tuweze kupata muda wa kumpa Mheshimiwa Waziri mwenye hoja ili aweze kumalizia shughuli yake.

Kwa maana hiyo sasa nianze kumwita Mhe. Juma Ali Khatib ili atoe mchango wake.

Mhe. Juma Ali Khatibu: (Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum) Ahasante Mhe. Spika, mimi nachangia moja kwa moja, nimesikiliza michango mingi ya

Waheshimiwa Wawakilishi, michango yao ni mizuri lakini nataka kuwakumbusha kidogo tu kwamba haya yote yaliyotokezea ni sisi wenyewe wazee pamoja na wale vijana waliokwenda kusomeshwa na Serikali na baadae wakaikimbia nchi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepoteza pesa nyingi sana kwa ajili ya kuwasomesha vijana wetu kwenda kusomea utaalam wa kilimo, kwenda kusomea utaalam wa uvuvi, kwenda kusomea utaalam wa ufugaji na kadhalika.

Bahati mbaya hawa vijana wanapokuja hapa hawataki kuitumikia nchi yetu, hawataki kuwasaidia wavuvi wetu, wakulima wetu na wafugaji wetu, ndio maana sasa tukagundua kwamba kuna haya matatizo mengi Waheshimiwa Wawakilishi waliyoyazungumza hapa. Sasa mimi nilikuwa na fikra kama itawezekana sasa, kwa sababu ukiangalia Serikali inapoteza mabilioni ya mapesa kusomesha taaluma mbali mbali kwa Wizara mbali mbali. Sasa kuna haja ya kubadilisha sheria zetu kwamba yeyote anayekwenda kusoma nje kwa lengo la kutumikia nchi na taifa akiamua sasa kutoroka kuwe na mikataba ambayo kwa wazee na wale wahusika wasaini ile mikataba.

Mimi napenda kumpongeza katibu Mkuu wa Wizara hii, namkumbuka wakati anasoma Chuo Kikuu pale Dar es Salaam kwa kweli kaonesha uzalendo mkuba bwana Juma, mpaka leo yupo anaitumikia nchi. Kwa hivyo huu ni mfano wa kuigwa. Lakini leo kama tutamuuliza Waziri wa Wizara hii atupe majina je, ni wataalamu wangapi wamesomeshwa na Serikali… kwa hivyo nataka kuwaambia Waheshimiwa Wawakilishi kwamba Serikali ina nia nzuri, ina malengo mazuri, ina mipango mizuri na imejitolea na imetumia pesa nyingi sana kusomesha vijana wetu lakini tatizo vijana wetu ndio mwanzo wa matatizo haya. Wao badala ya kuja kuisaidia nchi wanakwenda kufanya kazi nchi nyengine au sehemu nyingine, sasa ifike wakati sheria hizi tuzibadilishe wale watakaopata fursa ya kwenda kusoma nje basi wawe tayari kwanza kuweka uzalendo mbele kutumikia nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi namkumbuka mtaalam mmoja sasa hivi anatengeneza mambo ya *nuclear* yuko Marekani anaitwa Mohammed Omar Ali yeye ni mtu wa Mjimbini; huyu jamaa ni mtaalam mkubwa sana lakini wakati wa marehemu Karume Rais wa kwanza wa nchi hii hawa vijana walikwenda wakasomeshwa wakarudi hapa, lakini kwa uzalendo kuna wengine walitaka kuchukuliwa Nairobi na kadhalika lakini wale wakaonesha mapenzi ya taifa lao wakaja kufanya kazi hapa mpaka baada ya muda wakastaafu ndio wakaenda Marekani kufanya kazi.

Kwa hivyo ukiangalia sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sasa hivi wana watu wengi sana waliowasomesha kwa nia njema tu, lakini sisi watoto wetu au vijana wetu hawana uzalendo. Kwa hivyo tumegundua kwamba tatizo si serikali, tatizo si Waziri lakini tatizo liko kwetu sisi. Kwa hivyo mimi ninachoomba kwamba tubadilike kuanzia sisi wazee tuseme na watoto wetu na hata wale watoto wanaopata fursa waweke uzalendo mbele. Ahsante sana Mhe. Spika sina mengi kwa sababu ya muda. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naunga mkono hoja na nataka niwaambie Wawakilishi tuipitishe bajeti hii kwa kuunga mkono hoja hasa ukizingatia Waziri ni mpya, Naibu Waziri ni mpya halafu isitoshe Waziri kwa muda mfupi ameonesha mafanikio makubwa katika Wizara hii yeye na watendaji wake. Kwa hivyo tushirikiane tuipigie kura kwa asilimia mia moja. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Said Soud Said (Waziri asiye Wizara Maalum): Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na pia nachukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wa nchi yetu Mhe.Dkt. Ali Mohammed Shein na Mhe. Seif Ali Iddi kwa kusimamia vyema muongozo mzima wa Serikali yetu. Nina imani kabisa kwamba chini ya uongozi wao tutafika pahala pazuri.

Mhe. Spika, bajeti hii ya kilimo hatuna budi sote kwa pamoja tuiunge mkono na kwa maana hiyo naunga mkono hoja kwa sababu bajeti hii inaonekana wazi ina nia, dhamira na kusudio la kufufua kilimo katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kwa sababu gani nasema hivyo, kwa sababu tu Mhe. Waziri ameonesha moyo wa huruma na upendeleo mkubwa kwa Wazanzibari kwa kujitolea yeye mwenyewe kwa hali na mali kufuatilia kila penye tatizo. Ni kweli kabisa kwamba sisi kama Wazanzibari tumeweza kuipoteza rasilimali yetu ya visiwa hivi na hatimae sasa tunalia sana na ajira.

Ni ukweli kabisa kwamba kilimo cha minazi na mikarafuu kimepotea sana katika Visiwa vya Unguja na Pemba. Kilimo cha minazi kinatoa ajira kwa Wazanzibari walio wengi ukiangalia mnazi unatoa ajira kwa muangushaji, muokotaji, mfuaji, mbanjaji, mchomaji, msekuaji na hata mwisho inapelekea yule ambae anakwenda kukamua mafuta ya nazi basi pia nae anapata ajira, lakini mambo yote hayo yamekosekana baada ya kuwa sasa mnazi wenyewe tumeamua kuukata, hatimae sasa tumefika pahala tunanunua nazi kutoka nchi za nje. Sasa kimsingi Wazanzibari wote kwa pamoja tusimame kufufua kilimo cha nchi yetu ili tufikie pahala pa kuonesha uzalendo na muongozo mzima wa Serikali, ili kufikia pahala yale yote yaliyotegemewa kufanywa na Serikali yapatikane.

Mhe. Spika, kilimo kilichozoeleka katika visiwa vyetu ni kilimo cha mkono na sasa hatuna budi tubadilike, kwa vile natoa wito kama Serikali kubadilisha kilimo na tutokane na kilimo cha asili moja kwa moja turukie na kilimo cha biashara, vilimo vya asili vya kujikimu tumeshazoea kuwa navyo ni vilimo vya kawaida, lakini sasa kulingana na hali ya maisha tunalazimika kwenda kwenye vilimo vya biashara. Ndugu wananchi pamoja na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi mnaonisikiliza, kimsingi kilimo cha biashara tukiweza kupanda michikichi, milangi langi, mi-sun flower, mikarafuu kwa wingi, minazi kwa wingi, vanila kwa wingi, midalasini kwa wingi, tukipanda mishokishoki kwa wingi, nchi hii itafika pahala biashara ya kilimo itanawiri sana na hivyo ni vilimo vya biashara.

Mhe. Spika, wenzetu Comoro wanazalisha mafuta ya *perfume* kwa milangi langi wanauza dunia nzima, wenzetu Kigoma wanazalisha michikichi mifupi kabisa wanatengeneza mafuta ya mawese, wanauza Tanzania nzima, sasa sisi Wazanzibari tumefika pahala tunakaa kitako tu tunasubiri Serikali iwapelekee watu chakula majumbani, tuachane na hiyo hoja. Huu ni wakati wa kufika pahala tukabadilika na tukaungana kwa pamoja kukifanya kilimo cha Zanzibar kuwa ni mkombozi wa maisha yetu. Kwa sababu Serikali ishakuwa tayari kusaidia kila pahala ili wananchi waondokane na ziki hiyo, basi ni vizuri Wawakilishi tukatoka humu na agizo la kwenda kushajiisha kilimo majimboni mwetu, kazi hii si ya Serikali peke yake; wawakilishi ni sehemu ya Serikali kwa hivyo ni vizuri wawakilishi mkatoka hapa kwenda kusimamia magurupu ya vijana kuwatoa katika dhana ya kisiasa, na kuwapeleka katika dhana ya kilimo.

Tumeshuhudia sasa hivi kilimo cha mboga mboga kimeshaweza kuokoa pesa za Wazanzibari nyingi sana, tulikuwa tunaagiza matikiti, tunaagiza figili, karoti, pilipili boga, nyanya kutoka bara lakini sasa hivi baada ya mshajihisho mkubwa ambao wenyewe Wazanzibari wamejitokeza, sasa vilimo hivi vinaweza kubana pesa hizi kwenda bara na tulikuwa tunapoteza zaidi ya bilioni mbili kwa mwaka kuzipeleka bara kwa kilimo kama hiki. Kwa hivyo sisi kama salamu ya serikali ni wajibu wetu kutoka na sio kusubiri Serikali, sisi wenyewe ndio Serikali tutoke na msimamo wa kwenda kushajihisha kilimo ili Wizara hii sasa tuweze kuangalia itasimama kutafuta wataalam. Tunasema sote kwamba Wizara hii ina wataalam wengi lakini bila ya sisi wenyewe kuwataka wataalam wafanye kazi, hawafanyi kazi.

Mhe. Spika, na kwa sababu tu kuna mambo mawili yaliwakwaza wataalam kushindwa kufanya kazi; la kwanza walikuwa wanasubiri Serikali waje waifanyie kazi sasa tunawaambia wataalam Serikali ndio hii ya kuifanyia kazi

wanaweza kufanya kazi wafanye kazi, hawawezi kufanya kazi waache kazi, hii ndio Serikali yetu na hii ipo kwa ajili ya Wazanzibari wote.

Suala la pili ambalo lilikuwa linakwaza ni kwamba watu walikuwa wanafikiria tu kwamba labda kuna uwezekano wa kwamba kila mtu anaweza akajiamulia kulima vile anavyotaka yeye; kilimo lazima kuwe na wataalam, ardhi inahitaji kuendeshwa kitaalam. Nimesikia wawakilishi wengi wakinung'unika kwamba mipunga inaungua wakitia mbolea, wakitia mbolea inakufa hii yote ni kutokana na kwamba wataalam hawateremki mabondeni. Sasa basi ni wajibu wetu kama Serikali kuhakikisha sote wawakilishi, Madiwani kuteremka mabondeni kuwasaidia wananchi, tukiwasimamia na mabwana shamba na mabibi shamba kufanya kazi ya wananchi, aliyekuwa hataki tupeni taarifa kama Serikali. Hilo tutalihisabu ni jipu na hatuwezi kubakisha majipu sisi kazi yetu tutapasua majipu.

Mhe. Waziri nakwambia usimuonee huruma mtu, Zanzibar inahitaji kukombolewa na kilimo na ardhi iliyopo kama itatumika vizuri tunaweza kuagiza chakula kidogo sana kwa ajili ya nchi yetu lakini chakula kingi sana kikazaliwa ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia na wawakilishi wote naomba tuunge mkono hoja ili Mhe. Waziri tumpe kazi akafanye kazi kwa ajili ya nchi yetu. Ahsante sana (Makofi)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia bajeti ya Wizara ya Kilimo. Najua muda mfupi na mimi nitajaribu kukatisha yale ambayo nilikuwa nataka niyaseme nitasema kwa ufupi kabisa.

Mhe. Spika, tukiangalia takwimu za Zanzibar utaona kwamba mchango wa sekta ya kilimo umepungua katika pato la taifa, kwa sababu uchumi wa Zanzibar tunakwenda katika wakati wa kimaendeleo. Sasa hivi mchango wa huduma na biashara umekuwa mkubwa ukilinganisha na mchango wa kilimo katika pato zima la taifa la Zanzibar katika anga hizi za uchumi. Kwa misingi hiyo tunaona kwamba kuna mabadiliko kidogo katika suala zima la kilimo na sekta nyengine katika uchumi.

Mhe. Spika, kwa kweli umefika wakati sasa hivi kama Taifa letu la Zanzibar tuzingatie hasa kilimo chetu tunakitaka cha aina gani, kwa sababu lazima tufike wakati tuamue kushajiisha kilimo cha biashara au tunashajiisha kilimo cha chakula hatuwezi kwenda kama hivi tunavyokwenda. Kwa sababu sasa hivi

tunataka mambo yote tuyafanye, hatuwezi kufanya mambo yote kwa ajili ya kukuza maendeleo yetu.

Mhe. Spika, lilizungumzwa suala zima la viwanda katika sekta ya kilimo ndio maana nchi nyingi hata wenzetu Tanzania bara wanazungumzia mapinduzi ya viwanda, na sisi Zanzibar tulipozungumzia mapinduzi ya viwanda macho yetu yote pale Wizara ya Biashara tunaangalia sekta ya kilimo kwa kiasi gani sekta ya kilimo itachangia katika sera nzima ya mapinduzi ya viwanda. Mhe. Spika, tukiangalia viwanda tuna viwanda 2050 lakini viwanda hivi asilimia 90% viwanda vidogo vidogo tunataka kuvibadilisha viwanda vidogo vidogo viwe viwanda vikubwa ambavyo vitakuwa vinachangia katika maendeleo ya uchumi wetu. Kwa ufupi tunao uwezo wa kuibadilisha Zanzibar kwa kutumia sekta ya kilimo, lakini kuna mambo ya msingi lazima tuyazingatie.

Mhe. Spika, nasema naunga mkono bajeti hii mia juu ya mia na ningewaomba ndugu zangu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu na wao wakaunga mkono bajeti hii, kwa sababu sio kwamba Serikali inafanya kwa makusudi haya yaliyozungumzwa wengine kwa jazba na kauli ya kukata tamaa, serikali haifanyi kwa makusudi lakini lazima mkubali kwamba uchumi wa Zanzibar bado uko chini. Kwa hivyo yale yote ambayo tunataka tuyafanye hatuwezi kuyafanya kwa sababu uchumi wa Zanzibar uko chini na tunatakiwa tuingize mtaji mkubwa sana katika mambo haya ambayo tunayataka kuyazungumza.

Mhe. Spika, mimi ningesema kitu kimoja tunazungumzia masuala ya *Economic scale* kwa sababu tuseme kwamba uchumi wetu uwe unazalisha kwa hatua kubwa, kwa mfano tunazungumzia viwanda vya kilimo tuchukulie kiwanda sasa hivi cha kufanya *spice* kama hatuwezi kuzalisha viungo vya kutosheleza soko, hatuwezi kuzalisha, hatuwezi kuwa na viwanda vya aina hiyo. Masoko yapo nimerudi juzi Dubai wanasema masoko ya vitu vyenu vya viungo yapo ya kutosha kuanzia *super markert* mpaka majumbani mpaka viwandani, lakini tujiulize kuna Mheshimiwa mmoja aliuliza hapa viungo viko wapi. Huko nyuma Zanzibar tulikuwatukisifiwa kwa kulima mazao kama haya tukiuza nje pilipili hoho, pilipili manga, karafuu na vyengine vyengine lakini uzalishaji wetu ni mdogo.

Kwa hivyo ninachosema ni kwamba lazima tukae kitako sisi sote tusiseme Serikali peke yake, wenyewe tukae tuzungumze tunataka kilimo cha aina gani; cha biashara au kilimo cha chakula. Bila ya kuamua hivyo tutakuwa tunafanya kazi ambayo tunajidanganya. Natoa mfano mmoja, kuna mtu alisema tunataka Zanzibar kuuza ndizi lakini nini maana yake kwamba tuwe na bishara ya kuuza ndizi nje, kwa wale waliokwenda nje wakaona mashamba ya ndizi sijui kama

wapo ambao walikwenda kuona; mashamba ya ndizi yanachukua sehemu kubwa unaweza kusema mfano kama Kaskazini nzima ni shamba moja tu la ndizi. Tunaanza kuchukua ndizi kuvuna, kusafisha, kutia kwenye kiwanda, kutia *stamp*. Tunaweza kufanya hivyo hatuwezi Mhe. Spika, lazima tuamue kwa makusudi kwamba nchi yetu itakwenda katika kilimo cha biashara na kilimo cha kuweza kupata mazao ya kuweza kuuza nje, kama hatujaamua hivyo hatuwezi kufikia huko.

Mimi binafsi katika sera yetu ya mkakati wa mapinduzi ya viwanda tutakwama hapa kwa sababu hatujaweza kuzalisha vitu vingi, kwa mfano mwengine Mheshimiwa tunazungumzia *Branding* tumesema kwamba karafuu ya Zanzibar itatiwa katika *Branding* yaani itakuwa na hatimiliki yake, suala linakuja karafuu ya Zanzibar ni nzuri ya hali ya juu haijafanyiwa utafiti. Kwa hivyo hatua tuliyokuwa nayo sasa hivi ni kuomba kampuni moja India kutufanyia utafiti wa kuweza kusema kwamba Karafuu ya Zanzibar ni ya aina hii ambayo mtu mwengine yeyote hawezi kudanganya akasema nauza karafuu ya Zanzibar.

Jengine Mhe. Spika tunaposema karafuu ya Zanzibar hatutaki tutoe *branding* ya kitu kimoja lazima iunganishe na vitu vyengine, imetiwa pilipili hoho, imetiwa pilipili manga na mazao mengine kama mdalasini. Mhe. Spika, mazao haya hakuna ya kutosha kwa hivyo hata tukifanya *branding* kampuni itakayotuuzia vitu hivi ipo kwa sababu zitakuwa nzuri za kuvutia, hakuna mazao ya kutosha. Kwa hivyo ndugu zangu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mueleze wananchi wetu huko waliko kwamba tunatakiwa sasa hivi kulima kwa bidii zaidi na kuongeza mapato yetu zaidi, kwa sababu kama mtu unalima hekta mbili au hekta moja aongeza alime hekta tano, sita, sasa lakini hapo pana tatizo, kwanza changamoto zilizopo.

Kama nilivyosema kunatakiwa kuwe na utaalam maalum wa mazao haya, utaalam mmesema upo lakini hautoshelezi sasa tuwe na utaalam wa kutosha. Kubwa jengine tuwe na mitaji ya kutosha kwa sababu mazao kama haya yanatakiwa mtaji wa kutosha ili watu waweze kulima. Kama unafanya *irrigation* unatakiwa uwe na fedha, unatakiwa uwe na mbegu zilizokuwa nzuri, unatakiwa na utaalam.

Kwa hivyo mitaji kwa shughuli hii nayo ni muhimu tusikae tukalaumu serikali, mitaji hii inakuwa labda watu binafsi au inakuja kwa serikali. Bado suala zima la kushirikisha watu binafsi katika sekta ya kilimo nayo vile vile haijafikia mahali pazuri nalo hilo vile vile linatukwamisha.

Mhe. Spika, vile vile niseme kunatakiwa tutizame mbinu mpya, mikakati mipya ya kilimo kama hiyo moja niliyosema mfano wa *branding* lakini pia nyengine ni masuala ya kutumia *packaging*. Mhe. Spika, kuna bidhaa sasa hivi za kilimo zinakaushwa kwa jua, hizo nazo zikikaushwa kwa jua zinauzwa vile vile zinapakiwa vizuri vinauzwa ndani na nje ya nchi. Hatuna utaalamu huo hatujafikia hivyo hatuna kilimo, mazao hayo ya kutosha hatunayo, lakini vile vile kuna mazao mengine yanakaangwa. Ndizi zinakaangwa zinafanyiwa *packaging* zinauzwa, lakini utaalamu hatujakuwa nao lakini vile vile mtaji wa kufanya mambo kama hayo hatuna.

Jengine la mwisho Mhe. Spika, katika mkakati mpya kuna kitu kinachoitwa *organic products* yaani mazao ambayo yanazalishwa bila kutumia mbolea wala kitu chengine. Hayo nayo yapo kuna masomo fulani fulani kidogo ambayo wanafanya mambo kama hayo lakini sio mengi. Kwa hivyo Mhe. Spika, nakusudia kusema kwamba kama serikali tunayo kazi kubwa ya kufanya lakini serikali haiwezikufanya peke yake bila ya kushirikiana na wenzetu wawakilishi lakini pia na watu waliomo katika sekta binafsi. Uwezo huo tunao, utaalamu wa kufanya kazi kama hizo tunao, tafiti nyingi zimefanywa, masuala yende mimi mwenyewe nimeona embe zinazotengenezwa zikawekwa zile nyengine zikafanywa kama peremende, nyengine zikafanywa kama achari, kuna embe za kufanya *juice* zote zinawezekana na utafiti huo ushafanywa wa kutosha. Tatizo kubwa la Zanzibar ni kutoka kunako utafiti na kuvipeleka sasa kuanza kuvizalisha, kwa ajili ya viwanda ili viweze kuuza nje na ndani.

Kwa hivyo Mheshimiwa changamoto tuliokuwa nayo na hii kama nilivyosema naiunga mkono bajeti ya wizara hii, changamoto waliokuwa nayo kwamba kunahitajiwa tuwe mazungumzo maalum ya kusema kilimo chetu tunataka kiwe vipi na tutaweza kufaidika vipi na nani hao ambao watakuwa ni wabia katika sekta hii ya kilimo hasa katika utaratibu mzima wa viwanda katika sekta hii ya kilimo. Kama hatujafanya hivyo Mhe. Spika, tutakuwa tunalaumiana, tutakuwa tunaishtumu serikali na vile vile kubwa itakuwa wajibu wetu sisi kama wananchi wa Zanzibar hatujaufanya.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili: Mhe. Spika, nami ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini pia nitajitahidi sana kuuheshimu wakati wako kwa sababu mengi yameshazungmzwa, kwa hivyo nitafupisha maelezo yangu. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuimarisha kilimo nchini.

Mhe. Spika, katika kipindi kifupi tumeona jitihada kubwa anayoifanya Mhe. Waziri katika kuisimamia wizara hii na naamini ataweza kuleta mabadiliko makubwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu. Aidha, niwashukuru sana mawaziri wenzangu walionitangulia kwa kuelezea kuunga mkono bajeti hii nami niungane nao kwa kuiunga mkono bajeti hii asilimia mia moja. Na niwaombe wajumbe wenzangu waiunge bajeti hii mkono kutokana na umuhimu wake wa wizara hii.

Mhe. Spika, niwapongeze sana Waheshimiwa Wawakilishi waliochangia katika sekta hii kweli michango yao ilikuwa ya upeo mkubwa, yenye muono mkubwa sana wa maendeleo ya kilimo na ukweli wameeleza changamoto zilizo mbele yetu. Kwa ufupi dhamira yao na dhamira ya serikali ni moja, sote wawili tunazungumzia lugha moja ya maendeleo ya kilimo. Tunafanya hivyo kwa sababu asilimia 70 ya wananchi wetu wanategemea kilimo. Kwa hivyo ni wajibu wetu kama viongozi kuhakikisha mabadiliko makubwa yanatokea katika sekta hii ya kilimo.

Ni kweli tunazo changamoto za msingi na moja kubwa Mhe. Spika, ni ardhi, ardhi ndogo na idadi kubwa ya wananchi tunaongezeka kwa wingi na ardhi inabaki hapa hapa na ardhi ndio kilimo chenyewe.

Changamoto nyengine kubwa Mhe. Spika, maji. Maji yanaendelea kupungua, ili kilimo kinawiri na kiendelee kunahitajika maji. Changamoto nyengine hizi za utaalam na miundombinu zinaweza kwa njia moja au nyengine kupata majibu kadiri ya tunavyojitahidi. Lakini hizi kubwa mbili ndio changamoto za msingi. Na ukitizama Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wote walikuwa wanazungumzia suala hili la ardhi kwa upana katika maelezo yao ya kuimarisha kilimo. Na mimi niungane nao hapa ndio *challenge* yetu iliyopo kwamba ardhi ndogo idadi yetu inaongezeka na asilimia 70 ya watu wetu wanategemea kilimo. Sasa wajibu wetu kubuni mbinu bora, mikakati mizuri itakayotuondoa hapa ili kilimo chetu kiwe kilimo chenye kuleta tija na faida kubwa kwa wakulima wetu, watu waone hamu ya kilimo.

Kwa hivyo ni *challenge* yetu sote sisi tuliomo ndani na wananchi. Lakini moja ambalo lazima sote tulielewe yale mambo yamsingi tunayoambizana katika kuihifadhi hiyo ardhi ibakie na itumike kwa kilimo.

Moja ni lile suala zima la ujenzi holela; tunapojenga ovyo ovyo hususan katika njia za maji na mabondeni tayari umeshazidi kupunguza ardhi hiyo ya kilimo, kwa hivyo tayari utaona sisi wenyewe tunaongeza tatizo katika tatizo. Tunapoharibu vianzio vya maji na unahitaji maji kwa ajili ya umwagiliaji

tunaongeza tatizo juu ya tatizo. Kwa hivyo yapo mambo ya msingi, ni wajibu wetu sote wananchi na serikali kuyasimamia ili yatoe nafasi ya kuongeza nguvu ya kilimo.

Kwa hivyo wakati umefika *mind set* zetu sote kwa pamoja tuone umuhimu wa kilimo, tuone kwamba wakati umefika hatuwezi tena kwenda na kilimo cha wakati ule kwa kutumia eneo kubwa la ardhi kwa kuzalisha kidogo. Lazima tufikirie kama alivyosema Waziri wa Biashara nanma gani tutaitumia ardhi ndogo kwa kuzalisha vizuri. Kwa hivyo ni aina gani ya kilimo tutaamua tukishike twende nacho kwa ajili ya maslahi yetu ni *challenge* nzuri ambayo Mhe. Waziri wa Biashara ameiweka lakini hicho ambacho tumeamua kukilima lazima tukilime kwa utaalam mzuri, kwa njia bora ili uzalishaji wake uwe mkubwa.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wawakilishi wengi walizungumzia suala la kwamba viwanda vyetu *base* yake iwe ni bidhaa za kilimo na kweli muelekeo wetu ni *agro processing*. Kama alivyosema Waziri wa Biashara, muelekeo ni kwenda huko lakini upo umuhimu ikiwa tumeamua kwenda huko basi kile ambacho tunacho tuendelee kukidhibiti na kukikuza. Kwa mfano moja katika *agro processing* ni Kiwanda cha Sukari Mahonda kinazalisha sukari, kinalima miwa, wenzetu wamekuja wamewekeza wameleta utaalamu, tumeona sura ya kunawirika. Lakini wanapotokea watu wakenda kuchoma moto miwa tunajirudisha nyuma. Sasa tunataka kwenda kwenye *agro processing* lakini sisi wananchi wenyewe tuna-*discourage* hizo jitihada.

Kwa hivyo lazima *mind set* zetu zibadilike panapokuwa na *challenge* kama kuna jambo lolote wananchi pale wanapoona ipo athari kwao kwa ajili ya kilimo kile cha miwa ni vizuri basi wananchi, serikali muekezaji wakae pamoja kutatua tatizo hilo. Lakini umuhimu kuwa na kiwanda kile ni kitu kizuri sana, tutapata sukari, tunapata ajira na ule muelekeo wa sera yetu kwamba *base* yetu ya viwanda itokane na bidhaa ya kilimo tutaanza mfano mzuri. Kwa hivyo kile ambacho tunacho lazima *mind set* yetu ielekee kwenye kukilenga, ikiwa sisi wenyewe tunaharibu mwengine hawezi kuja akaunga mkono jitihada hizo.

Jambo jengine tuna kiwanda kizuri sana cha maziwa amekianzisha ndugu yetu Sheikh Said Bakhressa, ni kiwanda cha mfano sio tu kwa hapa Zanzibar lakini katika Afrika Mashariki nzima. Kiwanda kizuri kina muelekeo mzuri na kingesaidia sana kwa wakulima wetu hususan wafugaji kwa ajili ya kuuza maziwa, lakini kadiri inavyoelekezwa kutaalamishwa na kadhalika wananchi wetu hawawi wapokeaji vizuri wa kuunga mkono jitihada zile. Matokeo yake sasa kiwanda kile inabidi kiagize maziwa ya unga kutoka nje tu-*process* hapa

tuanze kuuza maziwa kwa utaratibu mwengine, wakati kingetumika kile kwa kuuza maziwa zaidi.

Sasa haya mambo ambayo yanajitokeza tayari ni *comparative advantage* zetu, tuzihifadhi, tuzione tushirikiane ili tuhakikishe tunakwenda mbele. Kwa hivyo mimi nakubaliana na waheshimiwa wote waliokuja na mtazamo huu wa *agro processing* na ndio dhamira ya serikali na ukweli ukitiza *base* yetu ya viwanda hamna njia nyengine zaidi ya kutegemea bidhaa za kilimo. Tukizungumza kilimo ni pamoja na uvuvi, mifugo na kilimo chenyewe, kwa hivyo hata wale waliozungumzia sana kuhusu kiwanda cha kusarifu au kusindika samaki nawaunga mkono sana, lakini ikiwa tunaona kiwanda cha miwa hiki kipo watu wanachoma miwa usitegemee *investor* mwengine atakuja kuekeza kwenye samaki. Lazima tutazame ule muelekeo wa kuvutia uekezaji na tuzungumze lugha moja.

Jengine, suala hili limezungumzwa na ndugu yangu sana Nadir, misitu yetu hii tuitumie kiutalii na ndio dhamira ya serikali kwamba *eco-tourism* kwa kiasi kikubwa inaendana na hiyo sifa uliyoitaja kwamba misitu yetu hii itumike kuwa ni sehemu ya vivutio vya utalii. Tumeanza kule Jozani, Ngezi na kadhalika. Dhamira ni hiyo, kwa hivyo msingi wake ni kuipokea vizuri tukafanya kazi kwa pamoja ili tulete manufaa zaidi.

Mimi nadhani wakati wa kulaumiana uwe umepita, sasa kama alivyosema mwenzangu ni wakati wa kufanya kazi kwa kisayansi zaidi ili tija ipatikane. Maana wenzetu hawa wachina na wengine, wao *population* yao inaongezeka ardhi yao ni ile ile, lakini mapato yao yamekuwa makubwa sana. Kubwa litakalotumika ni *new technology* pale. Ni sayansi inafanya kazi matokeo yamekuwa makubwa. Kwa hivyo na sisi sasa tuache hizi hadithi nyengine tuelekee katika kujenga misingi ya kuimarisha sayansi, kwa maana ya kuwa na *modern technology* zitakazosaidia katika maeneo madogo ya ardhi yakazalisha zaidi na tukapata tija kubwa.

Waheshimiwa walitaka serikali itoe kauli kuhusu ukataji wa vipando hivi vya wakulima wetu, mihogo, mikarafuu na kadhalika. Ukweli asubuhi ya leo tulipokuwa tukijibu swali hapa, serikali ilieleza kusikitishwa kwake na vitendo hivi vya aibu sana. Kama nilivyosema asubuhi unapomkatia mtu kipando chake cha kupatia rizki humkeri yule mtu tu lakini unamkera mpaka Mungu. Unavunja sheria za nchi, kwa hivyo unagombana na serikali, unagombana na jirani yako, unagombana na Mungu rada yake kubwa. Ndio nikasema mtu huyo anaechukua tabu atoke akate miti halafu aiache hapo hapo arudi nyumbani kwake akalale bila ya faida yoyote huo ni ujinga, ushamba. *(Makofi).*

Sasa watu kama hawa hawakusidii kushirikiana kuleta maendeleo ya nchi yetu, sisi tunaendelea kuviagiza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vianze kazi ya ziada kuwashughulikia watu hawa na kuwapeleka katika vyombo vya sheria, ili sheria ichukue mkono wake. Mwendo huu kwa njia moja ama nyengine unauhatarifa usalama wa nchi yetu na tunajua kabisa kwamba watu hawa wanapenda kuifanya nchi yetu isitawalike na wanapenda saa zote tuzungumze habari zao, ili tuwache mambo yetu ya msingi ya maendeleo ya watu wetu. Kwa hivyo wananchi lazima wafahamu kwamba viongozi hawa wanaowatoa katika mstari ndio wanaodogosha maendeleo yetu na ndio wanaosababisha kuimarisha umaskini wakati sisi tunapambana nao kuuondoa. Kwa hivyo hao hawawezi kuwa viongozi wema wa kuungana nao, dawa yao ni kuwaacha mkono na kuunga mkono wenye nia njema na si wengine ni Chama cha Mapinduzi na ilani yake tunayoitekeleza.(*Makofi*)

Kwa hivyo Waheshimiwa Wawakilishi tuliacheni hili jambo ndani ya serikali lizidi kuendelea kulitafakari zaidi ili kila aliyefanya kosa aonje mkondo wa sheria na adabu apate sawa sawa ili maisha yake asithubutu tena kufanya vitendo hivyo. Katika kuyashughulikia hayo hatoshughulikiwa yule tu aliyekwenda kuvikata vipando lakini tunataka tujuwe na aliyetoa amri nani ya kwenda kukata vipande. (*Makofi*)

Ni jambo la kusikitisha sana, la kuhuzunisha katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhan anaenda kuvikata vipando vya mwenzake halafu unafunga, funga hiyo iko wapi, huna funga wewe. Huwezi kwenda kung'oa muhogo kwa makusudi wa mtu ambaye ndio anategemea kwa maisha yake ukasema umefunga. Unakata mikarafuu ya mwenzako ambae anaitegemea ndio inayomuendeshea maisha yake, ukasema unafunga hapo funga huna na uislamu wako una *question mark.* Kwa hivyo wananchi nawaomba sana tuache tabia hii ambayo haitupeleki popote nchi yetu, tunahitaji tujenge umoja, mshikamano na tuhakikishe nchi yetu inakuwa na amani na utulivu. Ili tufanikiwe nchi lazima iwe katika amani na utulivu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii tushirikiane. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili,Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia na kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuhusu hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi ya bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017. Waheshimiwa Wajumbe nitaomba radhi kutokana na sauti yangu. Mhe. Spika,

napenda kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa uwasilishaji wake wa bajeti pamoja na watendaji wake wote, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu kwa kuandaa kitabu hiki kizuri.Vile vile napendavkuwapongeza waheshimiwa wa Baraza lako Tukufu kwa kuichangia vizuri hotuba ya Wizara ya Kilimo, Maliasili na napenda niwahakikishie kuwa michango yao, maelekezo na ushauri wao waliotupa tumeupokea na tutaufanyia kazi kadri ya uwezo utavyoruhusu kwa lengo la kuleta mafanikio wizara na wananchi wote kwa ujumla.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi (Mhe. Yussuf Hassan Iddi) pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa michango yao na maelekezo katika utayarishaji wa bajeti hii.Tunaahidi kwamba wizara itayafanyia kazi maelekezo na ushauri walioutoa.

Mhe. Spika, napenda kulieleza Baraza lako tukufu kwamba ni kweli kuwa mchango wa sekta ya kilimo umepungua kutoka asilimia 27.9 mwaka 2014 kufikia asilimia 19.2 mwaka 2015. Hali hii inaonesha kuwa ni muelekeo mzuri kwa nchi yetu katika mipango yetu inayoelekea katika uchumi unaotegemea huduma na viwanda. Hata hivyo, wizara imeelekeza nguvu zake zaidi na mikakati yake katika kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo ambapo imekua kutoka asilimia -0.4 mwaka 2014 kufikia asilimia 2.7 mwaka 2015.

Mhe. Spika, napenda pia kulieleza Baraza lako tukufu kuwa ushauri uliotolewa wa kuitaka wizara kuangalia upya vyanzo vya mapato na kuziba mianya ya upotevu, wizara imeupokea ushauri huo na inaahidi kuendelea kuchukua hatua madhubuti ili kuhakikisha mapato yote yanakusanywa na kuwasilishwa serikalini. Mikakati na hatua zinaonesha kwamba kuna mafanikio kwa iliyokuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kuongezeka kwa mapato kwa miaka mitano mfululizo 2010-2015. Hata hivyo, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imefanya mapitio na kuandaa kanuni mpya za bei za mazao ambazo zimeshaanza kutumika. Kwa sasa wizara pia inaendelea na kuandaa kanuni za mifugo, maliasili na uvuvi na kusimamia vyema tonzo za uchimbaji na usafirishaji wa maliasili zisizorejesheka jambo ambalo litafanikisha utekelezaji wa mikakati tuliyoiweka.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kujua idadi ya miche ya mikarafuu inayotolewa kwa wakulima, mingapi iliyomea na mingapi iliyokufa. Wizara inafuatilia kwa kina suala hili ambapo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ufuatiliaji unaonesha kuwa wastani wa asilimia 54.8 ya miche yote iliyopandwa na kumea. Ufuatiliaji huo umebaini kuwa miche ya mikarafuu iliyoota inaendana na

juhudi za wakulima. Kwa mfano, mkulima Sultan Hemed wa Junguni Mzabibu, Pemba na Mohammed Issa wa Chonga, Pemba miche yao imeota kwa zaidi ya asilimia 85.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili Mifugo na Uvuvi inaendelea na utaratibu wa kuhifadhi maeneo ya misitu yaliyopo na kuongeza maeneo mengine. Aidha, napenda kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba katika mwaka 2016 Wizara kwa kushirikiana na *UNESCO* imefanikisha Hifadhi ya Taifa ya Jozani na Ghuba ya Chwaka katika mtandao wa Kimataifa wa "HIFADHI HAI" (*MAN AND BIOSPHERE RESERVE*). Hatua hii ni kubwa sana na itasaidia kuendeleza utalii wa kimazingira na tafiti za kimataifa kupitia *UNESCO*. Pia, juhudi hizi tumeanza kuzichukua kwa Msitu wa Ngezi, Pemba.

Mhe. Spika, katika kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu, wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza tafiti ya ukusanyaji wa takwimu katika ngazi ya Wilaya (*Small Area Estimate*) ambapo Benki ya Dunia tayari imeshatoa mafunzo kwa wakusanyaji wa takwimu hizo. Vile vile, wizara kwa kushirikiana na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Zanzibar na Taasisi ya Takwimu ya Taifa zinaendelea na utafiti wa ukusanyaji wa takwimu za kilimo. Aidha, kwa kuimarisha takwimu zetu wizara imeimarisha ukusanyaji wa takwimu kwa kutumia madodoso maalum na inaendelea na zoezi la matumizi ya mizani kwa ajili ya upimaji wa mazao hayo.

Mhe. Spika, napenda kulieleza Baraza lako tukufu kuwa wizara imeupokea ushauri kushirikiana na *ZSTC* kushughulikia zao la mwani. Aidha, kuhusu bei ya mwani tayari vikao na wadau vimefanyika pamoja na wakulima wa mwani, makampuni ya mwani na Wizara ya Biashara. Suala hili limewasilishwa Baraza la Mapinduzi na imeundwa kamati maalum ya Baraza la Mapinduzi chini ya uongozi wa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Hivyo, suala la mwani linashughulikiwa katika ngazi ya juu ya serikali.

Mhe. Spika, wizara imeupokea ushauri wa kamati juu ya kufuatilia vikundi 144 vya ufugaji wa mazao ya baharini ili kuongeza uzalishaji. Aidha, wizara imeunda kitengo cha ufuatiliaji na tathmini ili kufuatilia maendeleo ya miradi katika wizara. Hivyo, vikundi hivyo vitafuatiliwa pamoja na kupatiwa ushauri na mafunzo ili kuboresha uzalishaji na ubora wa mazao yanayozalishwa.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kuimarisha doria kwa kushirikiana na KMKM, ushauri tumeupokea na wizara itachukua juhudi za kuimarisha na kuendeleza doria na KMKM ili kuhifadhi rasilimali za bahari na maeneo yetu ya hifadhi na kukomesha uvuvi haramu.

Mhe. Spika, napenda kulieleza Baraza lako tukufu kuwa serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inapenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi, kuwa wizara ina mkakati wa kuwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji katika gharama ndogo ili nao waweze kuuza bidhaa zao kwa bei nafuu. Aidha, wizara ina mipango ya kufuatilia bei za bidhaa za kilimo pamoja na kuanzisha utaratibu wa kuuza bidhaa za kilimo pamoja na kutumia mizani ili kuhakikisha kuwa wakulima na wachuuzi wanapata usawa wa bei na mlaji analipa bei iliyo sahihi.

Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa wizara inakubaliana na ushauri wake kuhusu kuendelea na utafiti wa muhogo, *fertilizer programme* na utafiti wa mpunga. Hata hivyo, tunapenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi, kuwa serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imeendelea kuimarisha sekta ya utafiti kwa kukipandisha daraja kituo cha utafiti hadi kuwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar.Kujenga maabara mpya za utafiti wa mazao na udongo na kuwafundisha wataalam katika ngazi za Shahada ya kwanza (*degree*), Shahada ya pili (*master*) na Shahada ya tatu (*PhD*). Aidha, wizara inaendelea kushirikiana na *IITA, COSTECH, IRI, ASARECA, AGRA, ROKEFELLER FOUNDATIONS, GATE & MILINDA FOUNDATION (IAEA), TRI, FAO, UNDP, JICA, Kilimo Trust, USAID* katika tafiti mbali mbali ikiwemo mihogo, mpunga, mbegu na mbolea. Ripoti za tafiti hizi zipo na Mhe. Mwakilishi, anakaribishwa kutembelea Taasisi ya Utafiti ili kupata taarifa za karibuni zinazoonesha namna wizara inavyosimamia utafiti huo.

Waheshimiwa Wajumbe, mmeona bajeti ya mwaka jana ilivyokuwa finyu na changamoto nyingi za utekelezaji kama zilivyojitokeza katika hotuba yetu kwenye ukurasa wa 55, 56 na 57. Kwa hiyo, tunachoahidi ni kubwa tutashirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ili bajeti ya mwaka huu 2016-2017 tupate fedha za kutosha kwa asilimia kubwa ili tuongeze ufanisi katika utekelezaji wa programu zetu hizi.

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza napenda kuunga mkono hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Na kabla ya kumaliza nitoe wito kwa Waheshimiwa Wawakilishi, pale wizara inapopandisha miche basi ni jukumu letu sote kuienzi na kuilinda, kwa sababu ni faida ya kizazi chetu kijacho. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kusudio ni kuimaliza kabisa hii bajeti leo leo, lakini muda tulionao kwa sababu nitamuhitaji sasa mtoa hoja aje aanze kujibu hoja za waheshimiwa, lakini tutakwenda kwenye kupitisha vifungu pia.

Nitamuomba sasa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, atutolee hoja ya kutengue kanuni ya wakati ili tuendelee mpaka tutakapomaliza. Lakini kabla ya hapo baadae nitawaomba wataalamu wa mheshimiwa, waweze kushuka ili wakae vile viti vya nyuma kuweza kumsaidia baadae katika upitishaji wa vifungu, kwa sababu ni kwa bahati mbaya sana mheshimiwa hajapata muda wa kukaa na wataalamu wake, yaani amekuja michango yenu imetoka kwa wingi na anahitaji kutoa majibu kwa masuali ambayo mengine yalikuwa yakitaalamu sana na yanahitaji takwimu.

Kwa maana hiyo baadae nitawaomba wale wataalamu wa mheshimiwa, mtaruhusiwa kuja kukaa humu ukumbini ili muweze kutoa msaada. Nichukue nafasi hii kwanza kumuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tafadhali naomba kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hasa nikielewa leo tuko katika mwezi mtukufu wa Ramadhani na wengi wetu hapa tuna misikiti yetu ya kusalisha na mawaidha wakati wa Laasir. Kwa hiyo, kwa kuwa muda tulionao hautoshi kumaliza shughuli zetu ikiwa ni pamoja na kupitisha bajeti hii, na kwa kuwa leo ni Ramadhani, kwa hiyo, naomba sana waheshimiwa, tujitahidi ijapokuwa tutaweka kanuni kando ili shughuli zetu tuzimalize mapema. Kwa hiyo, naomba Mhe. Spika, tuweke kanuni kando ili tuweze kumruhusu Mhe. Waziri, amalizie kufanya majumuisho ya wizara yake pamoja na kupata muda wa kupitisha bajeti hii. Mhe. Spika, naomba tuweke kanuni kando ili tuweze kumaliza shughuli zetu zilizo mbele yetu leo. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa, kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, tafadhali niache kwanza nihoji, kaa chini.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya mheshimiwa, wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba sasa nichukue nafasi hii kumwita mtoa hoja ili aje awasilishe mada yake. Tadhali karibu sana Mhe. Waziri wa Kilimo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, awali ya yote naomba niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na utukufu kutujaalia jioni hii baada ya shukurani na dua nyingi za waheshimiwa kukiri kuipitisha bajeti hii ili tukasimamia maendeleo ya nchi yetu.

Pili, naomba kwanza niwataje wale wote walioshiriki ama kwa kuchangia kwa maneno au kuchangia kwa maandishi kwenye hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo.

Mhe. Spika, kwanza niishukuru sana kamati, kamati imefanya kazi nzuri sana, wakati sijaingia kwenye Baraza hili huko nje watu walifikiria kwamba Baraza hili litakuwa bubu kwa sababu hawapo wenzetu na kadhalika. Dhana ilikuwa potofu sana na wanaoangalia hali ya wajumbe wanavyochangia, Wenyeviti wa Kamati wanavyodhibiti mambo katika kamati, ni kielelezo thabiti kwamba Baraza hili lina watu sahihi wa kuwatekelezea mambo yao wananchi. Nataka niwapongeze sana kwanza Wenyeviti wote wa Kamati na hasa kamati iliyosimamia wizara hii, kwa kweli wamefanya kazi ya kiutaalamu sana kinyume na matarajio ya watu wengi sana. Mimi niliposoma taarifa yao kwa mara ya kwanza kusikia kwa bahati mbaya sikuwahi kufika kwenye kamati, nimeridhika kabisa pamoja na uzoefu wangu wote mkubwa nasema hawa watu wamekomaa na wana uwezo mkubwa sana. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Sasa kamati Mhe. Yussuf Hassan Iddi, ndiye Mwenyekiti lakini hapa iliwasilishwa taarifa yao na Mhe. Hamad Abdalla Rashid, kule nyumbani maarufu tunamwita (Gerei), na ndugu yangu Mohammed Aboud, alikuwa ananitania anasema leo watu wa Wawi nyote mmeazimia hapa, maana yake yeye ni mtu wa Wawi na mimi ni mtu wa Wawi, basi mambo yalikuwa mazuri. Nakushukuru sana. Pili, niwashukuru sana:

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
Mhe. Masoud Abrahman Masoud
Mhe. Simai Mohammed Said
Mhe. Suleiman Sarahan Said
Mhe. Ali Khamis Bakar
Mhe. Bahati Khamis Kombo
Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti
Mhe. Shehe Hamad Mattar
Mhe. Shamata Shaame Khamis
Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
Mhe. Mtumwa Peya Yussuf

Mhe. Hassan Khamis Hafidh
Mhe. Abdalla Ali Kombo
Mhe. Omar Seif Abeid
Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Said Omar Seif
Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Juma Ali Khatib)
Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Said Soud Said)
Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na
Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

Mhe. Spika, nawashukuru sana kwa kazi nzuri waliyoifanya na mimi naomba tuungane katika kuipitisha bajeti hii.

Aidha, naomba niwatambue waheshimiwa waliochangia kwa maandishi, na kwa bahati mbaya wengine hapa namalizia ndio wananiletea tena inawezekana katika orodha yangu hawatokuwepo nitaomba radhi nitakapokumbushwa nitaweza kuwaandika baadae nao ni:-

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
Mhe. Masoud Abrahman Masoud
Mhe. Simai Mohammed Said
Mhe. Suleiman Sarahan Said na
Mhe. Naibu Spika, nae vile vile alinileta kwa maandishi mawazo yake.

Napenda niwashukuru sana wote na wale ambao sijawataja naomba wataalamu wangu watakaponiletea nitawataja majina yao, nawaomba radhi sana.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, samahani, bahati nzuri kumbe imekuja nyengine hapa ni:-

Mhe. Ali Khamis Bakar
Mhe. Bahati Khamis Kombo
Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti
Mhe. Shehe Hamad Mattar
Mhe. Shamata Shaame Khamis
Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
Mhe. Mtumwa Peya Yussuf

Mhe.Hassan Khamis Hafidh wengine wamerudia kule wamechangia na wameandika tena
Mhe. Abdalla Ali Kombo
Mhe.Omar Seif Abeid ni wale wale eeh, basi na hao wataalamu wamenikorofisha.

Mhe. Spika, la kwanza nataka niseme mambo matatu ya jumla. La kwanza nataka tumshukuru sana Dkt. Ali Mohammed Shein. Tumshukuru kwa sababu ilijengwa dhana kwamba daktari Rais wetu si msikivu. Mara anaingia kwenye awamu ya sita, mimi nikiwa Mbunge, nikiwa vile vile ni Mbunge ninayeiwakilisha Afrika katika Bunge la *AWEPA*, nilikwenda Ireland nikakuta kilimo cha mwani kinavyotunzwa, kinavyoendelezwa na kukuzwa. Miongoni mwa watu tukashirikiana mmoja alikuwa *Former Minister* wa *Agriculture* wa kilimo nikawaomba waje Zanzibar. Wakaja Zanzibar nikaenda nao mpaka Micheweni Pemba wakauona mwani halafu wakafanya mazungumzo na Rais Shein pamoja na Balozi wa Ireland mambo matatu tukawaomba.

La kwanza, tukaomba kufufua shamba la ng'ombe Chamanangwe huu walikuwa wakiuendesha wao zamani.

La pili, tukaomba kuendeleza ukulima wa mwani. Baada ya kumaliza mazungumzo yale mimi sijawa MBM, wala siko Zanzibar niko kwenye Bunge la Jamhuri, Rais akanifuatilia sana wageni wetu wamefikia wapi kwa yale tuliowaambia. Huyu ndiye anayeambiwa Rais sio msikivu, sijawa MBM, nikamwambia Mhe. Rais nafuatilia. Kwa bahati nzuri wale wenzetu wamefanya mawasiliano na mimi na kwa taarifa yenu hata jana kile chuo kinachofanya utafiti wa mwani wamefanya utafiti wakagundua kwamba mwani huu tunaoambiwa hauna bei, kumbe una bei nzuri na unatumika vizuri *South Africa* wana kiwanda. Na wameniahidi tarehe 20 mwezi huu watakuja na mtaalamu atusaidie kuongeza thamani ya mazao ya mwani kuliko yale mlionja jana na juzi. Hilo la kwanza.

Rais huyu Shein nikenda kumueleza kwamba sekta hii inaajiri watu 23,000, watu 23,000 mara 5 chukua kila familia ina watu watano unazungumzia watu 100,000, Mhe. Rais hatuwezi kuwaacha mkono watu hawa, akaniambia kabisa kabisa itakuwa ni ujinga wa kisiasa kuwaacha mkono. Huyu ndiye Rais anayesikiliza watu jamani, na ndio maana akaunda kamati chini ya Makamu wa Pili wa Rais tusimamie namna bora ya kusimamia zao la mwani ili mwani ama tununuwe au tu-*process*, lakini wakulima tusiweze kuwaacha solemba hata kidogo.

Hizo ni juhudi ambazo amazichukuwa Rais. Na mimi nasema wewe ni CCM, nikasema siyo, mimi ni Mzanzibari na mimi ni Mtanzania, na mimi ni muumini wa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu anasema; "*Inna llaha Maasabirin*" Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaosubiri, halafu anasema "*Haku llah hakku rassul wauliamri minkum",* ndiyo maneno ya Mwenyezi Mungu hayo, usiporudi kwenye *tauhid* shida utapata kubwa sana, unapambana na Mwenyezi Mungu, mimi sina ubavu wa kupambana na Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu ameandika Rais Shein awe Rais, mimi "*Haku llah hakku rasul wal-amri minkum"* lazima nitii, lazima nitii, ni amri ya Mwenyezi Mungu. Sasa kama wewe unapingana na Mwenyezi Mungu endelea tu na mimi nawaambia wenzangu mapema, mimi namfuata Mwenyezi Mungu anaefuata shetani aendelee kufuata shetani. (*Makofi*)

Mhe. Spika, na ninawaambia kabisa Wazanzibari, tunataka maendeleo tuna mambo mawili tu ya kufanya; kumuweka Mwenyezi Mungu mbele na kufanya kazi kwa bidii na kutii viongozi wetu. Ukifanya vyenginevyo vyovyote huwezi ukafanikiwa katika maisha yako, *take it from me*, kuwa na hela, kuwa na kila kama hujamuweka Mwenyezi Mungu mbele na amri zake na ukatii amri aliyokuagiza Mwenyezi Mungu huwezi kufanikiwa hata siku moja. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hiyo, nasema huo ndio msingi wangu, Mheshimiwa, aliniuliza msimamo wangu, msimamo wangu ni thabiti kabisa, naheshimu kiongozi yeyote, nimekuwa kiongozi wa upinzani Bungeni, nimefanya kazi yangu kama kiongozi wa upinzani Bungeni, nikiunganisha vyama chungu nzima ndani ya Bunge, lakini tulisimama na nguzo na Bunge la 9 likajenga heshima katika nchi hii chini ya uongozi wangu sijabadilika, na lolote zuri linalofanywa na Serikali ni wajibu wetu kuliunga mkono, lenye kasoro tulirekebishe kwa sababu hii ni nchi yetu, hilo nilitaka niliseme la kwanza la muhimu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini la pili niseme, uko wajibu unaofanywa na Serikali na uko wajibu unaofanywa na raia. Serikali inaendelea tu vizuri kama raia anatimiza wajibu wake, kwa sababu ukitimiza wajibu wako Serikali yenyewe itaona haya, mimi sijapata kuona Serikali yoyote duniani inatoa asilimia 80 ya *inputs* za kilimo kwa ruzuku, niambieni moja Balozi anajuwa hapa Balozi Karume, asilimia 80 inampa mkulima ajiendeleze halafu mkulima anasema haisaidiwi na Serikali anasaidiwa. Waheshimiwa, nikiwasomea hapa takwimu za boti zilizotolewa na Serikali ni 148, kawaulize wavuvi zikowapi wameshaziuza. (*Makofi*)

Mhe. Spika, idadi ya mashine zilizotumika kila boti moja angalau tumewapa mashine moja chukuwa hesabu hiyo hiyo tu, mbali ambazo zimeharibika na

nyengine tukatengeneza ziko wapi, waulizeni kwenye majimbo yenu, nimewafuatilia mimi nimewauliza, tukutaneni jamani munieleze mashine mulizonazo ziko wapi, kila mtu anakupa hadithi. Kuna mmoja nilimpa mimi mwenyewe mashine bure mimi mwenyewe, *wallahi laadhim* havui, kauza. Kwa hiyo, nasema uko wajibu wa Serikali na Serikali hii inachangiwa na walipa kodi wote, haichangiwi na wavuvi peke yao, haichangiwi na wakulima peke yao, haichangiwi na wafanyabiashara peke yao, tunaichangia sote, kinachokusaidia Serikali lazima ukitunze kwanza. (*Makofi*)

Mhe.Spika, leo anatoka binadamu eti ana akili timamu anakwenda kuukata muembe, anakwenda kukata migomba, anakwenda kukata nini, huyu hajui athari zake, Mhe. Mohammed Aboud, kazieleza vizuri sana, lakini athari kubwa moja ni kwamba na yeye ni sehemu ya mchango ule anaoutoa, ni sawa sawa amekaa juu ya muembe na yeye anajikata kiuno, anajikata mwenyewe tu, mama yake na baba yake wamechangia, yeye anachokata baba yake na mama yake ama *indirect* au *direct* wamechangia katika pato la taifa, utu gani, ubinaadamu gani huu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jana nilikuwa naangalia kwenye televisheni maskini ya Mungu, Sheha yule amekatiwa migomba yake, amekatiwa miti yake, ni ubinaadamu gani? Nenda Makka pale ukakate mti wakati wa Hijja, unaruhusiwa? Unatoa *fine* kukuonyesha Mwenyezi Mungu hata mti wacha binaadamu ni dhambi kukata, leo unakwenda unamkatia mtu mazao yake, ameshategemea maskini ya Mungu yamsaidie katika maisha yake, wewe unakwenda kumdhulumu, nasema kwanza ni dhambi, lakini nakubali kabisa na wenzangu sasa Serikali tuwaambie kabisa katika Wizara ya Mambo ya Ndani, habari ya hadithi ya kufanya *research* hakutaki *research* wakamatwe watu wapelekwe Mahakamani.(*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi nimekaa *Home Affairs* sijapata kusikia polisi wanafanya *reconciliation* au *dialogue* na muhalifu, *a criminal is a criminal*, muhalifu unamkamata aka-*prove innocence* yake Mahakamani *that's all*. Wanakwambia tunao tunawadhibiti, unawadhibiti nini, saa arubaini na nane peleka Mahakamani, waende Mahakamani wakasema wao ni *innocent.* Tumekwenda pale na Rais, anasema kaja kiongozi fulani hapa ndie aliowa-*organize* anakuja na *confess* kama yeye anakubali, hujamkamata, namwambia askari gani wewe, *I'm sorry to say so,* haiwezekani, hatuwezi tukachezea uhai wa watu, hatuwezi kuchezea rasimali za nchi.

Serikali inagharimika, walipa kodi watu wanaanguka katika mikarafuu halafu tumwachie mtu mmoja tu kwa sababu ya uzembe anafanya uzembe, hapana, *we*

have to stop this business. Hili nasimama kabisa kidete wala hatukubali kabisa kabisa, kuna mmoja ananiambia eh, ukisema sana watakuja kukuuwa, namwambia kwani tunakufa mara ngapi, si tunakufa mara moja tu au kuna mtu anakufa mara mbili, mara moja tu, *you die only once*, tutakutana na Mwenyezi Mungu mbele ya safari, lakini *we have to say*. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hiyo, mimi ninakubaliana kabisa na Wawakilishi na Mhe. Hamza, amelisema kwa uchungu sana na wengine wengi, naomba kabisa tusimame kidete katika hili na maeneo yetu tunawashuku watu tuwaseme fulani na fulani tunamshuku anafanya tendo hili, kwa sababu na askari na wao wanataka wapate *information,* wapeni habari, akipewa *information* hakuifanyia kazi tumkamate ambaye amepewa *information* haikuifanyia kazi, hatuwezi kuliacha hili jambo hivi hivi, mimi nalisema kwa uchungu kwa sababu nimekuta mpunga, mpunga una kimo hichi hapa umekwenda kukatwa kama mtu anakata majani ya nyumbani kwake, binaadamu gani, yule mama anasema muhogo wangu nimeshategemea Ramadhani hii nitakula muhogo unakwenda unang'olewa wote, hivi unapata nini wewe. Sisi tunajitahidi tunatoa mbegu, tunajitahidi tunasaidia, wewe unasema hapana, unakwenda mtu unamdhulumu haki yake, hapa ninasema ninaungana na Waheshimiwa Wawakilishi, naungana na Serikali lazima tuwe *vigilant* katika kupambana na jambo hili likome. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hilo lilikuwa la pili, la tatu, Mhe.Mwenyekiti, niseme la mwani, nimesema kidogo nikaliacha. Nimesema sekta hii inaajiri watu wasiopuguwa laki moja. Waziri Amina, namshukuru sana aliposema juu ya viwanda ambavyo vita-*process* mazao haya. Sisi tuna uchumi ambao unaenda mara mbili; kilimo cha biashara na kilimo cha chakula, karafuu kwetu ndio kilimo cha biashara, maana hatuli karafuu wala hatuli makonyo, tuna-*process* na kuuza, sasa hivi tumeingia kwenye *essences* mbali mbali kama mchaichai na kadhalika tuna-*process*, kwa hivyo. *agro-industry* ipo inahitaji kukuzwa na inahitaji kutunzwa. Na mimi nataka kukuhakikishieni kabisa tupitisheni hii bajeti mtupe muda, tumefanya kazi kubwa katika kipindi kifupi sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Cha kwanza kuweza kujua tatizo gani tulilonalo.Tatizo la kwanza hatuko *focused* kwamba, mwaka huu tunataka tuhakikishe jambo fulani tumelimaliza na tumelifikia lengo fulani hatuko hivyo na ndio maana tukiisoma bajeti utakuta hapa umepeleka shilingi kumi, hapa ishirini, hapa thalathini, huoni *impact* tunataka tuone *impact.* La kwanza kabisa alilosema Rais, hatuna sababu kwa nini tuendelee kuagizia tani thamanini elfu za mchele, hakuna sababu, tuna hekta 8500 kwa ajili ya *irrigation,* kwa utalaamu walioutoa kina dokta hapa kwamba tunaweza tukatoa tani 14, mimi mwenyewe Bagamoyo

chini ya magereza tukizalisha tani 7.5 za mpunga kwenye hekta moja kwa mvuno huu mmoja, kwa hivyo, mvuno miwili unapata tani kumi na tano, tupate tani saba tu zinatosha kabisa kupata kilo thamathini elfu za mchele katika mivuno miwili ya msimu.(*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa Mhe. Mohammed Aboud, kasema vizuri, watu wanajengwa ovyo, vianzio vya maji vinaharibika, kwa hiyo, tuna tatizo la maji, tumewaita ndugu zetu kutoka Israel na tumezungumza nao watusaidie katika *drip irrigation* kama unatumia maji kidogo lakini unazalisha vizuri, hata lile tatizo la mbolea kuharibu ardhi ukitumia *drip irrigation* unatia mbolea kiasi kinachotakiwa, kwa hivyo, huwezi kupata matatizo ya ardhi baadae, wanakuja tarehe 25 mwezi huu tunamaliza mazungumzo tunaandika *MU*, tunaipeleka kwa Mwanasheria Mkuu tukimaliza hapo tunaanza biashara. Tumalize la mchele, (*Makofi*)

Mhe. Spika, nimekutana na Mzanzibari hapa mzuri tu kasomea Uturuki anajuwa kilimo kuliko ninavyojuwa mimi, amepewa zawadi hata Tanzania huku, ameniambia tugaiye hekta 200 tukazalishe mbegu ya mpunga sisi wenyewe, hivi sasa ameshaandika barua, ameshaileta, Katibu Mkuu wangu anasema tukimaliza bajeti tunaenda kumkabidhi eka 200 atuzalishie mbegu, hatuna haja ya kuzitafuta mbegu kutoka nje tena basi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hiyo, tukizungumzia sekta ya mpunga tu peke yake katika kipindi cha miezi sita Waheshimiwa, nitawachukuwa mukatembee mukaone hali ilivyo, na mimi nimemwambia Rais Shein, kama nilivyowahi kumwambia Rais Nyerere, nilimwambia miezi sita Rais Nyerere kama sijailisha magereza najiuzulu; namwambia Rais Shein ikifika miaka mitatu kama hatujazuia kuagizia mchele hapa bora tu nikuwachie tu Wizara yako. Aibu, labda watu wafanye *sabotage*, labda itokee *sabotage*, lakini kama kuna *good will* hakuna sababu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Zanzibar ndogo sana, eneo dogo sana, mie muda mfupi mwezi mmoja na nusu nimeshatembelea *almost* 70% ya eneo hili la kilimo. Kama unapata watu *committed* na unafanyaje katika hili lazima *u-involve private sector* ifanye kazi, ndiyo nasema lazima tukubali hilo.Ndugu yangu Bakhressa ameomba nafasi kiwanda chake cha maziwa aruhusiwe apewe eneo afuge ng'ombe wa kutosha Bambi, lakini wanasiasa sisi tukasema ah! ardhi tusimpe, kiwanda kimekaa anaagizia unga. Nakubaliana kabisa na Mhe. Hamza, tuwache siasa tufanye kazi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuna *investors* wako tayari kabisa kutusaidia, nimewaleta ma-*investors* kutoka Brazil, nazungumzia tatizo la maziwa, tunahitaji ng'ombe 18,000 wa maziwa wanaozalisha angalau lita 30, nimewaleta na nimewapeleka kwenye mashamba yetu ya ng'ombe, wakasikitika wakasema ah! shamba lote hili hekta 300 una ng'ombe 40 Hamad na kila ng'ombe anatoa lita tatu, aibu. Kesho kutwa tukiwaambia tunawapa ardhi hawa kufanya hiyo kazi mtaleta siasa hapa ndani, mtaleta siasa, sasa *when I commit myself,* ni kwamba lazima tui-*allow private sector* ifanye kazi na *private sector* itafanya kazi kama sisi tutashirikiana humu ndani kukubali kama *private sector* ifanye kazi.Kwa hivyo, sio kuahidi kwenye *air* tu, hata Mwalimu Nyerere nilipomwambia nilimwambia ukinipa zana hizi na hizi na hizi mimi nafanya, akanipa nikaenda magereza *KPF* nikakaa nao nikamwambia mimi nimechukuwa miezi sita ya kwenu minne kwaherini, miezi sita tumeuza chakula, *commitment has to be there,* haiwezi kuwa kwa mtu mmoja tu, tuwache siasa.

Mhe. Spika, viongozi wetu wa Mikoa, viongozi wetu wa Wilaya waelewe tunataka kufanya kazi ya kuondosha umasikini katika nchi, huwezi kuondosha umasikini kwa siasa, wanaongoja siasa ni wale wanaongoja mkono unatembea kama fisi wanafikiri utaanguka, huu hauanguki tena unaendelea na safari, mkono huu hauanguki unaendelea na safari. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Hamza na wenzetu nakubaliana na wewe kabisa kabisa *let's us leave politics outside* kama kweli tunataka ku-*feed ourselves.*

Mhe. Spika, nimemwita mzalishaji anayesafirisha kuku kutoka Brazil na Marekani nikakaa nae, nikamwambia kwa nini usinunue kuku hapa Zanzibar, akaniambia nipe Zanzibar nahitaji kilo laki tatu na nusu kwa wiki, kilo ngapi, laki tatu na nusu kwa wiki, mnazo? Anyanyuke mmoja anambie mimi nina laki moja tu, anyanyuke mmoja anambie mimi nina hamsini elfu tu, *but the industry is there already,* hasa uamuwe kukifunga kile kiwanda au tuendelee kufanya hiyo shughuli, mimi nikamwambia hapana, tukuwezeshe nini ili Wazanzibari wazalishe wenyewe kuku, akasema vitu vitatu; cha kwanza unipe kiwanda cha kuzalisha chakula cha kuku, hawa wafugaji mnaowapigia kelele tatizo lao kubwa hawakuwa na pahala pa kufugia kuku, hawakuwa na chakula cha kulisha kuku, mnipe kiwanda kwanza, pili nihakikishieni mna maji ya kutosha, tatu nihakikishieni na umeme wa kutosha, nne nahitaji *skilled people,* yaani watu wenye uwezo wa kufanya kazi, vijana wetu tunawafundisha kazi, nenda leo kaangalie kwenye mahoteli tuna wageni wafanyakazi, *people are not skilled,* hawana uwezo tuwa-*train* watu wawe na uwezo.

Mhe. Spika, nimekwenda Chuo cha Kilimo Kizimbani nikakaa na wataalamu, nikawaabia wataalamu kuna *challenge* hii, nashukuru sana leo mmesema jambo

kubwa sana kwamba, wao wataalamu wa kilimo waonyeshe mfano, na mimi nasema msije mkaonesha mfano halafu mkasema wanaiba Serikalini, maana yake ndio tatizo letu na sisi, atatumia utaalamu wake atatumia muda wake wa kazi atakwenda kuzalisha, tusije tukamwita mwizi baadae, na mimi nasema hiyo ndiyo njia bora ya kuendeleza watu wetu wabaki hapa, kwa sababu mishahara ni midogo wanachokipata, wanahitaji mshahara mzuri na mshahara mzuri wataupata kama kuna muda wakati sio wa kazi anafanya shughuli nyengine, nikawaambia hivi kweli hatuwezi kupata kilo laki tatu na nunu sisi, wakanambia Mheshimiwa, tatizo ni kubwa hapa alilosema Mhe. Mohammed Aboud, ni *finance*,

Mhe. Spika, mimi Mheshimiwa, nishaingia kwenye biashara. Nimetembea mabenki yote natafuta mkopo wa dola milioni mbili na nusu kwa ajili ya kununulia meli ya uvuvi imeshindikana mpaka Ulaya wakanipa asilimia 80 ya mkopo natafuta asilimia 20 hapa ndani ya nchi imeshindikana, unakwenda kwa *Banker* anasema aah! Sijui mambo ya uvuvi na nini, tunaona ni *very risky, risky area*, hivyo hivyo kwenye kilimo, hivyo hivyo kwenye uvuvi. Kwa hiyo, moja ambalo ninalikubali na waheshimiwa, mmelisema hapa tuwe na Benki zilizo-*specialize* katika *line* hiyo, *I agree hundred percent*, tumeli-*discuss* sana hili *when I was Vice President* wa *Africa* kwenye Bunge la *IPU* kwamba njia za viungo vya fedha hizi kusaidia sekta hizi za kilimo ni tabu, lazima Serikali zianzishe taasisi mbali za kuweza kusaidia wakulima na wafugaji, ndio maana sasa hivi benki ya kilimo, hata wanawake walikuwa hawataki kukopeshwa kuna Benki ya Wanawake hivi sasa, mimi nafikiri *we have to go* na mimi naishukuru sana *Islamic Bank* yetu tuliyonayo tumejitahidi sana kuweza kuwasaidia watu walioandika miradi yao vizuri.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kwenye Wizara tulichojipanga katika hilo, mambo matatu; La kwanza, wataalamu tunaowafundisha lazima na wao waonyeshe mfano sio tu kwamba na wao wakae tu. La pili, tuhakikishe kabisa asilimia 70 ya muda wetu tunautumia *field* badala ya kukaa maofisini. Na la tatu, hawa tunaowafundisha hebu tukawafanyie tathmini kile tulichowafundisha wanakiendeleza. Lakini la nne, tuzungumze na wenzetu wa *financial institutions* namna gani wanaweza kuwasaidia ili hii sekta nayo ikakuwa. Hizo ni *measures* tumezichukua katika kipindi kifupi sana. Kwa hiyo, mimi nasema tuko *positive* katika hilo, *investors* wote wako tayari.

Mhe. Spika, nimelizungumza suala la kuni asilimia 90 bado tunaendelea kutumia kuni na mkaa, nchi imemalizika, nimekwenda kwa ndugu yangu Hamza yule anayevuna mchanga pale nikaliangalia lile eneo, sio Hamza huyu, ukenda pale ukiliangalia lile eneo unasema Zanzibar imekwisha, waliopewa

maeneo wengine wameiba usiku mna maeneo kama kumi na tano watu wanaiba usiku hawana kibali, nenda kaangalie mashimo yaliyoko, Zanzibar hii iko *below sea levels*, ukichimba zaidi mita tatu, maana yake unazidi kukizamisha kisiwa. Tumekaa kwenye Baraza la Mapinduzi tunafikiria njia gani ya kuliokoa hili, ndio kazi ambayo tunafanya chini ya Makamo wa Rais kuona namna gani tunaweza kupunguza uchimbaji wa mchanga ovyo ovyo kiasi ya kwamba nchi inabaki sio salama, *we are doing that*, na njia ziko mbili.

1. Tuingie kwenye *prefabricated housing.* Tuache kujenga kwa kutumia matofali huu wakati umekwisha, nchi ndogo itamalizika tu. Tuna vibali sasa hivi waliyoomba zaidi ya 38 kila mmoja anataka kuchimba mchanga, ukiwapa watu kumi nchi imekwisha. Hilo ni tatizo la msingi tunalikabili katika serikali.

Hata Rais wakati anasema, alisema jamani jambo lenyewe ni *very sensitive*, unajua kwa sababu gani, si watu wanapata riziki yao huko ndani, ukienda ukilisimamisha tu hivi kienyeji enyeji haiwezekani.

2. Lakini nataka tuelewe kama tuna tatizo kubwa, tuna tatizo la ukataji wa minazi ovyo, tuna tatizo la ukataji wa miti ovyo.

Nimekwenda kwa mzalishaji mkubwa sana kwa kutumia minazi Selem, nikamwambia Mheshimiwa, wewe ndio mnunuaji mkubwa wa miti ya minazi tufanyeje, akacheka sana, akanambia Mheshimiwa, mimi ni mtaalamu, kosa la kwanza mlilofanya Zanzibar hamkuweka alama mnazi gani na gani unafaa kukatwa, anasema kiutaalamu lazima uvunwe tu huo mnazi, si umefika miaka mia hautoi tena nazi, kilichobaki sasa unasaidia tu kwenye mazingira, huo mnazi lazima ukatwe lakini usikatwe bila ya kupandwa mwengine. Anasema matokeo mliyonayo matatu; la kwanza, mnakata ulio mpevu, mnakata ulio mchanga lakini hampandi. Sasa wizara sisi kazi yetu ni kutoa mbegu, ni kama vile bwana mtu amekuja umempa mke, kenda nyumbani halafu useme jamani huyu mke wangu nilishie tena, hiyo sio sahihi. *Role* ya serikali ni kusaidia kutoa miche, tunatoa miche ya kutosha ya kila aina; ya mikarafuu, ya minazi na kadhalika, lakini wajibu wa kutunza mche huu mpaka ukawa salama ni wa kwako.

Mhe. Spika, ukishakwenda hospitali daktari kakusaidia umepata mtoto tena unamwambia na huyu mtoto huku nyumbani njoo unitunzie, hapana. Sasa kama miche haitoshi mimi nasema tuka- *budding* tutatoa miche zaidi.

Vile vile, nataka tuiongeze *private sector* iweke miche, sio miche serikalini tu, nawashukuru sana wale wakulima waliokubali kuweka miche ya mikarafuu na

wao. Tuwekeni vitalu katika mashamba yetu kuweka miche, miche ni ya kwako, sisi kazi yetu ni kusaidia utaalamu wa mbegu gani bora ya kuweka, hiyo ni kazi yetu na hili mimi nasema nitawabana wataalamu sana, nikimkuta mtaalamu kakaa mara tano ofisini hajanipa taarifa ya *field* hataachana naye na wanalielewa. Nimewaambia mimi hapa hakuna habari ya siasa, anayetaka kubaki kwenye siasa abaki kwenye siasa, lakini hapa ni "kazi tu". *(Makofi)*

Kwa sababu hata Mwenyezi Mungu anasema; "Ukishafanya ibada zako asubuhi, (*fantashiruu fil-ardhi*), katafute riziki", sio ukakae barazani upige siasa, siasa hushibi hata kidogo. Kwa hiyo, hilo tunalifanya Waheshimiwa na nakuombeni sana na ninawaambia kabisa wale wanaokata miti ovyo, wenye mashimo ya kuchimba udongo usiku na mchana tutawavizia usiku, wanaopitisha ng'ombe kienyeji pale mimi nitaamka saa kumi ya usiku nitakwenda pale tukiwakamata tutawapeleka polisi. Kuna watu wanaleta ng'ombe na mbuzi kienyeji kule Kisakasaka, nawapa habari kabisa waache mara moja, tutawavizia na tutawakamata tu.

Mimi nashukuru sana ninaye kamanda hapa waziri na vikosi tutafanya kazi, lazima nchi ibaki kwenye *law and order*, hakuna *development* kama hakuna *law and order*, *we have to have law and order in order this country to develop*. Tumeelewana jamani? Nawashukuru sana naomba sasa mniunge mkono kwa hilo. (*Makofi)*

Kwa hiyo, ukipata *support* ya wanasiasa wenzako na wakiona kwa kweli una nia ya kufanya kazi kama tulivyo na nia, Rais kaunda *cabinet* nzuri sana. Nataka nikwambieni tumpe *credit* sana Rais, amekuwa *very careful* katika kuunda serikali. Makosa madogo madogo ya kibinadamu si kila mmoja anayo hapa, yuko mkamilifu eti hapa, hamna mkamilifu. Hata Manabii wenyewe na wao wameteremshiwa sura kali kali kwa kuonywa kutokuwa wakamilifu, lakini amejitahidi kwa sababu nia yake ni safi na sisi lazima tuoneshe nia safi.

Mimi nawashukuru Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi toka tuanze tumeonesha *spirit* ya kuiunga mkono serikali, tuendelee kuiunga mkono serikali, mimi naamini tutafika mahala pazuri.*(Makofi)*

Suala la takwimu nakubaliana na nyinyi kabisa na takwimu sio tatizo letu sisi, nenda Afrika kote kuna tatizo kubwa la kukusanya takwimu. Katika moja ambalo *FAO* wamekubali kutusaidia namna gani tutaboresha takwimu zetu. Nakubaliana kabisa na Dkt. Mwinyihaji Makame kwamba, ni vizuri ukiambiwa viazi umezalisha tani 10 basi tani 10 zimezalishwa kwenye hekta ngapi, *unit cost* ijulikane, *unit production* ijulikane. Hilo tunakubaliana kabisa na

ninakuhakikishieni kabisa mtakuja kuona maendeleo baadae tunavyokwenda kwa kutumia ardhi ndogo kuzalisha zaidi na ndio maana tumesema kuanzia sasa bidhaa zote zipimwe, mambo ya kuuziana kwa mafungu yamekwisha wakati wake. Kazi yetu kubwa sasa ni kutafuta minzani za kutosha tuhakikishe kuna minzani, lakini kuna zaidi ya hili, watu wanaiba pesa katika hili, ukienda pale yeye anakukisia tu, yeye anachukua risiti kwa kukisia tu.

Kwa hivyo, mapato ya serikali yanapungua na hili ni eneo moja ambalo nashukuru sana kamati wamelisema, kwamba hawaridhiki na kiwango cha mapato tunachopata, nakubaliana kwa asilimia mia moja na nyie.

Juzi nilipokwenda kwenye shamba la mchanga niliwauliza, ehee, wewe mtu wa Halmashauri unakusanya kiasi gani, risiti zako ziko wapi, akanionesha, wewe wa wizara kiasi gani, hee, na wewe mwenye shamba kiasi gani, hee, nataka tufanye *reconciliation* ya haya mambo. Shehe ilikuwa kigugumizi kikubwa sana, kufanya *reconciliation* ilikuwa ni kigugumizi, takwimu hazikubaliani. Tunamuomba Waziri wa Fedha kuanzia sasa tupate ile *electronic device* ili tuweze kukusanya mapato vizuri. Haya mambo ya kuandikiana risiti hizi za kubabaishana wakati risiti zenyewe sio *genuine* wakati wake umekwisha. Nakubaliana Wajumbe, kabisa tunahitaji kudhibiti mapato ya serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ndugu zangu wamezungumzia sana suala la kusarifu mazao kwenye maabara. Pale chuoni Kizimbani nimesaidiwa na *KOICA* kujenga ile taasisi. Kwa bahati mbaya hawakutupatia vifaa vyenyewe, tumeendelea na mazungumzo nao lakini tunataka sasa tuipeleke serikalini ili tutafute vifaa vya maabara sisi wenyewe. Hili nakubaliana na nyinyi kabisa katika kamati kuwa hili tutalifanyia kazi ili tuone maabara zile zina vifaa vya kutosha. Lakini *centre* tayari ipo, imeshajengwa chuoni pale tutaifanyia kazi ili iweze kufanya kazi katika hili jambo.

Nimeulizwa suala la Makurunge. Hili nataka kukupeni uthibitisho tena wa Rais Ali Mohammed Shein. Niko Bungeni pale nikakaa siku hiyo ikanijia tu, tulikuwa na hekta 50,000 Makurunge ziko wapi? Basi nikenda kwa Waziri wa Ardhi wa Bara nikamwambia nakumbuka Zanzibar ina hekta 50,000 Makurunge, akanambia ni kweli, ngoja nitalifuatilia. Mimi nika-*fire out* nikaja hapa nikaoana na Rais Ali Mohammed Shein, nikamwambia Rais nakuomba ulifuatilie lile shamba la Makurunge tutalikosa, akanambia nakushukuru sana nitalifuatilia, amelifuatilia akakuta zimebaki hekta 7,000 kutoka 50,000. Zimebaki kwa sababu wakati wanaendelea na *negotiation* ilikuwa sisi SMZ isipewe serikali ardhi, ardhi haipewi serikali inapewa kampuni, tulitakiwa tuunde kampuni ndio tukaombe ile ardhi, basi tukachelewa chelewa mpaka

tukafikia hekta 7,000 ndio tumeunda sasa hivi hiki Chuo cha Kilimo cha Kizimbani ndio sasa hivi mmiliki wa hizo hekta 7,000 na wameshatangaza *tender* ili kufanya usanifu hekta 7,000 tunazitumiaje.

Kwa sababu gani? Halmashauri ya Bagamoyo wamesema eneo lile sasa sio tena la kilimo, ni eneo ambalo litumike kwa shughuli nyengine za kibiasahara mahoteli na kadhalika. Sisi kwa upande wetu tukasema *Alhamdulillah* maana ndani yetu kuna *beach* kule ndani tutajenga mahoteli, chuo kitapata fedha za kujitegemea wenyewe. Hiyo *study* inafanyika na ninawashukuru sana ndugu zetu wa Bagamoyo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia zile hekta 7,000, lakini vile vile mlango uko wazi kama tutataka maeneo mengine ya kwenda kulima tutakapoanzisha kampuni yetu tutalishughulikia hilo nalo vile vile.

Kwa hivyo, namshukuru sana Rais Ali Mohammed Shein, nasema ushauri huu nimempa sijakuwepo hapa. Kwenye *GNU* hawa waliokuwa wakisema hasikilizi, mbona mimi nasema anasikiliza tena masikio yake ni mapana tu, maana anakupa uhuru wa kuzungumza sijapata kuona pahala popote mimi. Anachambua kila neno, kwanza yeye mwenyewe msomi, anasoma, kwa hiyo, si mtu wa kuburuzwa buruzwa tu hivi, anafanya *home-work* vizuri, ndio mnapomuona wakati mwengine hatekelezi jambo, ni mtu ana tabia ya ubinadamu sana na mtu akiwa na tabia ya ubinadamu anaona ah, huyu pengine siku moja ataamka atakuwa binadamu na yeye, ana dhana hiyo tu, *he is a good man*, lakini watu wakorofi wana-*take advantage of that*, tusifanye hayo. Tumsaidieni Rais.

Kwa hiyo, shamba hili jamani tunazo hekta 7,000 liko chini ya Chuo cha Kizimbani na *Inshaallah Biidhnillahi Taala,* karibuni *tender* itatoka tutapata ushauri wa kitaalamu namna gani tuziendeleze katika taswira ambao wenzetu Halmashauri ya Bagamoyo wanahitaji.

Mhe. Spika, suala la malisho limezungumzwa sana. Kilimo bila ya malisho ni kudanganyana, kilimo bila utafiti ni kudanganyana na ndio maana hawa washirika wa maendeleo hasa *FAO* na *IFAD* wamekubali kabisa ku-*invest heavily* katika suala la utafiti, suala la kitaalamu na ndio maana ukitizama katika hotuba yetu utakuta *training* mbali mbali tulizozitoa kwa watu wetu. Lakini kum-*train* mtu ni jambo moja na kuitumia taaluma yake iliyokuwa *trained* ni jambo jengine na ndio maana wengine wakishapata *training* wanaondoka hawakai. Lakini kama serikali ni wajibu kuendelea kufundisha, maana huwezi kumsoma mtu ndani ya moyo wake.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hapa kasomesha watu wengi, lakini wengine hawamo tena, wengine wanamuheshimu wengine hawamuheshimu. Juzi Mufti alipokuwa Pemba alikuwa anazungumza na wanafunzi wake, waliinuka wanafunzi wawili wakasema maneno mabaya sana mbele ya Mufti kana kwamba si wanafunzi wake. Wenzetu wamefika pahala pabaya, wamefika pahala maana yake laana moja kwa Mwenyezi Mungu ni kumdhalilisha na kumdharau mwalimu wako, kumdhalilisha mwalimu wako ni dhambi kubwa sana wamefika hapo baadhi yao, lakini masikini Mufti mtu mzima, mwenye taaluma, ametulia, akawachukulia tu yakaisha. Naomba tuwaheshimu walimu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, wako vijana wengi tumewapeleka mafunzo kama 72, naamini kabisa na Chuo chetu cha Kizimbani sasa hivi tutajitahidi sana kukipanua kichukue vijana wengi zaidi ili vijana waweze kupata taaluma na ninakubaliana kabisa na ushauri wa Wajumbe hili suala la ajira katika wizara hii ina sehemu kubwa sana ya ajira lazima tuifanyie kazi ajira hii ipatikane. Sasa tunafanyaje katika ajira? Kuna mambo matatu.

Nilipokutana na Chama cha Wafanyabiashara nikawaambia kina Bopar rafiki yangu nyinyi mnaagizia mchele, mbona tuna eka 8,000 hapa kwa nini msianzishe mchele hapa hapa? Kwa sababu tatizo lile alilosema Mheshimiwa, hapa ni tatizo la *mind set*, akili zetu Wazanzibari wengi ni kununua na kuuza, akili za *investment* hazipo na mimi ndio maana namshukuru sana Mhe. Said Salum Bakhresa amejitahidi sana kuonesha kwamba tunaweza tukafanya *investment* wenyewe na *potential* la *investment* ni kubwa katika hii nchi, hatujaitumia vizuri tu.

Mhe. Spika, nimezungumza hapa *Deep Sea Fishing.* Leo katika Bahari Kuu kuna meli 84 zinazovua, meli tatu tu ndio zinapepea bendera ya Tanzania na meli zote zilizobaki zinapepea bendera ya kigeni. Nimekaa na wa-*authority* nasema hii haiwezekani, wakasema hapana tumejitahidi wame-*train* vijana zaidi 30 sasa hivi ili na wao waweze kuingia katika uvuvi wa Bahari Kuu, lakini wakishafanya hayo wanahitaji chombo, chombo ili kipate lazima uhitaji pesa, lazima uende Benki ukapate pesa.

Kwa hivyo, moja ni kweli tunahitaji kuwa na chombo hicho, lakini tunahitaji kuwa na mitaji ya kuendelea. Nataka nimuombe kabisa rafiki yangu, swahiba wangu mkubwa na waziri mwenzangu Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, tunakosa mapato ya meli za kigeni haziji kufunga gati hapa, eti, kwa sababu pale bandarini hatuna *plug* za kuweza kufanya hizi *refrigerator*

containers kuweza kuzi-*plug in*. Hiyo ndio sababu yenyewe, kaisimamie wiki hii tupate *plug*.

Mhe. Spika, sheria inasema meli zote zinazokuja kuvua Tanzania lazima zije, aidha, Bandari ya Zanzibar, ya Mtwara, Dar-es-Salaam, tuzikague ili tujue wanachovua na sisi tupate mapato na mapato yanatokana katika maeneo matano yafuatayo:

La kwanza, meli ikija ikifunga gati pale watu wa *harbor* wanapata mapato, tunapata kuwapa maji, tunapata kuwapa mafuta, tunapata kuwapa chakula, lakini tunakuwa wafanyakazi wetu wanaingia na vijana wetu wanapata kazi ndani ya meli hiyo. *Five areas*, wakitoka hapa wakishavua wanakwenda *low Seychelles* au Mauritius na kwengineko, eti, kwa sababu sisi hatuna *plug* za kutosha kwenye bandari zetu. Mwanzo walikuwa wakinambia lazima waijenge gati, sio kweli, *sea plug* za ku-*feed* ile *electricity* ya kutosha kwenye zile *refrigerator container* ili ziwe *minus 16* ukishafanya hiyo tayari. Sheria ipo hatuhitaji kubadilisha.

Jengine ninaloliomba Baraza hili ile sheria bahati mbaya hamjaja kuridhiwa ndani ya Baraza. Nalo hilo ni tatizo lazima tulitatue sisi na Waheshimiwa Wajumbe, kwa pamoja. Tunalifanyia kazi na wanasheria, tutakaa na Mwanasheria Mkuu ili tulimalizie hilo ili tuone kama tumepata sheria nzuri, lakini kwa kuanzia sasa hivi kwa sababu meli zipo 84 zinavua lazima tuhakikishe wanakuja hapa na hizi huduma tano zipatikane. Sasa huduma tano muhimu wapi?

Umuhimu wa hizi huduma tano, lazima uwe na kampuni yenye uwezo wa kupeleka chakula kinachotakiwa, maana yake tumezungumza hapa tuna kila kitu, kaangalie zile ndizi zinazozalishwa zina makovu matupu huwezi kusafirisha zile, embe tunazozalisha zina kovu huwezi kuzisafirisha. Kwa hivyo, suala la *packing* na *management* ya *crops is very important* hasa kwenye hizi meli, ukawapa kitu kibovu hawanunui tena mara ya pili. Hilo la kwanza.

La pili, lazima kuwe na kampuni inayoweza ku-*supply* maji vizuri, mafuta na wafanyakazi ambao ni *skilled* ili waweze kuingia katika zile meli. Tumeelewana ee? Hili litasaidia kuweza kuongeza mapato, lakini ziko meli 84 sasa hivi, tatu ni za Zanzibar na sasa hivi ninavyosema kuna *application* ya meli 15 nyengine zinataka kuja hapa kuingia kwenye *Deep Sea Fishing* lakini nimewaambia lazima wawe *registered* na wa-*fly Tanzania flag*. Lazima waje lakini lazima wa-*fly Tanzania flag*, mambo ya bendera za nje hizi habari yake imekwisha, *you need your support*, lakini sisi tumejipanga vizuri kabisa

kuhakikisha kila rasilimali tunaweza kuitumia kwa ajili ya manufaa ya Wazanzibari na Watanzania tutalifanya kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimechukua muda wako mrefu, najua Waheshimiwa Wawakilishi, wamesema mambo mengi, mengine ni ya ushauri, nawahakikishia kabisa hakuna ambalo hatukulifanyia kazi na tutalitolea taarifa ndani ya Baraza hili, kwamba hili mlitupa kwenye bajeti tumekwenda kulifanyia kazi hali yake ni hii. Nasema haya ya jumla kwa sababu naona ndio mambo ya mshiko ya msingi ambayo wamedai, la kama watakuwa na hoja moja moja, najua mzee wangu Mhe. Hamza Hassan Juma, pale amesharidhika, basi naona tumemaliza shughuli.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja, ahsante sana.*(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa namna ulivyojumuisha na mara nyingi unakuwa unapata hii *standing ovation* ambayo inatupa matumaini kwamba labda hii kazi itakayofuata baadae itakuwa nyepesi zaidi kwa sababu mchango ulikuwa mzuri sana.

Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, naomba kwanza sasa basi tuiamue hii hoja, naomba kuwahoji. Wale wote wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali Hotuba ya Bajeti Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

KIFUNGU L01 WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI

Kifungu Ll0101	Ofisi Kuu Pemba	555,420,000
Kifungu L0104	Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka	881,979,000
Kifungu L0108	Idara ya Kilimo	65,000,000
Kifungu L0109	Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani	70,000,000
Kifungu L0110	Idara ya Maendeleo ya Mifugo	59,200,000

Kifungu L0111	Idara ya Maendeleo ya Uvuvi	1,186,000,000
	Jumla Kuu	**2,817,599,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu na vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU PL0101 Programu kuu ya maendeleo ya Kilimo

Kifungu SL010101

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante, Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, umechangia?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimechangia, nisingesimama. Mhe. Mwenyekiti, mwezi wa Ramadhani huu sijalewa mimi, nisingesimama kama sijachangia.

Mhe. Mwenyekiti: Yaani, umechangia vipi, kwa sababu sijakusikia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimechangia kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa maandishi?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naam.

Mhe. Mwenyekiti: Haya lete hoja yako sasa. Endelea, lete hoja.Usianze kubishane.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hakuna kubishana, kufahamishana tu kwa kujua Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Lete hoja Mheshimiwa, usitupoteze wakati.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja kuna mradi wa umwanguliaji maji kijiji cha Muyuni na sio pesa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ni msaada kutoka Japan muda mrefu. Haujasaidia kutatua matatizo na hakuna kinachoendelea, msaada huu alifanya aliekuwa Mbunge kwa kushirikiana na Mwakilishi ambaye sasa uko nchini Kweit, namshukuru sana. Na hoja nyengine...

Mhe. Mwenyekiti: Hoja moja tu Mheshimiwa. Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni kweli anayosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwamba huu mradi ulisimama kwa sababu hauko kwenye utaratibu wetu wa kiserikali. Sasa hivi tumeurudisha na tunaufanyia kazi na nakuhakikisha kabisa hapa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, huu ni mwaka wa tatu, sijui kazi gani inayofanywa. Nitarajie nini mie au miaka mitatu ndio anayosema ikiwa mpunga haujapatikana ataachia madaraka ndio haya tujue. Lakini sasa ni mwaka wa tatu, sijui kazi gani inayofanywa Mheshimiwa, au ndio hiyo anayosema mchele hautotoka nje ndio hii nusu miaka mitatu mingine sawa. Lakini naomba nipe jawabu wananchi wa Jimbo la Muyuni wanataka kujua jawabu hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa tuendelee au vipi?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sijasema tuendele Mhe. Mwenyekiti, huu ni mwaka wa tatu ananambia nisubiri, sijui nisubiri mpaka muda gani?

Mhe. Mwenyekiti: Umesemaje sawa. Tuendelee au?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahaa!

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nakuomba kabisa uchukuwe ahadi yangu kwamba tutalifuatilia hili jambo na wewe tutakushirikisha katika hili. Nakuhakikishia kabisa tutakushirikisha, tutakuwa pamoja na utaona hatua tunazozichukuwa na utaridhika nazo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, huu mradi ukifika pahali unakufa kabisa na zile pesa zinapotea kabisa zinakuwa muflis.

Mhe. Mwenyekiti: Sijakufahamu Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Huu mradi ukifika pahali ukiwa haujafanyika unakufa na pesa zinakuwa muflis. Sasa sijui kama atakwenda leo au vipi?

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, amekuahidi na amefunga na yeye vile vile, naomba upoke kama unavyotoa wewe kwamba, husemi uongo umefunga na wengine ni hivyo hivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa, huu ni muda mrefu, mimi wala sina matatizo, huu mwezi mtukufu wa Ramadhani. Huu mradi ukishafika muda unakufa na zile pesa tutazikosa.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri keshasikia Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mheshimiwa, tena namuongezea tu tumefanya, utafiti kile kisima kimekuwa na matatizo ya chumvi, ndio maana tunaendelea kufanyakazi kwa kushikiriana kwa pamoja na kwamba pamoja na kuwa mradi huu hauko katika serikari uko kwenye serikali, bado sisi tumeona ni *input* iko pale tutawasaidia wakulima lazima tukifanyie kazi. Namuhakikishia kabisa tutaufanyia kazi tu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa Mwenyekiti, panapo chumvi lile eneo ni kubwa, kukaa pale eneo lile lote litakuwa na chumvi. Lakini tukijenga hizi hoja lazima tujenge vizuri kwa sababu wananchi wanakisikiliza hichi chombo, panapo hoja na panapo chumvi ni pahali pengine, lile eneo ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, waziri amekuahidi kwamba uende ukaonane nae ili mshirikiane kuhisia na suala hili na wananchi wako pia wamesikia hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Wale si wananchi wangu, mimi jimbo langu la Paje liko Makunduchi Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Waheshimiwa, nitawapa nafasi watu wengine wawili. Nitampa nafasi Mheshimiwa Mwakilishi wa Bububu na Mhe. Miraji. Hoja moja moja tafadhali.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, jana nilizungumzia suala la *TASAF II* ambalo limetengeneza bonde la umwangiliaji maji Bumbwisudi, lakini kwa bahati mbaya mpaka leo miundombinu tayari lakini umeme haujafikishwa na nilimuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa aniambie, lini ataufikisha umeme kwenye eneo hilo la Bumbwisudi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nalifahamu hilo suala, tumeshalipa baadhi ya fedha kwa wenzetu wa Shirika la Umeme, tatizo pale hasa ni *high tension* ya umeme, wanalishughulikia na fedha tumeshatoa kidogo na bajeti hii *Inshaallah*, tutaweza kulimaliza.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia kwa maandishi nilimuuliza Mhe. Waziri, kuna mradi mkubwa wa umwagiliaji wa serikali na serikali iliitisha tenda katika huu mradi na wazabuni wakajaza. Sasa nataka kujua hatua gani zilizofikiwa na serikali hadi hivi sasa na mradi huu unataka kupata pesa kupitia *Exim Bank.* Nilikuwa nataka maelezo ya huu mradi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Nafikiri Mhe. Mwenyekiti, anazungumzia mradi ambayo ni upande na *Exim Bank* ya Korea, kama ni huo basi *process* inaendelea, ni kweli tenda ilitangazwa kwa bahati mbaya sana aliejibu ni mtu mmoja na sheria za tenda yetu hairuhusu. Ikabidi serikali ikaamua tu-*retender again* ili kupata watu ambao wanabidi kwenye mradi huu. Tunaendelea na hiyo *process* sasa hivi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Nashukuru sana kwa majibu ya Mhe. Waziri, lakini nataka atuhakikishie kwa sababu tulipoomba huu mradi kulikuwa kuna wakati fulani kwa hizi pesa zinakwenda na muda. Sasa ni lini serikali itatoa hiyo tenda nyengine ili kuweza kuharakisha upatikanaji wa hizi fedha. Sasa mara nyingi fedha hizi zinavyotoka kwa wenzetu hawa wanakuwa wanatoa na muda. Nilikuwa nataka kujua ni lini serikali itaanza *process* upya.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza hizi fedha za mkopo, si pesa za kugaiwa, ni za mkopo, serikali imekopa 50 milioni dola la kwanza.

Pili, pamoja na yote lazima zile taratibu za kisheria za *procurement* zifanyike na ndio maana Baraza la Mapinduzi likaamua kabisa baada ya kupitia *data* zote tukaamua kwanza turudi kwenye *retendering*. Kwa hivyo, itakapotakiwa serikali kutoa mchango wake baada ya tenda kumalizika tutafanya hivyo. Tunahitaji hizi hekta 1600 zimwagiliwe maji zote.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana na majibu wa Mhe. Waziri na naomba tuendelee.

Kifungu SL010101 Programu ndogo ya Umwagiliaji maji 1,068,660,000
Kifungu SL 010102

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Waziri, amejitahidi sana na kwa kweli majibu aliyoyatoa inaonesha hata wiki ya kufika ofisini hajaa ofisini, kama alivyokuwa Maalim Rashid jana alipokuwa akijibu masuala yake, nafikiri na Waziri wa Kilimo na yeye anajitahidi, hongera sana.

Mhe. Mwenyekiti, Niliuliza suala zima mradi wa mpunga wa Nerika, nashukuru sana kwa *commitment* ya Mhe. Waziri kwamba, hii yeye ametuahidi ndani ya miaka mitatu. Tatizo la mchele kwa Zanzibar litakuwa historia. Mimi naomba taasisi zote zinazohusika zimpe *support,* tuache siasa tupige kazi tupate kula mchele.

Sasa nilikuwa tu nataka maelezo, hebu huu mradi wa Nerika kwa sababu aliouzungumza yeye sio katika mpango wa Nerika, naamini toka kukaa ofisini amejaribu kuwauliza wataalamu wake...

Mhe. Mwenyekiti: Hebu jaribu kwenda katika suala.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Nataka nipate hatua ya huu mradi wa Nerika, yaani mpunga wa Nerika au ule tunauacha umefeli, tunakwenda katika programu nyengine. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni kweli mbegu ya Nerika ililetwa ikafanyiwa utafiti, mambo matatu yaligundulikana;

Kwanza ukitaka kuutwanga ule mpunga ni mgunu sana. Lakini pili kuonekana kama haukubali baadhi ya maeneo. Kwa hiyo, kilichofanyika ni kwamba kuendelea na utafiti kuona kwamba pamoja na uzuri wa mbegu yenyewe, pamoja na kwamba mnasema hauna ladha sana na kadhika, maana yake hili ni tatizo, unajua sisi hapa tumezoea chakula ambacho kina harufu, pamoja na kwamba tunakula mapembe hayana harufu.

Kwa hiyo, utafiti umeendelea na ndio maana sasa hivi tuna mbegu nyengine ambazo tunaendelea na utafiti, nakuhakikishieni Waheshimiwa, wakulima mara hii watapata mbegu ambayo wanaihitaji na hii tutaendelea nayo katika utafiti. Lakini matatizo hayo matatu ambayo nimeyaeleza. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ni yale yale niliyoyasema Mhe. Waziri, kila unalomuuliza keshalifanyia kazi. Lakini tu nilikuwa namwambia kwamba, kumpiga maswala mwalimu wako inategemea maswala yenyewe, maana yake Mwalimu Haroun Ali Suleiman alinitizama sana hapa, tuendelee.

Kifungu SL010102	Programu ndogo ya Utafiti na mafunzo ya kilimo	1,820,158,000

Kifungu SL 010103 Programu ya maendeleo ya huduma
za kilimo na karakana ya matreka

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, jana nilimuuliza kutoka mwaka 2010 mpaka 2015 ni matrekta mangapi yaliyoagizwa na mangapi yanafanya kazi.

Jengine inasemekana kwamba kuna vipuri ambavyo vimenunuliwa lakini vipuri hivyo haviafikiani na hayo matrekta ambayo yapo yalioharibika. Je, fedha hizi ambazo zimenunuliwa vipuri ni za tajiri au serikali na kama ni serikali aliyekwenda kununua hivi vipuri anachukuliwa hatua gani.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alivyosema Mheshimiwa, serikali imekuwa imeagizia trekta tumekuwa na matrekta tumechukuwa SUMA JKT, matrekta 40 na sasa hivi idadi ya matrekta ambayo ni mazima kabisa yanafanyakazi ni matrekta 28 na mengine ambayo yanahitaji kufufuliwa upya.

Lakini la pili, niseme tu kwamba vipuri vilivyoletwa viliingizwa kwenye kutengeza matrekta na ndio haya ambayo tumeyafufua. Lakini ni kweli kabisa matrekta mengine yanahitaji vipuri na katika bajeti hii ndio maana tumeomba fedha ili kumalizia hayo matrekta mengine ambayo yapo.
Idadi hasa halisi ya matarekta ambayo tunahitaji kukamilisha kilimo kiwe kizuri ni matrekta 80 kwa sasa tuna matrekta 42 pamoja na hayo mabovu unayoyasema.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, bado nina wasi wasi na jibu la Mhe. Waziri, bado ndani ya karakana zake kuna vipuri ambavyo vimeletwa na havifai kutia kwenye hayo matrekta.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sina taarifa ya vipuri ambavyo havifai, lakini nitafuatilia hilo suala lakini *so far* mpaka nimetembelea kwenye karakana pale mafundi wangu walikuwa wanalia kwamba hawana vipuri ili waweze kufufua matrekta. Nikawaambia tusubiri bajeti ipite ili tuweze kufufua matrekta ambayo yamebaki.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu SL 010103	Programu ya maendeleo ya huduma za kilimo na karakana ya matreka	3,382,472,000
Kifungu SL010104	Program...	

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, nyanyuka, nani Mhe. Panya au sie, haya.

Mhe. Panya Ali Abdalla Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya na kweli anatupa matumaini makubwa na *Inshaalla* Mwenyezi Mungu atamsaidia. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kujau kwenye kifungu hichi cha uhakika wa chakula na lishe kwa sababu tulipitisha sheria hapa ambayo inahusu uhakika wa chakula na lishe na Mheshimiwa, kwa jinsi alivyopania nilitaka kujua.

Je, yale ambayo yamepangwa katika wizara yake ameshayakamilisha kwa kuona anajipanga vizuri ili kupata utekelezaji mzuri. Kwa sababu ndani ya kifungu cha sheria hiyo namba 17, kulitakiwa kuundwa kamati ndani Shehia husika ambazo zipewe majukumu. Halafu kuna kifungu cha 18 hivyo hivyo kilipewa majukumu na kifungu cha 19 chenyewe ambacho kiliitaka wizara hiyo hiyo iwe na mpango kazi wake na iwezo kuutekeleza.

Lakini kuna kifungu cha 21 mpaka 23 ambacho kilikuwa kimepangiwa katika mawizara mengine ndani ya wizara yake lakini kuna mawizara yalihusishwa ambayo yakapewa majukumu yale. Nilitaka kujua je...

Mhe. Mwenyekiti: Swali lako Mheshimiwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Swali langu nilitaka kujua kwanza hizo kamati kwenye hizo Wilaya zimeshaundwa au bado na kama hazijaundwa ni vipi ataweza kutekelezeka huu mpango wa uhakika wa chakula la lishe. Lakini pia katika wizara nazo zilipewa majukumu yake, ninataka kujua na ikiwemo...

Mhe.Mwenyekiti: Mheshimiwa, mruhusu ajibu basi swali lako, halafu uulize hilo jengine kama lipo.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Eeh!

Mhe. Mwenyekiti: Ninaona kama una maswali zaidi ya moja. Hoja ni moja, tayari. Mhe. Waziri, majibu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza Kamati ile ya Kitaifa imeshaundwa na sasa hivi wapo kwenye *process* wa kuweza hizo Kamati za Wilaya kama alivyosema. Lakini ninasema suala la chakula ni letu sote, si la sheria wala siyo la Kamati.

Sisi sote tukubali kwamba tunahitaji kuzalisha, kila mwenye fursa ya kuzalisha azalishe. Na muhimu nafasi ya kupata akiba ya ziada aweke akiba.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Panya.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru Mhe. Waziri, kwa majibu yake na anavyotupa moyo sitaki niendelee kumuuliza tena nyengine, ninataka nione tutafuatilia na yeye mwenyewe tunajua ni mfuatiliaji mkubwa. *Inshaallah,* tuendelee tutasaidiana juu ya kadhia hii. (*Makofi*)

Kifungu F

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe.Mwenyekiti, embe ni chakula. Niliuliza nilipokuwa ninachangia bajeti, nilisema kwamba embe zina matatizo ya wadudu. Sasa ana mkakati gani wa kuweza kuzitibu hizo embe ziondokane na matatizo ya kuwa na wadudu Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe.Mwenyekiti. Ni kweli kabisa ameuliza Mhe. Hassan, na sisi katika kufuatilia kwenye wizara, kwanza tuliangalia hii taaluma tuliyoitoa juu ya kupambana na hawa inzi waharibifu, je, inafanya kazi au haifanyi kazi.

Tukagundua kwanza kuna mambo matatu lazima tuyafanye:-

1. Kuendeleza taaluma yenyewe,
2. Kuleta ile dawa ya kupambana na wadudu wenyewe,na
3. Jukumu la kutumia ile dawa ni la wakulima wenyewe.

Kwa sababu mtu anategemea serikali imfanyie kila kitu. Sasa mimi ninakuhakikishia kabisa tutahakikisha dawa inapatikana, lakini tunataka na wakulima wenyewe yule mwenye uwezo wa kufanya afanye. Tunahitaji kufungua maduka ya vifaa hivi vya kilimo ili watu waweze kujinunua wenyewe. Ninawashukuru sana wafugaji hawa wa mifugo ya ng'ombe na mbuzi, wao ndio wanatafuta madawa, wanatafuta madaktari, lakini wakulima wengine mpaka uwafuate wewe mwenyewe. Sasa ninasema lazima tujenge utaratibu wa *ownership,* kwamba hichi ni kitu cha kwangu, lazima nikitunze. Ninamuhakikishia kabisa dawa ya kupambana na wadudu wale itapatikana ya kutosha kabisa itaifuatilia. Lakini ninataka tupate ushirikiano wa pande zote mbili zinazohusika.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika na majibu. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee hivyo hivyo tuweze kupata dawa jamaa zangu wa Mchangani embe zao ziwe salama. Ninaomba tuendelee.

Kifungu SL 010104	Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe	Shs.344,454,000/-
Jumla Kuu		**Shs.6,615,744,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko)

Kifungu PL 0102

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe.Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia Mhe.Waziri, ninamshukuru alinijibu na ile hoja niliyokuwa nimeijenga na yeye pia alikuwa imemuuma kuhusu suala la ukataji wa minazi. Na alitwambia alimfuata yule mwekezaji ambaye ana kiwanda cha minazi na alisema kwamba mnazi ukishafika miaka mia, kwa vyovyote inabidi ukatwe kwa mujibu wa sheria.

Lakini tatizo lililokuwepo Mhe. Mwenyekiti, sasa minazi ambayo hata haijafika hiyo miaka mia. Mimi mwenyewe Mhe.Mwenyekiti, ni shahidi. Nina kijishamba changu kule Kiboje minazi imekuja imekatwa na minazi mwenyewe nilikuwa ninaangua nazi.

Sasa nilishauri serikali kupitia Waziri labda tungelizuia kwanza *at least* tukafanya hiyo tathmini, halafu ikawa *identified* hiyo minazi au maeneo ambayo hiyo minazi inapaswa kukatwa, halafu baadae kama itakuwa ipo ya miaka mia ithibitishwe na Masheha, halafu tuendele.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa, lakini kabla sijamruhusu, nitamruhusu Mhe. Waziri, ajibu. Lakini hapo ulipogonga buti ni hili kubwa. Kwa hivyo, kwenye ile programu yenyewe ndogo ile SL 010201 utajibiwa suala lako. Tuendelee.

Kifungu PL 010201	Programu Kuu ya Maendeleo ya Raslimali za Mali Zisizorejesheka	Shs.96,711,000/-

Mhe. Hamza Hassan Juma: Naomba nijibiwe.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa ndiyo ninampa Mhe. Waziri, ajibu hilo swali lako. Mhe. Waziri, majibu tafadhali.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana. Mhe.Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na wewe kwamba kunahitajika kufanyika utafiti wa kina. Ila ninashangaa na ninashauri kwamba tukisitisha hafla, maana yake unakata ajira, unakata kodi na unakata kila kitu. Kwa sababu hili jambo lilitakiwa serikali iamuwe kwa jumla, hatuwezi tukaliamua hapa sasa hivi. Serikali itaweza kuamua tu pale ambapo tumefanya utafiti wa kutosha kuona zile athari zote zilizotokea na hatua za pili tunazochukuwa.

Kwa mfano, nilipokuwa ninazungumza na yule mtumiaji mkubwa akasema kwa nini kwa sababu mashamba haya ya mpira yameshakomaa sasa hivi, hayatoi tena mpira tena wa kutosha. Kwa nini musiniruhusu mimi nikaanza kuvuna kule na nikapanda na minazi. Sasa hilo siwezi kuliamua peke yangu lazima tulipeleke kwenye Baraza la Mapinduzi, liamuliwe halafu tulipeleke kwa wananchi.

Ninakubaliana tufanye utafiti ili tuiwezeshe serikali sasa kufanya maamuzi ya pamoja. Ninakubalana kabisa na hoja yako, lakini lazima twende kwenye *processes* za serikali, siyo kuamua hapa hivi sasa ili hatimaye tupate maamuzi ya pamoja. Hili nitalifuatilia Mhe. Hamza.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa kauli ya Mhe. Waziri. Lakini labda mimi nilikuwa nina ushauri.

Labda ili ajira isikatike na ule uwekezaji uendelee lakini uwekezaji uwe na manufaa na sisi. Kwa nini sasa hivi wizara itoe toleo kwamba mnazi wowote utakaokatwa lazima kipatikane kibali cha Sheha. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti,...

Wajumbe: Aaah! siyo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Yaani ninakusudia kibali cha Sheha ili kuthibitisha ule umri wa mnazi, siyo kwamba mtu akishakuwa na kibali cha Sheha, maana yake tunajua tena umeshakuwa na kibali cha Sheha itakuwa ruhusa, aah! Ili kujiridhisha kwamba huu mnazi unaokatwa tayari umefika umri wa kukatwa.Yaani hiyo ndiyo hoja yangu nilipokusudia. Maana Waheshimiwa Wajumbe, tayari wameshataka kuniparamia huku.

Mhe. Mwenyekiti: Eeh! Mheshimiwa, ukumbi wote naona umebadilika baada ya kutaja kwamba kibali cha Sheha kiruhusu mpaka ukakatwe mnazi. Mhe. Waziri tafadhali.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Ninamshukuru sana Mhe. Hamza. Mimi ninasema tumshukuru ameonesha *concern* kwamba, hili jambo ni jambo kubwa linaathiri nchi. Tunakushukuru sana na Waheshimiwa muendelee na *spirit* hiyo ya kwamba tunahitaji kuona uzito wa jambo lenyewe kwamba miti inakatwa na kadhalika.

Sasa ninasema kwa utaratibu wetu ni kwamba huruhusiwi kukata mti wowote mpaka ipate idhini na kibali kutoka kwanza Idara yenyewe ya Misitu, halafu hicho kibali unakichukua kwenda nacho kwa Sheha ili kumuonesha Sheha mimi nimepata kibali Wizara kwamba niukate huu mti. Tatizo tulililonalo ninakubaliana na wewe kabisa kuna haja ya hawa watu wanaokata hawana kibali, lazima tuwakamate na tuwashitaki kwa sababu wanavunja sheria ya nchi. (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninafikiri hawa wataalamu wetu, yaani watu wa Misitu wajaribu zaidi kufuatilia. Kwa sababu mimi kwa utafiti wangu mdogo nilioufanya, wengi wao hawendi kukata hivyo vibali. Kwa hivyo, ina maana hilo ni kosa kubwa. Lakini kimsingi hiyo ni kazi ambayo ninamwambia Mhe. Waziri, aifanye na ninaamini ataifanya na tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa ninachangia hotuba hii ya bajeti nilisema kwamba kumetoka tamko kwamba minazi isikatwe. Lakini minazi ninahisi kupitia tamko hilo kama imezidishwa kasi ya katwa.

Sasa ninauliza ni watu wangapi wamefikishwa Mahakamani na kuhukumiwa?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ninataka niwe mkweli, sina *data* hapa sasa hivi, nitazitafuta baadae.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, umpe muda ninafikiri akupe hiyo takwimu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ninashukuru, lakini nitaomba aniletee kwa maandishi Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, tafadhali.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, tunaendelea.

Kifungu PL 010201	Programu Kuu ya Maendeleo ya Raslimali za Mali Zisizorejesheka	Shs.96,711,000/-
Kifungu ASL 010202	Programu Ndogo ya Maendeleo ya Misitu	

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ninasemaje kwa ruhusa yako na mimi nilipokuwa nichangia nilizungumzia suala la *Eco-tourism* katika misitu. Na suala hili Mhe. Waziri, anyanyuke anipe majibu kamili kwa sababu hili ni jambo jipya. Ninachokiomba hii misitu ni hifadhi, ni raslimali yetu ya nchi. Tunapotaka kuifungua kuitumia kwa ajili ya *Eco-tourism.* Isejeikafanywa kama Forodhani kila mmoja anaingia, tukajifunze kwa wengine tuelewe na iwekwe katika hifadhi ya kimataifa.

Ninatumai serikali yote imenisikia na ninazungumza hasa misitu ya Jozani pamoja na Ngezi.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana ninaomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Kifungu ASL 010202	Programu Ndogo ya Maendeleo ya Misitu	Shs.1,570,725,000/-

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichangia kwenye hotuba ya Mhe. Waziri, lakini ninaamini binadamu kasahau. Nilizungumza suala la kuibiwa kwa kima pungu pamoja na kuibiwa kwa makobe wale wadogo kwenye *Prisoner Islander.*

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kujua wizara yako Mhe. Waziri, ina taarifa gani ya kuibiwa kwa hawa kobe na watu wangapi wameshakamatwa waliiba hawa kobe na kima pungu na kupelekwa nchi za nje.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nishukuru wale makobe walikuwepo chini ya Wizara ya Fedha, na sasa hivi tunafanya njia ya kuweza kuwahamisha kuwarudisha kwenye wizara yetu. Na tumeshakaa na Wizara kuweza kuzungumza. Hilo ni kwanza.

La kima pungu sina taarifa ya kuibiwa mpaka sasa. Lakini kama yeye ana taarifa nitamuomba anipatie na ninaamini tutalifanyia kazi pamoja

tutashirikiane na vyombo vinavyohusika, hao watu husika wakamatwe. (*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi na jibu lake, lakini nitashirikiana naye kuhakikisha tunashirikiana kwenye kukamata hivi vitu. Lakini mimi kama nilivyomueleza na ninaeleza kidogo.

Nilienda nchi fulani nikakuta *red monkey*s wa Zanzibar nimewakuta huko kwenye *zoo*.

Mhe. Mwenyekiti: Wapi?

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Aah! Nchi ambayo niliwahi kwenda. Sasa nitakaa naye nitashauriane naye kumsaidia. Ahsante sna Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu ASL 010202	Programu Ndogo ya Maendeleo ya Misitu	Shs.1,570,725,000/-
Kifungu PL 0103	Programu Kuu ya Maendeleo ya Mifugo	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala la kutokuridhika kwangu, kwanza uingizwaji wa fedha katika Idara ya Mifugo, yaani fungu lipo dogo ni asilimia 18, lakini vile vile namna ya kuwahifadhi wafugaji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, nimemsikia vizuri alipokuwa akijibu, katoa ufafanuzi mzuri sana. Na katika ufafanuzi alioutoa aliwahi kuzungumzia suala la hoja ya mwekezaji Ndugu Bakheressa alipotaka kuwekeza kwenye shamba la Bambi tulikataa hapa Barazani. Na mmoja katika waliokataa ilikuwa ni mimi na nilikataa kwa sababu ile ni sehemu ya *fertile area*, pale watu wanalima viazi vikuu na nini katika mwezi wa Ramadhani tunafaidika.

Na niliwashauri waende katika shamba lile la ng'ombe pale Pemba wanaita Chamanangwe. Kwa hivyo, ina maana pale kipindi kile sasa ile hoja yangu ilionekana siyo ya msingi na mimi nikasema kwa kwenda kuwaondoa wakulima wa Bambi pale kwa mtu kufuga ng'ombe kwa kweli itakuwa siyo sahihi. Hivyo, bado ile hoja yake ya kusema kwamba wanakwenda kufuga kule Chamanangwe, kwa kweli ninaiunga mkono sana.

Lakini hoja yangu zaidi ipo hapa hawa kuku wa *perdue.* Mhe. Mwenyekiti, kuku wa *perdue* ninamshukuru sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri. amemuona yule mwekezaji anayeleta wale kuku na akajaribu kushauriana naye, kampa *condition* nyingi. Sasa hapa tunapitisha bajeti ya maendeleo ya mifugo, bado wafugaji wadogo wadogo hawa tumewafikiria kitu gani.

Mimi nina ushauri kwamba huyu mwekezaji ajaribu ku-*invest* zaidi, aidha. kama yeye au atafutwe mwekezaji katika kuweka hicho kiwanda cha chakula cha kuku, ili hawa wafugaji waweze kufuga kuku kwenye gharama nafuu.

Sasa hebu hili katika hichi kipindi cha mpito ili na wafugaji wetu pale tuwaridhishe. Hebu anipe ile mipango yake nione, halafu baadae nitamfuata ofisini kwa sababu hawa wafugaji wapo wengi sana.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niseme tu kwamba ukitaka mahitaji ya kiwanda kile cha Bakheressa cha lita zisizopungua arobaini na tano elfu kwa siku unahitaji shamba kubwa kidogo.

Pili, mwekezaji yeyote lazima ataangalia *cost of productio*n. Akiwekeza Pemba, maana yake unamuongezea gharama za kuleta maziwa na kuja kuuzia hapa. Inawezekana akawa nini...

Labda tungekaa tukazungumza tu kama kuna *alternative* ya kuwasaidia wakulima namna gani tunaweza kuwasaidia kwa wepesi wakulima hili shamba lipatikane lifanye kazi. Kwa sababu ukenda kuangalia pengine lile shamba walilonalo ambapo ni *fertile* kama unavyosema, lakini *production per unit* inayofanyika pale ni kidogo sana. Na *impact* itakayopatikana kwa kuwekwa ng'ombe pale akapata maziwa ajira ikaongezeka marudufu sana kwenye kiwanda na kiwanda kile kitakuwa kinatoa maziwa kutokana na hichi, kodi yake itakuwa ni kubwa sana inayopata serikali.

Sasa lazima uziangalie hizi *mutiples effects economy* ili umwambie mtu kafanye jambo fulani. Yeye ameshafanya *studies* anajua. Mimi ninafikiri tungekaa tukaliangalia.

Lakini cha msingi ulichokisema wale watu tunawasaidiaje? Mimi hilo ninaona ndiyo jambo la kuzingatia kama serikali. Ndiyo maana sisi tuna programu na hawa wawekezaji wote kwamba chochote wakakachowekeza kuanzia sasa, lazima tuone programu ya kiasi gani tunawasaidia wazawa wa ndani, kwamba

usije tu wewe mwenyewe ukawekeza halafu ukaondoka. Lazima tuhakikishe na wazawa wenyewe wameshiriki katika uwekezaji.

Kwa hivyo, tunazo programu tatu; Programu moja inatokana na wawekezaji, programu ya pili tunayo ya *FAO* na programu ya tatu tunaitumia kwa Chuo chetu cha Kizimbani ili kuwasaidia hawa wafugaji, wakulima na kadhalika, kuwawezesha sasa na wao wenyewe katika jumuiya zao waweze kupata mikopo.

Na ninashukuru sana nilipozungumza Mhe. Waziri Castico amesema katika ule mfuko wa ujasiriamali atakuwa tayari vile vile kuwasaidia vikundi kama hivi. Mimi ninafikiri tukiendelea na hiyo na kuwabana hawa wawekezaji kuwashirikisha ndugu zetu, ninafikiri tutapiga hatua nzuri sana. Lakini ninakubaliana na wewe kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua tatizo la wananchi wetu sasa hivi, unajua sasa hivi wanasema; "Ukigongwa na nyoka, ukiona unyasi unashituka" kwamba kuna wananchi walipewa maneno mazuri sana katika maeneo ya uwekezaji. Wakatoa maeneo yao, mutapata ajira, mutapata nini, matokezea yake baadae ngoma ikaja ikageuka ajira zile wamezikosa. Ndiyo maana watu wa Bambi walituita sisi kama Kamati, tukenda walikuwa wakali kama moto na ndiyo maana tukajaribu kujenga hiyo hoja.

Lakini bado mimi ninafikiri Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, Pangeni tunalo shamba sisi la serikali na hapa Unguja bado yapo mashamba ambayo hayatomuingizia *cost* ya kusafirisha haya maziwa. Hebu tujaribu kuangalia haya maeneo mengine ya mifugo. Kwa sababu sisi tunataka kumuona yule mwekezaji anafanya *production* na vijana wetu wapata ajira. Lakini vile vile tusiwaumize wengine kwa kumuinua mwengine vile vile.

Hebu haya mashamba mengine yalikuwepo hapa Zanzibar. Kwa mfano kama Upenja, haya mumejaribu kuyafanyia utafiti.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, tutafanya utafiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu ASL 010202	Programu Ndogo ya Maendeleo ya Misitu	Shs.1,570,725,000/-
Kifungu SL 010301	Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo	Shs.1,633,529,000/-
Kifungu SL 010302	Programu Ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo	Shs. 127,217,000/-
Jumla Kuu		**Shs.1,760,746,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu PL 0104

Mhe. Mwenyekiti: Subiri kwanza Mheshimiwa, tunaendelea, halafu utasimama.

Kifungu PL0104 Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi

Mhe. Mwenyekiti: Sasa ninakupa nafasi Mhe. Jaku Hashim Ayoub, halafu Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mimi nilifikiri unafanya haraka haraka ili tumalize tuondoke.

Lakini nipo katika suala la mwani na Mwenyezi Mungu kanijaalia neema kubwa uingiaji wangu humu kuna milango mitatu ya kuingilia.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, nenda kwenye hoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ni Ikulu au uteuzi wa chama. Nimezungukwa na bahari, lakini miaka mitano yote niliyokuwemo humu ndani, nilikuwa nikisikia tu suala la mwani, mwani. Mwisho, Mhe. Rais, aliagiza wizara nne zikae, nazo ni; Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Biashara na Wizara ya Fedha.

Bado wananchi wanaendelea kuteseka, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa ya mwani. Na ikashauriwa serikali ifanye utafiti. Hatua ile ya kiongozi mkuu wa nchi yetu imefikia wapi?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwenye majumuisho yangu kwamba, kwanza

nataka tumshukuru sana Mhe. Rais, kuwa yeye mwenyewe ameguswa sana. Mhe. Rais katika kuwasaidia wakulima wa mwani aliwahi kutoa vile viboti vidogo vidogo zaidi ya 300 na mara hii amepanga kutoa vyengine 500, hizo ni juhudi peke yake za kuonesha kwamba anathamini sana mchango mkubwa unaotolewa na wakulima wa mwani.

Vile vile, nashukuru serikali hii imejitahidi kukaa na wafanyabiashara wanaosafirisha mwani, ili kujua bei hasa halisi wanayouzia mwani. Mfanyabiashara mmoja alisema wanauza kwa dola 300, kwa hivyo, wanapata kama shilingi 600 kwa kilo. Nikamuuliza kwa nini wakulima mnawapa shilingi 300? Mwengine akaniambia dola 450, nikamwambia hizo maana yake ni shilingi 1,000 kwa nini muwape shilingi 300 wakulima. Kwa hivyo, tukakuta kwamba kuna kama muungano wa aina fulani ya kuwalalia wakulima. Lakini pengine na hawa walioko hapa wana ma-*agents* wao kutoka nje ndio wanaowabana hawa wasafirishaji.

Kwa hivyo, tumejifunza hilo na ndio maana ilikuwa jana tukae kikao na Makamu wa Pili wa Rais, kwa bahati mbaya na kwa sababu ya bajeti hii niliyokuwa nayo mimi kikashindikana kile kikao. Tayari tushatengeneza waraka na nimeshafanya utafiti wa kutosha. ni kiasi gani tunaweza kuwaondoa wakulima wa mwani pale walipo. Kama nilivyosema wako watu si chini ya milioni 118 wanafaidika na sekta ya mwani. Wenyewe wanasema; "mjane halali na njaa", maana yake ni kwamba, ni sekta ambayo imeajiri watu wengi na inahitaji kusaidiwa sana. Lakini kubwa zaidi asilimia 80 ya wakulima wale ni kinamama na wao ndio walijitahidi kuangalia *added value* ya mwani. Ndio zile jana mlizokula kashata, sabuni mkaziona na dawa zile, ni wanawake hawa maskini wamejiunga wenyewe ili kuongeza thamani ya mazao haya. Ndio maana sisi tukafanya utafiti zaidi kwa wenzetu wa nje wanafanyaje katika kuendeleza zao hili.

Mhe. Mwenyekiti, nawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe, sisi tuko *very much concerned* juu ya suala zima la kuwasaidia wakulima wetu wa mwani waondokane na umaskini. Ndio maana tumeshirikisha Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tuone kama *ZSTC* wanaweza kununua karafuu hata bei ikiwa ndogo, kwa nini tusiwa-*save* wakulima wetu wa mwani? Hayo ni mawazo yatakuja lakini baada ya kufanya utafiti wa kutosha kujua kwamba shirika lenyewe haliwezi kupata hasara wala serikali haiwezi kupata hasara. Nia ya serikali katika kipindi kifupi kabisa ni kuondoa tatizo la bei ya mwani kwa wakulima. Nawahakikishieni kabisa liko kwenye *pipe line* serikali iko *serious*, Rais yuko *serious* na ndio maana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndiye mwenyekiti wetu jana tulikuwa tufanye kikao, kutokana na hii

bajeti tumeahirisha, lakini mara tu tukimaliza bajeti hii tutakaa na wakulima wa mwani watapata majibu sahihi juu ya bei yao ya mwani. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, bado, haya ndio majibu ya serikali, Mhe. Waziri, akishakuwepo mbele tena, linalokaa mbele ndio linalojibiwa ndio hilo hilo. Mhe. Mwenyekiti, bado miaka mitano nimedima ndani humu na hii miaka mitano mengine naona kama nitamaliza. Lakini bado suala la mwani limekua kizungumkuti, sijaridhika na jawabu la Mhe. Waziri na Mhe. Rais katika hotuba yake serikali itanunua vihori 500 vya kuchukulia mwani na kusambazwa kwa wakulima wa mwani 3,000 Unguja na Pemba ili kuongoza uzalishaji wa mwani.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais, hii hali anaitaka, anawajali wananchi wake, lakini sasa Waheshimiwa Mawaziri, naona muda mrefu na keshaagiza wizara nne zikae, mpaka muda huu. Kesho nitaambiwa vyengine na keshokutwa nitaambiwa vyengine, haya ndio majibu ya serikali. Nasema utumishi wangu humu ndani ni kwa eneo langu limezungukwa na bahari, sitowafanyia haki. Bado majibu haya mimi hayajaniridhisha na kuna hatari ya kupiga kura leo, mara yangu ya mwanzo itakuwa leo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, majibu ya waziri, nafikiri yalikua yamejitosheleza sana. Mimi nitaomba tupige kura kabisa sasa hivi. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa hili sina mswalie mtume na huu mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio tunapiga kura.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Bora unitoe nje nitoke tu, lakini kwa hili hapana.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana, hapana. Ndio tunapiga kura Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Huu mwezi mtukufu wa Ramadhani, sote tumefunga, sikotayari kwa hili la mwani, nimeshachoka na majawabu ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba ukae Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi bora uchukuwe Askari ndio nitoke, lakini kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, naomba ukae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Siwezi Mheshimiwa. Haiwezekani *yakhe* kwa suala kama hili. Mhe. Rais, keshaangiza kiongozi wa nchi!

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, naomba ukae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Haa! *no, no*. Watu wanateseka nje na sisi tunawajibika kushughulikia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, naomba utoke.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: *Hewallah*.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea. Mhe. Simai Mohammed Said.*(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilikua nina swali dogo kwa Mhe. Waziri. Katika mchango wangu nilizungumzia suala la *Exclusive Economic Zone (EEZ)* na kwa habari tuliokuwanazo ni kwamba kutokana na maelezo aliyozungumza Mhe. Waziri, ni kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi hivi sasa haipati faida yoyote kwenye eneo la *EEZ*, na inavyoelekea hakuna njia ya kuweza sisi kulilinda na tayari nchi nyingi pengine zinapita huko zinavua samaki aina *tuna* au *sour fish* au wanaofanana kwa matani kibao.

Mhe. Mwenyekiti, swali langu ni kwamba kwa nini Mhe. Waziri. kwa kupitia uwezo wake na uzoefu asiishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sisi tukalitumia lile eneo la *EEZ* tuweze kulikodisha kwa nchi ambazo tayari wao wana uzoefu nao kama Mauritous ili tukapata pesa. Je, linawezekana? Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa uzoefu wangu sijakuta nchi inakodisha eneo la mipaka yake kiasi hicho, kwanza hiyo ni mipaka ya nchi na nchi haikodishwi. Hilo la kwanza.

La pili, sio kweli hatufaidiki ukiangalia ile *Deep Sea Fishing Authority* asilimia 40 inapata Zanzibar na asilimia 60 inapata Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndio maana hata kwenye bajeti utakuta tumeweka *one bilion*. Nataka niwaarifu Waheshimiwa Wajumbe, hapa kwamba hiyo *one bilion* tayari tumeshai-*ceiling* kutokana na hivi vikao tulivyokaa hivi sasa. Kwa hivyo, mapato tunapata. Lakini nasema kama kuna maeneo ambayo anafikiri bado

tuyafanyie kazi. Tunamkaribisha tukae ofisini tuzungumze namna gani tuweze kuimarisha udhibiti wa rasilimali zetu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba *record* ikae sawa, sijasema mipaka ya nchi. Eneo la *EEZ* haiko kwenye mipaka, ni eneo jipya limekuja kwa miaka 20, ni jinsi gani nchi inaweza kufaidika kiuchumi, na hadi hivi sasa tayari meli nyingi zinakwenda. Nilizungumza mwanzo katika *records* ambazo nilizisoma katika...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, eneo hilo liko wapi unalosema wewe?

Mhe. Simai Mohammed Said: Liko katika mipaka Mashariki mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambalo liko katika *220 met miles*, ni mbali. Ni eneo ambalo limepangwa chini ya *low of the sea* chini ya Umoja wa Mataifa, nchi ambazo wanaweza kufaidika kiuchumi dhidi ya rasilimali zao.

Sasa mimi ninachokisema ni kwamba, labda hii ni kwa ajili ya ku-*save* Baraza, ametoa rai nzuri tuweze kukaa naye kushauriana. Ninachokiomba yeye kwa upande wake kutokana na uzoefu, ametoa hotuba ndefu sana na nimeridhika nusu ya maelezo yake, ninachokitaka ni kwamba tupate *commitment* ndani ya Baraza, ni kwamba SMZ itafaidikaje katika siku za mbele kwenye eneo hili la *EEZ*, atuletee na atufahamishe, ikiwezekana tuje tufanye semina ya pamoja ili Zanzibar iweze kufaidika katika eneo hilo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti...

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mhe. Miraji Khamis, nilimuona Mhe. Waziri wa Fedha, alikuwa na maneno kidogo anataka kuongezea hapo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kidogo kuliweka sawa, kama alivyolisema Mhe. Waziri, anayehusika na sekta. Nilitaka kumfahamisha Mhe. Mjumbe kwamba, eneo la *EEZ* ni eneo ambalo limetolewa kwa *United Republic of Tanzania*. Kwa hivyo, sisi kama Zanzibar kwanza hatuna uwezo huo kisheria kulitoa hilo eneo au kulikodisha. Lakini kama alivyosema Mhe. Waziri, faida inapatikana kutokana na kutoa leseni za uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, serikali yenyewe ina mpango, kuna programu maalum inaandaliwa kwa ajili ya kusaidia vijana wetu kuingia katika biashara ya uvuvi wa bahari kuu. Nilitaka kuliweka sawa hili.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia yangu nilimuuliza Mhe. Waziri, kuhusu *Smart Fishing,* yaani Mradi wa Uhifadhi wa Samaki na Ubora wa Dagaa, anipe maelezo kwa sababu serikali ilichukua jitihada kubwa ya kutoa elimu kwa Unguja na Pemba. Lakini sasa hivi kama kuna msitu mkubwa katika mradi huu. Nataka maelezo tu ili nijiridhishe katika eneo hili.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mhe. Mjumbe kwamba, kwenye *Smart Fishing*, programu kwanza zipo zinaendelea, ni *area* ambayo bado fedha zake zipo na ni mradi unaendelea, ila kuna kipindi fulani tu tulikuwa tumesimamisha tu *crane*, lakini programu baada ya kupitisha bajeti hii zitaendelea kama kawaida, cha msingi ni kwamba tuna *train* watu, tunachoomba tu baada ya kuwa-*training* watu basi watekeleze yale ambayo tulikubaliana katika *training*. Lakini nasema kama ana jambo la ziada zaidi ya hili, basi tunaweza kukaa pamoja akatuambia yeye anaona kuna eneo gani ambalo lina kasoro katika utekelezaji wa mradi huu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tumeshamaliza Waheshimiwa Wajumbe, hoja tatu zimeshakwisha. Tuendelee.

Kifungu SN 010401	Programu Ndogo ya kuimarisha ufugaji wa mazao ya baharini	4,285,734,000

Kifungu SN 010402 Programu

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia tena na nimekua nazungumzia kwa hisia za ndani mpaka moyo wangu unauma, kuhusu suala zima juu ya uvuvi unaofanywa baharini hasa katika eneo la *PECA* na kusini mwa kisiwa cha Unguja eneo la Kizimkazi kupiga mabomu. Mimi ninachokiomba kitu kimoja, kwa sababu huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani na nilishalizungumza sana na waziri ametoa maelezo mazuri.

Ninachokiomba hapa Mhe. Waziri, kwa sababu eneo la mazingira si eneo la Muungano, lakini bahari hii tunafaidika sote kwa pamoja; upande mmoja ni sisi kwa Zanzibar na upande wa pili ni Muungano. Sasa ninachokiomba Mhe. Waziri, anipe ahadi yake kwamba atashirikiana na waziri husika kwa upande wa Tanzania Bara wa Jamhuri ili kukomesha uvuvi wa mabomu, kwa sababu hili eneo sasa hivi kila siku mabomu sita au saba mpaka nane yanapigwa kwa kutumia *dynamite* Kusini mwa Unguja na eneo la *PECA*. Watu wanasikia Kaskazini Pemba, watu wanasikia Kusini Unguja, nao ni watu kutoka Unguja na Pemba wanatumika kutoa taarifa. Lakini katika mazingira hayo hayo hao wanaofanya *patrol* kwenye boti zetu sasa hivi kama hao KMKM na wengine hawana mafuta wala chochote ambacho kitawasaidia huko.

Mhe. Mwenyekiti, ninachokiomba waziri anipe maelezo kidogo mazito, ambayo angalau yatanipa moyo kwamba katika miezi ya mbele hili jambo angalau sasa tutanza kuliona linapungua na tunalishinda hawa wanachotufanyia.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme tu kwamba suala la uvuvi haramu bado linaendelea, pamoja na kulipiga marufuku kwa nguvu zetu zote na hili ni moja katika tatizo ambalo tungeomba kabisa tusaidiane sote kwa pamoja. Nilikutana na wavuvi nikawaeleza wanadai vyombo tuwasaidie zana na kadhalika, lakini hata sehemu ambazo tumeweka haya matumbawe ya *artificial*, samaki wako wengi wanazaliwa kwa wingi, lakini bado watu wanakwenda kufanya hujuma pale, tena tabia za watu wetu ni za ajabu sana, kitu ambacho kitakusaidia wewe na familia yako unaweza ukaki-*destroy*.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niliseme hili alipokuja Amir wa *Qatar* kutoka Dar-es-Salaam, alizamia baharini kwenda kuangalia viumbe tu vya bahari vilivyokua huko chini. Ile *deep sea* tunayoiona sisi kwao wao ni rasilimali muhimu sana. Halafu unakwenda unapiga mabomu unaharibu. Kwa hivyo, lipo tatizo la msingi la watu wetu, wanafikiri utajiri wa haraka ni kupiga mabomu. Nataka nikubaliane naye kwamba hili tatizo lipo.

Tatizo la pili ambalo lilikuwepo ni vifaa vyetu vilikuwa vimechakaa vingine. Sasa hivi katika programu utaiona hii, boti tunazifufua zote na tumeshazungumza na KMKM tushirikiane kwa nguvu moja kwenda kupambana na watu hao wanaopiga mabomu kwenye maeneo yetu ya samaki ambayo tunayatunza sasa hivi.

Jambo la tatu nasema, cha msingi sasa hivi ni kushirikiana sote sisi viongozi, kwa sababu watu hawa hawako mbali wako hapa hapa katika maeneo yetu, wanafanya, wanakwenda na wanarudi. Mengine wameyageuza hata ya kisiasa katika maeneo mengine tumekwenda wanafanya, na tumekasirika sana na hili jambo. Lakini nasema ni lazima tujitahidi kutunza rasilimali, kuna mapato makubwa sana ndani ya bahari kama tutatunza vianzo vyetu vizuri. Vyanzo vile vya kuzalia samaki kama hatukuvitunza basi hali yetu itakua mbaya sana Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, nakubaliana naye, tutazidi kushauriana, lakini na juhudi tutachukua zaidi tuweze kupambana na wavuvi hawa haramu.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Mhe. Mwenyekiti, unajua ningeweza kwenda zaidi kwa undani, lakini nafikiri maelezo mengi hayo ya waziri yanatosha. Lakini ninachokiomba atuletee *some sort of proposal* kwa wajumbe wote na wizara yake ikae karibu, kwa sababu tunachokiongelea sisi sasa hivi hapa, nataka nifahamike ni vizazi vya mbele vitakuja kutulaumu sote tuliokaa humu ndani, mabomu yanazidi kupigwa kila siku ndani ya bahari kote, matumbale yanazidi kuharibika. Sio hao watu wanakuja kuangalia ni kwamba tunaua hapa *the future generation* watakosa kula na kufaidika na hii rasilimali.

Kwa hivyo, anachokifanya Mhe. Waziri, kwa sababu yeye anasema atajipanga, lakini naomba katika kujipanga kwake atambuwe kwamba ni lazima am-*commit* Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hili, kwa sababu pia wanaotoka kule ni upande pia wanatoka Tanzania Bara kuja kupiga bomu, naomba hapo anipe kauli yake ili tuweze kuendelea.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mapema, tutashirikiana na vikosi vyetu vyote vya ulinzi na usalama. Kwa upande wa hapa Zanzibar KMKM na kwa Tanzania Bara ni ile *Marine Unit* ilioko kwenye Jeshi, ili kuhakikisha kabisa tunapambana na hili jambo. Tunao ushirikiano baina yetu na Bara katika jambo hili, kwa sababu hii ni rasilimali za nchi zote lazima tuzilinde, namuhakikishia kabisa hiyo kazi itafanyika kwa ufanisi mkubwa sana, tuko *serious* katika kupambana nayo.

Vile vile, sasa hivi ukiangalia katika huu ukanda wetu wa *Indian Ocean*, tunazo taasisi ambazo zinasimamia kabisa suala zima la uvuvi haramu unaotokea katika bahari zetu, hizi Bahari Kuu au bahari nyengine. Kwa hivyo, nasema tutatumia mbinu zote na taasisi zote hizi ili kuhakikisha tunapambana. Lakini

linabaki sisi kama binadamu kuthamini rasilimali hii alizotupa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti: Alitaka kufahamu unamu-*engage* vipi waziri mwenzio *counter part* wako katika suala hili.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Nasema tumeshapanga na tunavyo vikao viwili vya mawasiliano vya serikali, mimi mwenyewe nimeshamuandikia Mhe. Waziri Mchemba, tunahitaji kukaa na kuangalia Sheria ya *deep sea*, kuangalia vile vile mazingira haya ya uvuvi haramu na kadhalika. Tunangoja tu muda muafaka tutakaa baada ya kupitisha bajeti, nao kupitisha bajeti yao ili tuweze kulifanyia kazi.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba swali la mwisho, nashauri kwamba atakapokuja pia atayarishe na sheria nidhamu na jinsi gani wataweza kudhibiti hili jambo na kuweza kutoa adhabu ya nguvu kutokana na jambo hili linalokuja. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Khamis Bakar(Doholo): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokua nikichangia nilimuuliza Mhe. Waziri, kwamba Tumbe sote tunajua kwamba kuna soko lilijengwa pale, lengo na madhumuni ni ya wizara hii, limeainishwa hasa soko la samaki na mboga mboga na soko lile huu ni mwaka wa pili limekaa tu pale linaota mkoga. Sasa, je, nilimuuliza ni juhudi gani atazichukua kuona kwamba lile soko linatumika ili serikali ijipatie mapato yake na wananchi waendelee kulitumia lile soko.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Mjumbe, tushirikiane pamoja niende nikaiangalie hali halisi. Kuna siasa zilichezwa pale, tuka-*deal* na hizo siasa, tumalize nazo ili soko liweze kufanyakazi.

Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo): Mimi nakubali licha ya changamoto zilizopo, *Insha Allah* naomba tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, eneo hili naomba sana Mhe. Waziri, tukae nae, mimi nakubaliana na ile hoja aliyoizungumza Mhe. Simai Mohammed, eneo hili linataka utafiti wa kina. Lakini lipokua nikichangia Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza kwamba hii Sheria ya uvuvi ambayo tulipitisha hapa mwaka 2010. Sheria hii ilieleza vivuri na nikazungumza kile kifungu kinachompa nguvu *director* katika ku-*control* yale masuala ya *conservation*, na

zile nyengine na ndio maana mpaka akaunda zile *communities* ambazo zilikua zinasaidia mpaka katika hii *patrol*.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kutokana na kanuni ambayo iliyotungwa na ndio maana nikasema Mhe. Waziri, hili itabidi nitakuja kuomba baadae tukae nae ili tuangalie namna gani ya kuweza kulisaidia. Ndio iliyokuja kuuwa nguvu hata ya *patrol*, na nilisema pale kulikuwa na maboti zaidi ya 10 yalikua yanasimamiwa na Idara ya Uvuvi, yalikua ndio yanasaidia kwenda katika *patrol* wanasaidiana hivyo vyombo vingine. Wananchi wanapewa simu za mkononi pamoja na vifaa vyengine vya mawasiliano ili kutoa taarifa kwa hao wavuvi wanaotoka Tanzania Bara waliokuja kupiga mabomu. Leo kutokana na hii idara kupunguzwa nguvu ina maana yale mambo sasa hivi yameachiwa maharamia wanafanyakazi.

Sasa hebu katika hili Mhe. Waziri, amejipanga vipi katika kusaidiana ili kuipa tena nguvu hii idara kuweza kufanya *monitoring* pamoja na *patrol* na kuweza ku-*control* huu uvuvi haramu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka kusema jambo moja, sisi hapa tunapitisha sheria na sheria wakati wowote haiwezi kuwa kubwa kuliko kanuni. Kwanza tufahamu kanuni inatokana na sheria, hilo la kwanza. Pili, kusoma *Finance Act, Accounting Officer* wa Wizara ni Katibu Mkuu wa Wizara na sio Mkurugenzi, na ndio tatizo moja ambalo nimelikuta mule, kwamba watu wana *powers* kubwa kutumia bila Katibu Mkuu hata kujua.

Kwa hivyo, nikakataza kabisa na nakataa, sheria tumeipitisha hapa *The Accounting Officer* ni Katibu Mkuu ndiye tume-*summon* kwa matumizi ya fedha kwenye *Public Account Commitee*, Mkurugenzi ni msaidizi wake tu, sasa tunataka kufanya mambo ya kienyeji haya yatatugharimu. Mimi nimeona, tumekwenda pale tumekuta sisi pesa nyengine zinavyotumika nje ya utaratibu, tukakataa. Kwa hivyo, naomba kabisa tuheshimu, mimi naheshimu sheria na taratibu tulizokubaliana. Tumekubaliana *The Accounting Officer* wa Wizara ni Katibu Mkuu wa Wizara, *serious*, mpaka mtakapobadilisha sheria mkasema *Accounting Officer* sasa sio yeye nitakubali, yeye tena anatoa sasa katika mafungu haya wewe kasimamiye na utakaposimamia utakapofanya matumizi lazima nijue, ndicho kinachokosekana hicho.

Pili, sio kweli kwa sababu hiyo ndio maboti yamekuwa mabovu, hapana, kuna mambo mengi yametokea hapo katikati tutakwenda kuyasawazisha tuacheni tukayasawazishe, kuna majipu lazima tukayatumbue tu, tukubaliane. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kuna asilimia 70 na 30, asilimia 30 wanatakiwa ziachwe kwenye *Community*, lakini kuna wengine wanakusanya hizo pesa bila ya risiti na bila ya utaratibu, kwa hivyo, kuna mambo mengi waheshimiwa naomba tupitishe hii bajeti tutakuja kukaa pamoja, tutakwenda kwenye Kamati na tutakuja kuwaarifu moja baada ya moja ambalo tunalifanya kurekebisha kasoro hizi. Naomba sana Mhe. Hamza, ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, tumemuelewa sana Mhe. Waziri na hii sheria kama nilivyosema iko wazi sana na inajieleza vizuri, lakini vile vile hii Kanuni nayo inajieleza lakini bado kuna kitu kama *Contradiction*, lakini mimi nafikiri hoja yangu iko hapa. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hilo tatizo lililotokea pamoja na kwamba Mhe. Waziri, anasema maboti hayakuharibika kwa kiasi hicho, lakini si hayo maboti tu mpaka zile huduma za wavuvi sasa hivi, ina maana zile fedha kutoka huo mdorongo wa kwenda kwa Katibu Mkuu mpaka kuja huku chini zinakuwa zinakosekana kwa ule muda muwafaka. Kwa hivyo, ina maana hili ndio linasababisha, hata zile kamati za uvuvi kushindwa kutoa taarifa kwa wakati, yale maeneo yale kama nilivyosema, yale maboti ya *patrol* ambayo Mhe. Waziri, nilimuuliza yako mangapi na sasa hivi mangapi yanayofanya kazi ndio hayo yamelala.

Sasa labda basi angelinambia hiyo sababu haya maboti ambayo yalikuwa yakifanya kazi kipindi hicho kwa vizuri na sasa hivi hayafanyi kazi kuna tatizo gani wakati fedha zinakusanywa?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme tu kitu kikiwa kipya kitaendelea kufanya kazi na kikichoka lazima kitengenezwe, huwezi ukanambia boti ya mwaka jana ambayo ni mpya imefanya kazi hata kama kulikuwa na Mkurugenzi au hakuna Mkurugenzi kuna pesa, madhali ni mpya itaendelea kufanya kazi na ikichoka kama haikufanyiwa *Maintenance* na ndio tatizo la msingi, hayakufanyiwa *Maintenance in time*, ndicho nilichojifunza mie, kwamba vitu hivi vimeharibika havikufanyiwa *Main tenance in time.*

Kuna *pump* moja hapa ya *irrigation* imekaa miaka miwili na nusu, inakhitaji milioni kumi na tano wakulima 540 hawafaidiki kwa sababu milioni 15 *pump* imelala miaka miwili na nusu, *Maintenance* ya milioni 15 unawazuia wakulima wasipate huduma, kwa nini? Kwa hivyo, yapo mambo mengi tunahitaji kuyafanyia kazi, ndio maana nasema naomba tushirikiane na Baraza tushirikiane na Wajumbe wa Baraza tuondoe hizi kasoro hizi, sio hili tu alilioliona Mhe. Hamza, kuna mengi sana tutakuja kukaa pamoja, tutayatatua

kwa pamoja ili tupate maendeleo ya nchi yetu, yapo mengi sana tutakuja tuyazungumze.

Lakini nakubaliana na yeye kabisa kunahitaji kufuatilia hili jambo, tuone kabisa meli ngapi zinafanya kazi na ngapi hazifanyi kazi. Boti ngapi zinafanya kazi, hivi sasa ziko kama boti 5 zimeshatengenezwa na nyengine tunaendelea kuzitengeneza, lakini tukipitisha bajeti hii tutaweza kuzimalizia na nyengine kuzitengeneza, lakini bado suala la msingi ni kwamba *Maintenance* katika utaratibu wetu wa kazi nalo hatulizingatii sana. Pili, suala la usimamizi na la tatu, kuhakikisha kabisa ile rasilimali chache inayopatikana inakwenda pahala panapotakiwa, tukifanya hayo Mhe. Hamza, hatupigishani kelele tena na jambo hilo. Ahsante sana nakushukuru.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri wacha tumpe muda Waziri ili aende akatengeneze huo utaratibu, lakini kikubwa zaidi tunachokiomba bado kama ile hoja aliyoizungumza Mhe. Simai, ukiacha yale mambo ya kukaa na kuzungumza na Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kuna umuhimu wa boti zetu za *patrol* kuweza kutengenezwa kwa haraka ili zikaweza kudhibiti huo uvuvi haramu na ikaokoa hiyo rasilimali ya nchi. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu SL 010402	Program ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Hifadhi za Baharini	15,130,993,000
	JUMLA	**19,416,727,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo Juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

KIFUNGU PL 0105 PROGRAMU KUU YA MIPANGO NA USIMAMIZI WA KILIMO MALIASILI MIFUGO KILIMO NA UVUVI

Kifungu SL 0105

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ni mjumbe wa kamati, sina lengo la kutaka kuisumbua na kupiga buti kwa Mhe. Waziri katika kumtatiza masuala yake, lakini kwanza nimshukuru kwa dhati kwa namna ambavyo aweza kufanya *Presentation* yake katika masuala mbali mbali na kwa kweli tumpongeze kwa dhati kabisa, na sikutegemea kama kutakuwa na buti katika Wizara yake.

Lakini kuna jambo nilichangia kidogo mambo mawili, matatu kwa maandishi; nilichangia juu ya suala zima la watumishi kwamba, Wizara yake inaongoza kwa kufanya shughuli za siasa baada ya utendaji wa kazi, nililieleza *direct* kabisa, baada ya kufanya utafiti na kuangalia mustakbali wa Mhe. Rais, kwa sababu Wizara hizi mwanzo zilikuwa ziko tofauti, ilikuwa Kilimo na Misitu, nikaona Mawaziri, Manaibu na Makatibu wote wameondoka, *source* ilikuwa watu wanafanya kazi ya siasa zaidi kuliko shughuli za maendeleo. Kwa bahati na yeye mwenyewe kaelezea vizuri kwamba hilo kaliona na atalifanyia kazi.

Sasa kabla ya kumpongeza yeye, kwanza nataka kumpongeza Mhe. Haji Omar Kheir, baada ya kupata maagizo ya Mhe. Rais ya kuondosha ng'ombe mjini, *within three days* ng'ombe mjini hakuna, nimpongeze kwa dhati. Kwa hivyo, nataka kujua na yeye Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ndani ya muda gani watu ambao mpaka sasa hivi na nilizungumza kwa sababu nawajua na wanaendelea. Ndani ya muda gani watu ambao wanaacha kufanya kazi, wanafanya shughuli za kisiasa ndani ya Wizara yake atawapatia ufumbuzi au atatumbua majipu yao.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niwashukuru sana wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, mikutano miwili niliyofanya nao kazi ilibainika kabisa wafanyakazi hawa walikuwa wakati mwengine hawakupata maelekezo mazuri, walikuwa kato, lakini baada ya kukaa nao wote kabisa wamekubali kabisa kuna haja ya kuchapa kazi. Kila unapokutana nao wanachodai ni kimoja tu dhana za kufanyia kazi na fedha za kufanyia kazi, kwa hivyo, wakati mwengine unaweza kukuta watu wanapiga soga, lakini kwa sababu hawana zana za kufanyia kazi. Nilikwenda hapa Matrekta nikawakuta mafundi wamekaa, nikawaambia mbona mmekaa mnazungumza, wakaniambia sisi ni mafundi tunataka kutengeneza hatuna vipuri Mheshimiwa, twambie kuna vipuri tukafanye kazi? Watapiga soga.

Sasa nasema yapo mazingira mengine lazima tukubali kwamba yanasababisha watu kufanya mambo ambayo hayatakiwi, kazi yetu kubwa ni kuhakikisha watu wetu wanafanya kazi na tumegawana mipango ya kazi na nakuhakikishia kabisa baada ya mikutano hii miwili vijana wengi sana wamerudi kwenye mstari na tunafanya kazi, kama unamgundua mwengine yeyote hafanyi, tafadhali tuambie tutachukua hatua zinazostahiki.

Mhe. Ali Salum Haji: Nakushukuru Mhe. Waziri, kwa majibu mazuri, nataka nimuahidi kwa sababu sisi ndio kazi yetu na mimi ndio msimamizi mkuu wa kusimamia Ilani ya Chama cha Mapiduzi ndani ya Serikali hii, tutamsaidia na tukiwabaini tutampelekea, Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, mimi niliulizia nilipokuwa nikichangia hotuba ya bajeti yake, nilisema Zanzibar tumekuwa tunaliongelea suala la uvuvi wa bahari kuu, lakini hata Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu Zanzibar hatuna. Lini sheria ya bahari kuu italetwa barazani?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Mheshimiwa, Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu ipo na SMZ inafaidika na kuwa na asilimia 40%, lakini Makao Makuu ya uvuvi wa bahari kuu yako Zanzibar na Wakurugenzi wake wanavyoteuliwa kila miaka mitatu akitoka Bara, miaka mitatu anatoka Zanzibar, tulikuwa na Mkurugenzi Zahoro kamaliza muda wake sasa hivi kuna Mkurugenzi kutoka Bara na yeye akimaliza muda wake anakuja kutoka Zanzibar, tunafaidika sana Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ina maana sheria tuliyonayo ni Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au tuna Sheria ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Tumekubaliana kabisa *Deep See Authority* ni suala la Muungano na linapitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano, Baraza hili kazi yake ni kuja tu kufanya *Endorsement* baada ya kupitishwa kule, hiyo ndio *process* ambayo inaendelea hivi sasa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante tuendelee.

Kifungu SL 010501	Program ndogo ya utawala na uendeshaji wa Kazi za Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi	1,752,406,000

Kifungu SL 010502

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimpe pongezi Mhe. Waziri wa Kilimo kwa kazi nzuri aliyotuonyesha ataifanya, mimi wakati wa kuchangia kama nilitoa mawazo, kwa sababu wakati mengine lazima tunakumbushana, unajua hapa Zanzibar hasa maeneo yetu ya *Town* haya mashimo ya maji ambayo nilijaribu kumwambia, nikatoa mfano Mwanakwerekwe na mengine, tumeyafanyia utafiti gani kwa sababu yale ni kama tuseme ni mambo ya Mungu yale mashimo shimo, hatuwezi kusema Zanzibar kwamba tutapata mvua za kila mwaka, sisi inaweza kufika mwaka mzima tusipate mvua na yale mashimo tunayafuata sisi kuyajenga, sio kama mashimo yanamatatizo.

Nili mwambia Mhe. Waziri, ana mawazo gani na tafiti gani kuhusu haya mashimo ambayo tunaona kama ni adui kwetu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana nae kabisa kuna haja ya kufanya utafiti kujua kama haya mashimo yaliiyopo tunaweza kuyatumiaje. Juzi nilikuwa napita pale Bwawani kwenye Msikiti wa Mabluu pale, nikamuita mtaalam mmoja wa *Fisheries* nikasema kwa nini tusipande samaki hapa tukazalisha samaki tunaacha bwawa lile linakaa bure. Kwa hivyo, yapo maeneo mengi ya aina hiyo tutayaangalia ili tuone kama tunaweza kufanya hivyo, nakubaliana na ushauri wake tufanye utafiti Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Na mimi Mhe. Mwenyekiti, naomba nizuie kidogo kwamba wakati nilipokuwa nikichangia katika kipengele cha sera na utafiti nilisema kwamba, katika kipindi kilichopita kulikuwa na mradi wa vijana ambao uliwasaidia wafugaji mbuzi katika Wilaya ya Micheweni, kama sikosei nadhani Shehia kama tano au kumi, lakini nilitaka kujua kwamba shughuli hii au mradi huu umetoa matokeo gani katika tafiti hizo, kwa sababu lengo ilikuwa ni kuimarisha vijana ambao wamemaliza masomo yao *Form 11* na badala yake kuwawezesha ili kuweza kujiongezea kipato.

Sasa tunataka tuone matokeo, nilitaka Mhe. Waziri, anieleze hatua ambayo tumefikia kwa sasa hivi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na programu hizo na bado zipo zinaendelea za kuwafundisha vijana ambao wamemaliza *Form 11* na *Form 111* kama mlivyoshuhudia karibuni hivi tumeweza kuwakabidhi hata baskeli za kuweza kufanyia kazi zao, ndio tunataka tuwageuze wengine kuwa mabwana shamba na bibi shamba kwa sababu ya kusaidia katika programu kama hizo.

Kwa hivyo, nakubaliana na Mheshimiwa, kuna haja kuiangalia tena hii programu ili iwasaidie hasa watu wako wa Micheweni, eneo la Micheweni linahitaji kusaidiwa sana, ni eneo ambalo mara nyingi Zanzibar hapa tunapata upungufu wa chakula kutoka Micheweni, kwa hivyo, kuna haja ya kuliangalia, tutakaa na Mheshimiwa, ili tuone namna gani kama ana vijana zaidi tuweze kuwachukua na kuwaingiza kwenye programu zetu hizi ili tuweze kuisaidia Micheweni.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mheshimiwa, katika eneo hilo hilo kulikuwa na tafiti mbili ambazo niliuliza na moja iliyofanya ni kwamba kuangalia jinsi ambavyo tunaweza kuona kwamba tunaweza kuboresha mifugo ya mbuzi katika maeneo ya Micheweni, ambayo tafiti hiyo imeendeshwa na Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa kushirikiana na wafadhili wengine. Kwa hivyo, pia napo nilitaka kujua kwamba matokeo ya tafiti ni lini wananchi wa Jimbo la Micheweni watapata kujua matokeo ambayo yameweza kufikiwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, baada ya shughuli zetu za baraza hili nitamtafuta nitakaa na wataalam ili tujue ile programu hasa imefikia wapi na imesaidiaje.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu SL 010502	Program ndogo ya Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi	14,800,449,000
Kifungu SL 010503	Program ndogo ya uratibu wa kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Ofisi Kuu Pemba	2,963,792,000
	JUMLA	**19,516,647,000**
	JUMLA KUU	**48,977,300,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha za Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali Makadirio hayo na liyapitishe.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa naomba sasa niwahoji wale wote wanaokubaliana na Hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nami niungane nanyi kumpongeza Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi, kwa uwasilishaji wake wa hoja na namna alivyoweza kujibu hoja mbali mbali za Wajumbe, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana kwa aina ya staili yake alivyohitimisha hii hoja, napenda nimsifu kwa sababu hakupata ule muda wa kukaa na wataalam ili kuweza kupata hizi *data* za kukupeni majibu. Lakini kama alivyosema mwenyewe ameahidi kwamba wale wote ambao wametoa hoja atakuleteeni kwa maandishi na atakuwa mara kwa mara anakupeni matokeo ya hatua ambazo atakuwa amefikia katika shughuli ambazo mtakuwa mmependekeza zifanyike.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa sababu muda ushakwenda sana naomba sasa nichukue nafasi hii kuakhirisha shughuli za Baraza mpaka kesho siku ya Ijumaa.

(Saa 10.16 jioni Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 10/6/2016 Saa. 3.00 Asubuhi)